# DHIMA YA UTAWALA WA NABONGO MUMIA KATIKA MAENEZI YA LUGHA YA KISWAHILI UBUKUSUNI, MKOANI MAGHARIBI (KENYA)

**TASNIFU YA**

**ANDREW W. NAKHISA**

**Imetolewa kwa Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta**

**2009**

Nakhisa, Andrew W.
*Dhima ya utawala waa Nabongo Mumia katika*
2009/339398

**UNGAMO**

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine"

______________________ 4/6/09

NAKHISA W. ANDREW TAREHE

(MTAHINIWA)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Kenyatta"

______________________ 8/6/2009

DKT. RICHARD M. WAFULA TAREHE

______________________ 8/6/2009

PROF. IRERI MBAABU TAREHE

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa Babangu Jephneah Nakhisa Manyololi Kusimba na Mamangu mpendwa Hellen Nekoye Kusimba. Mlinionyesha utamu wa kusoma na basi kunirithisha uchu wa kupenda elimu.

Mke wangu mpenzi na Mwandani Janet Khakasa Kusimba na watoto wetu Vicky, RoyBevan, Latoya Noel, Marvin na kifunga mimba Ian, nawashukuru mno. Mlinitia ari na matamanio ya kuendelea na masomo yangu.

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati ni kwa Muumba kwa ulinzi wake. Amenipa uhai na ari ya kufanya kazi ili nijiendeleze kimasomo. Mambo yalinipowia magumu, upako wake ulininusuru.

Shukrani kwa wasimamizi wangu Dkt. Richard M. Wafula na Prof. Ireri Mbaabu kwa uelekezi wao uliosheheni busara na hekima. Safari hii ya usomi ingekwama kama haingekuwa mwongozo wao. Ushauri wao uliniwezesha kudhibiti chombo kisiende mrama.

Wahadhiri wangu katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika walinifaa zaidi. Walinitia hamasa tangia kipindi cha kutayarisha pendekezo la utafiti hadi tamati. Wahadhiri hawa ni Bw. Peter Mugambi (Mwenyekiti wa Idara), Dkt. Alic Mwihaki (Kaimu Mwenyekiti), Dkt. Sheila Ryanga, Dkt. Clara Momanyi, Dkt. Petronilla Mathooko, Bi. Miriam Osore, Bi. Hannah Gathenji, Dkt. Edwin Masinde na Bi. Everlyn Mudhune.

Tume ya kuwaajiri walimu (T.S.C) ambayo ni mwajiri wangu inastahili pongezi. Likizo ya miaka miwili niliyofadhiliwa ilinifaa ajabu. Nafasi niliyopewa ni ishara kamili kuwa tume hii inastahi lugha ya Kiswahili.

Kakangu Profesa Chapurukha M. Kusimba, nakuombea dua ya Mwenyezi Mungu. Ulinitia ari nikajazwa na jazba ya kusoma. Ilhamu uliopalilia ndani ya nafsi yangu,

iliniwezesha kufua dafu. Isitoshe, ulijitolea kwa hali na mali na kulipia masomo yangu. Chambilicho Shaaban Rovert, "Ni macho gani yasiyolengalenga kwa machozi ya furaha kwa ukarimu kama huo"? Ndugu James W. Kusimba, kutoa ni moyo, usambe ni utajiri. Utafiti wangu ulifanikiwa kwa sababu yako. Asante. Dadangu Clare Naliaka Kusimba, haba na haba hujaza kibaba. Shukrani kwa msaada wako ulionihakikishia nafasi yangu chuoni.

Namshukuru rafiki, mwandani, mwenzangu, mke wangu mpendwa Janet Khakasa Kusimba aliyeniauni kwa hali na mali. Alivumilia upweke nilipokuwa mbali naye huku akiniombea ili nisilegeze kamba.

Kadhalika, nawashukuru wanafunzi wenzangu, Muange 'Mkamba Mwema', Mumbua Jane, Ngugi Bonface, Ojenge Hellen, Njurai Felicity na Muinde Sarah. Tulifika, tukatalii, na takayafaridi 'majambo' pamoja. Shime tuliyotiana wakati bahari imechafuka huku barabara ni telezi, haipigiwi mfano. Kumbuka wenzangu msemo tuliotaniana "Ndo mkoko umealika maua tu". Zama zaidi.

Shukrani ziwafikie Bi. Mary Khaemba, Bw. Geoffrey Khamala kwa kupiga chapa kazi hii. Sheila M. Ozengo, heko kwa kuhakikisha kuwa ujalidi wa tasnifu hii unadhibitiwa inavyopasa. Tajriba yako ilinifaa sana. Ahsante. Siwezi kusahau wakurugenzi wa New Kamusinga Studios na Printers, wakiongozwa na Bw. J. O. Mulama na Bi. Aggie Mulama kwa kunifadhili kwa njia ya chapa na vifaa vyote vya utafiti. Hongera kwenu.

# IKISIRI

Utafiti huu umeeleza na kuchanganua dhima ya utawala wa Nabongo Mumia katika maenezi ya lugha ya Kiswahili Ubukusuni, Magharibi mwa Kenya. Utafiti huu ulijikita katika kipindi cha utawala wa Nabongo Mumia tangu kutawazwa kwake kama Chifu Mkuu, mnamo mwaka wa 1910 hadi kifo chake katika mwaka wa 1949.

Katika utafiti huu, tutalenga kuainisha, kueleza kuchunguza na kuchanganua mikakati iliyotumiwa na Nabongo Mumia kuchangia maenezi ya lugha ya Kiswahili. Katika kulifafanua swala la utawala, misingi iliyowekwa ili kufanikisha maenezi ya lugha ya Kiswahili iliangaliwa. Maendeleo na mabadiliko yaliyojikita katika asasi muhimu kama dini, biashara, ndoa na maingiliano ya kijamii kwa kuitumia mizani ya mifanyiko ya kijamii yalichangia maenezi ya lugha ya Kiswahili Ubukusuni. Lugha ya Kiswahili ilipata hadhi kubwa katika kipindi hiki kwa sababu iliendesha shughuli nyingi za Nabongo Mumia ambaye alikuwa mshiriki wa karibu wa mkoloni. Utafiti huu basi umebainisha nafasi muhimu ya utawala wa Nabongo Mumia katika kuwekea lugha ya Kiswahili msingi thabiti wa kuenea Ubukusuni.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi imeshughulikia swala la utafiti, sababu za kuichagua mada, upeo wa utafiti, madhumuni ya utafiti, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za mtafiti. Sura ya pili imechunguza historia ya jamii mbili – Ababukusu na Abawanga – hasa jinsi walivyoingiliana na kuathiriana. Sura ya tatu inaangalia dhima ya utawala wa Nabongo Mumia katika maenezi ya Kiswahili. Sura ya nne imeangazia asasi nyinginezo kama dini,

mahakama, ndoa miongoni mwa nyingine. Mwisho, sura ya tano ni hitimisho. Mtafiti ametoa muhtasari, matokeo kuhusu utafiti, mapendekezo ya utafiti zaidi na matatizo yaliyokumba utafiti huu.

Kutokana na utafiti huu imedhihirika kwamba utawala ulichukua nafasi muhimu zaidi katika maenezi ya lugha ya Kiswahili Ubukusuni. Pili, utafiti huu umeonyesha kwamba Babukusu walikuwa wategemezi kwa kuwa katika kuitumia lugha ya Kiswahili, walianza kuunga mkono utamaduni wa kigeni. Mwisho, asasi kama ndoa, dini, biashara, mahakama za Kiafrika, elimu, muziki, michezo na miundo misingi ilifanikiwa Ubukusuni kwa sababu ya kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa kiasi kikubwa asasi hizi zilifanikishwa na utawala wa Nabongo Mumia.

## YALIYOMO

Ungamo .................................................................................................... ii

Tabaruku.................................................................................................. iii

Shukrani.................................................................................................. iv

Ikisiri........................................................................................................ vi

Yaliyomo .................................................................................................. ix

Ufafanuzi wa Msamiati ............................................................................ ix

**SURA YA KWANZA** ............................................................................ **1**

1.0 Utangulizi ............................................................................................ 1

1.1 Swala la Utafiti .................................................................................... 3

1.2 Malengo ya Utafiti ............................................................................... 4

1.3 Sababu za Kuchagua Mada ................................................................. 4

1.4 Nadharia Tete ....................................................................................... 5

1.5 Upeo wa Utafiti.................................................................................... 6

1.6 Msingi wa nadharia .............................................................................. 6

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ............................................................. 13

1.8 Mbinu za Utafiti.................................................................................... 17

1.8.1 Utafiti Maktabani ............................................................................. 17

1.8.2 Utafiti wa Nyanjani .......................................................................... 18

1.8.3 Kuchanganua Data ........................................................................... 20

Kiishilio ..................................................................................................... 20

**SURA YA PILI**........................................................................................ **22**

2.0 Utangulizi ............................................................................................. 22

2.1 Historia ya Babukusu ........................................................................... 22

2.2 Historia ya Abawanga .......................................................................... 36

Hitimisho ................................................................................................... 43

**SURA YA TATU** ..................................................................................... **44**

3.0 Utangulizi ............................................................................................. 44

3.1 Nabongo Mumia ................................................................................... 44

3.2 Msingi wa Utawala wa Nabongo Mumia .................................................. 47
Hitimisho .................................................................................................... 65

**SURA YA NNE** ........................................................................................ **66**
4.0 Utangulizi ............................................................................................. 66
4.1 Uzalendo, Mwamko wa Kisiasa Ubukusuni .......................................... 66
4.2 Mahakama za Kiafrika .......................................................................... 78
4.3 Ndoa ya Mseto ...................................................................................... 83
4.4 Biashara Ubukusuni ............................................................................. 87
4.5 Nafasi ya Dini ....................................................................................... 90
4.6 Reli ....................................................................................................... 97
4.7 Ajira ...................................................................................................... 99
4.8 Michezo ................................................................................................ 101
4.9 Muziki .................................................................................................. 103
4.10 Usetla .................................................................................................. 105
4.11 Vita vya Kwanza na vya Pili ............................................................... 109
4.13 Mijini .................................................................................................. 112
4.14 Elimu ................................................................................................... 112
Hitimisho .................................................................................................... 117

**SURA YA TANO** ...................................................................................... **118**
Hitimisho .................................................................................................... 118
5.0 Utangulizi ............................................................................................. 118
5.1 Muhtasari ............................................................................................. 118
5.2 Matatizo ............................................................................................... 120
5.3 Matokeo ............................................................................................... 121
5.4 Mapendekezo ....................................................................................... 123

**MAREJELEO** ........................................................................................... **126**
Viambatisho ............................................................................................... 130

## UFAFANUZI WA MSAMIATI

| | | |
|---|---|---|
| Abamuima | - | Jamii iliyoishi Imanga - kitovu cha utawala wa Nabongo baada ya kuhama kutoka Tiriki, Karne ya 16. |
| Muima | - | Kiongozi wa Abamuima |
| Itookho | - | Himaya au Ngome |
| Bukusu | - | Jamii moja wapo ya Waluyia inayoishi katika Bungoma ya sasa, Mkoani Magharibi. |
| Abawanga | - | Jamii moja wapo ya Waluyia iliyokuwa na ushawishi mkubwa wakati wa mkoloni. |
| Nabongo | - | Kiongozi wa Abawanga |
| Musambwa | - | Dini au imani iliyoendelezwa na kiongozi mmojawapo wa Wabukusu, Elijah Masinde wa Nameme. |
| Lukooba (wingi ni Chingooba) | - | Ngome ya Wabukusu |
| Wangisieki | - | Jina la msimbo la kuashiria ujanja au utapeli. |
| Nywele ngumu | - | Watu wagumu kueleweka, watundu, na ambao si rahisi kushawishika |
| Mabalozi | - | Watawala walioteuliwa na Nabongo Mumia ili kutawala maeneo yaliyokuwa nje ya Abawanga. |
| Lukongo | - | Naibu wa chifu |
| Mulango | - | Wasaidizi wa naibu wa chifu |
| Kisoko | - | Watawala wa daraja ya chini<br>Wasaidizi wa Mulango |
| Omutapita | - | Mkalimani |
| Omutopi | - | Dobi |
| Okhwa | - | Mtoto wa .................... |
| Ekutusi, Kichabe na Ekhorere | - | Vifaa muhimu vya utawala miongoni mwa Wabukusu |
| Kananachi na Kikwameti | - | Majina ya rika hasa kwa wale waliopaswa tohara wakati mmoja. |

| | | |
|---|---|---|
| Lukulu lwa Masaaba | - | Mlima Elgon |
| Omurumwa na Nyasaye | - | Mtumwa wa Mungu |
| Wele Khakaba | - | Mungu |
| Bitasia na Chinengo | - | Bidhaa za biashara zilizotolewa na Wandorobo kutoka Mlima Elgon kuwauzia Babukusu. |

## VIFUPISHO

Vifupisho ambavyo vimetumiwa katika matini:

| | | |
|---|---|---|
| Mhj. | - | Mahojiano |
| D.Y.M | - | Dini ya Musambwa |
| K.A.P.E | - | Kenya African Preliminary Examination |
| C.E.E | - | Common Entrance Examination |
| C.S.E | - | Cambridge School Certificate |
| I.B.E.A | - | Imperial British East Africa Company |
| F.A.M | - | Friends African Mission |
| F.C | - | Football Club |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Wataalamu wengi wameshughulikia swala la maenezi ya Kiswahili kutoka Pwani hadi Bara. Mbaabu (1996:42) amenena kuwa shughuli za biashara kutoka pwani zilipanuka sana kuanzia mwaka wa1832 katika himaya ya Sayyid Said. Wafanyi biashara na Wamishenari walichangia pakubwa kukua kwa Kiswahili barani kwa vile waliitumia lugha hii kueneza injili na kuwasiliana. Furaha (1991) akimnukuu Gorman (1974:39) anashadidia kuwa istighala za kibiashara zilichangia maenezi barani kusababisha maingiliano kati ya wakazi wa bara na wakazi wa Pwani. Shihabuddin na Mathias Mnyampala (1977:72) wanasema kuwa misafara ilipenya sehemu mbalimbali za bara kuanzia Mombasa na Malindi hadi kufika Ziwa kuu la Nyanza na mbali zaidi na kuwezesha makundi kama ya Wakamba, Wakikuyu, Wanandi, Wajaluo na Waluhyia kukurubiani na Waswahili. Magharibi mwa Kenya, Mumias ndicho kilichokua kituo cha biashara kilichodhihirisha kwa kiwango kikubwa athari za maingiliano ya biashara kati ya wenyeji wa kituo hiki na Waswahili. Utamaduni wa Kipwani ukapanuka barabara kupitia dini ya Kiislamu iliyoimarishwa na Sudi wa Muslimu na Umari wa Kombo.

Bogonko (1992) anaongezea kuwa kupitia biashara, imani na utamaduni wa Kiislamu na upanuzi wa madrasa barani, Kiswahili kilipata hadhi kuu. Baadhi ya viongozi barani mfano Nabongo Mumia walisilimu na kujenga uhusiano dhabiti kati yao na Waswahili.

Kusimba (1999) anasema kuwa, pwani ya Afrika Mashariki katika kipindi cha majilio ya wageni, ilishuhudia ukuaji wa utamaduni anuwai, ukuaji wa miji kwa sababu ya biashara kutoka pembe tofauti za dunia. Misafara ya biashara ilipenyeza hadi himaya za Karagwe, Bunyoro na Buganda. Anasisitiza kuwa mtandao huu wa kibiashara ulijengwa na Waswahili miaka mianane iliyopita. Ingawa Waswahili waliingiliana na Wareno, Wahindi na Waarabu, utamaduni wao ulijikita katika mizizi ya Kiafrika. Licha ya Pwani ya Afrika Mashariki kutembelewa na wageni na hata kuweka makazi yao, waswahili walitawala eneo hili kitamaduni na kisiasa. Kiswahili kilikuwa lugha yao na basi kuwatambulisha kama jamii mahsusi. Kwa mujibu wa Kusimba (1999), waswahili waliingiliana na wageni kwa kipindi cha Millenia mbili na kufikia karne ya kuma na tisa, jamii ya Waswahili ilikuwa imekita mizizi katika biashara, ukulima, uvuvi na ubaharia.

Kutokana na historia hii fupi ni dhahiri kwamba baadhi ya hali zilizosababisha maenezi ya Kiswahili hazijatafitiwa. Baadhi ya hali hizi ni dhima ya viongozi au watawala waliochangia katika maenezi ya lugha ya Kiswahili. Lugha ni muhimu sana katika maswala ya uongozi, maana hufaulisha sera mbalimbali za utawala. Ushahidi uliotokana na utafiti huu ulidhihirisha nafasi muhimu ya Kiswahili katika asasi anuai. Itakuwa muhimu kuchunguza nafasi ya utawala katika kuendeleza maenezi ya Kiswahili barani. Nabongo Mumia alikuwa kiongozi mtajika Mkoani magharibi na kuchunguza umuhimu wake katika upanuzi wa Kiswahili katika maeneo aliyoyatawala ilichangia katika kuelewa jukumu la viongozi katika kuimarisha uongozi wao kupitia lugha. Jamii husika pia zilikuwa

na umuhimu wake maana mchango wao katika kueneza Kiswahili hauwezi kupuziliwa mbali.

Utafiti huu ulidhamiriwa kuchunguza jinsi utawala na Nabongo Mumia ulivyochangia maenezi ya lugha ya Kiswahili katika eneo linalokaliwa na Babukusu mkoani Magharibi.

## 1.1 Swala la Utafiti

Kufikia Karne ya 19, kati ya miaka ya 1896 hadi 1910,lugha ya Kiswahili ilikuwa inatumiwa katika asasi ya utawala, dini na shughuli za jamii katika eneo la Babukusu.

Huu ulikuwa wakati wa utawala wa Nabongo Shiundu na baadaye Nabongo Mumia ambaye alisilimu na kutawala mnamo mwaka wa 1910 hadi 1949. Eneo la Ubukusuni ni muhimu sana katika historia ya utawala wa Nabongo Mumia. Hili ni eneo kubwa kuliko wilaya zinazounganisha Mkoa wa magharibi. Umuhimu wake kihistoria ulitokana na uhasama baina ya utawala wa Mumia na Mkoloni. Sera za Mkoloni hasa ujenzi wa reli kuelekea Uganda, zilitatizika basi kumfanya Mumia kuungana na Mkoloni katika vita vya Chetambe ambapo Babukusu walishindwa. Katika misingi hii, tumeona bora kuchunguza ni vipi Mumia aliendeleza utawala wake dhidi ya jirani hasimu na hasa kufaulisha sera zake za utawala ikiwemo sera ya lugha ambayo kwetu ni muhimu. Utafiti huu ulilenga, kuainisha, kuieleza na kuichanganua mikakati iliyotumiwa na utawala wa

Nabongo Mumia katika uenezaji wa lugha ya Kiswahili Ubukusuni, Mko wa Magharibi mwa Kenya. Jambo kama hili halijafanyiwa utafiti katika historia ya maenezi ya lugha ya Kiswahili.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

(i) Utafiti huu ulinuia kuainisha mchango wa Nabongo Mumia katika kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika himaya yake.

(ii) Kuchunguza sababu nyinginezo zilizochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika eneo hili.

(iii) Kuchunguza na kubainisha baadhi ya pingamizi zilizokuwepo dhidi ya kuenea kwa Kiswahili na namna zilivyoepukwa ili kufanikisha malengo ya uenezaji

(iv) Kuchunguza ikiwa Babukusu walichangia katika mchakato wa maenezi ya lugha ya Kiswahili.

## 1.3 Sababu za Kuchagua Mada

Mada za utafiti huwa ni za kiakademia. Kwanini wasomi wa lugha ya Kiswahili wajishighulishe na maenezi yake?

- Lugha ya Kiswahili ni muhimu kwani ni lugha rasmi na ya kitaifa katika baadhi ya mataifa barani Afrika
- Utafiti huu ya maenezi yake utachangia katika harakati za sasa za kukiimarisha Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi.

- Mikakati iliyotumiwa na utawala wa Nabongo Mumia inaweza kuazimwa na utawala wa wakati wetu katika kuimarisha sera ya lugha nchini. Ikiwa utawala wa Mumia ulikosea, basi mafunzo fulani yanaweza kuibuka kutokana na utawala huo.
- Lugha ni muhimu sana katika uongozi au utawala wowote.

Mbaabu (1996) anakariri kuwa sera ya lugha katika uongozi wowote ni muhimu sana na hivyo mchango wa uongozi wa Nabongo Mumia katika kuendeleza sera mbalimbali ya mkoloni ulipata ufanisi kutokana na lugha ya Kiswahili, swala ambalo halijafanyiwa utafiti.

## 1.4 Nadharia Tete

Nadharia tete zifuatazo zitaongoza utafiti huu

(i) Utawala wa Nabongo ulichangia pakubwa katika kuenea kwa Kiswahili katika eneo la Babukusu.

(ii) Dini na biashara zilichangia sana katika kuenea kwa Kiswahili.

(iii) Watawaliwa walisaidia sana katika kurahisisha kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

(iv) Tuzo ambazo zilihusishwa na ujuzi wa lugha ya Kiswahili katika utawala wa Nabongo Mumia zilichangia katika kuenea kwa Kiswahili.

### 1.5 Upeo wa Utafiti

Kulingana na mada ya utafiti, utafiti huu utajikita katika:-

(a) Eneo la Mumias na Matungu ambapo utachunguza historia ya ukuaji wa Kiswahili chini ya utawala wa Nabongo Mumia. Hiki ndicho kilikuwa kitovu cha utawala wa Nabongo Mumia.

(b) Eneo la Babukusu, hasa la Kimilili, Bungoma na Malakisi lililotawaliwa kwa kuchunguza namna wakaaji wa eneo hili walivyoingiliana na wageni - watawala na wafanyi biashara. Nabongo Mumia alitawala eneo la Magharibi kati ya miaka ya 1910 na 1949. Kwa hivyo muda huu ni muhimu sana katika utafiti wetu.

### 1.6 Misingi ya Nadharia

Katika utafiti huu tulitumia nadharia ya lugha kama mfanyiko wa kijamii na nadharia ya utegemezi. Utafiti huu ulitumia nadharia hizi mbili ili kukidhi mahitaji ya malengo yote ya utafiti huu.

#### 1.6.1 Nadharia ya Lugha kama Mfanyiko wa Kijamii

Nadharia hii kama ilivyopambanuliwa na La Forge (1983:3) hujikita katika vigezo sita muhimu vilivyoainisha mtazamo wa mifanyiko ya kijamii kuhusu lugha:

- Mfanyiko wa mtu binafsi
- Mfanyiko kati ya watu wawili
- Mfanyiko wa kimawasiliano

- Mfanyiko wa kielimu
- Mfanyiko wa kimaendeleo
- Mfanyiko wa utamaduni

La Forge (1983:9) anasisitiza kuwa lugha ni watu, lugha ni maingiliano ya watu na vilevile lugha ni watu katika majibizano. Tranel (1968) anasema kuwa katika hali kama hii wanaojifunza lugha huhamasishwa kwa kiasi na hivyo kuwa wategemezi. Munby 1978 anasema kuwa wategemezi huwa kundi lisilo nguvu na huhamasishwa na kundi tawala au lenye nguvu kupitia vishawishi kadha wa kadha. Kundi tawaliwa hupitia mabadiliko. Mabadiliko haya ni kutegemea kundi lenye nguvu kupitia asasi ya utawala. Baadaye kundi hili huteta na kukinai, lakini baadaye huvumilia mwishowe baada ya kujifunza lugha hiyo hujitegemea wao wenyewe.

Curran (1972:90) ameongezea kuwa juhudi za kundi moja la kujifunza lugha ni kama kuzaliwa tena kwa kuwa hutazamwa kama tajriba ya binafsi na kijamii ambapo waliojifunza lugha ngeni huwa kama njia kuu za kujieleza na kujitosheleza.

Wardhaugh (1987) anachangia kuwa kigezo muhimu kwa uenezaji wa lugha ni kitovu chake ambako huchipukia ama ienee au itawale lugha nyingine. Kitove hapa ni eneo la utawala ambalo lugha hiyo hutumiwa hasa. Tajriba kutoka kwa lugha nyingine anavyosema Wardhaugh (1987) mfano Kilatini, Kigiriki,

Kiingereza, Kifaransa zaonyesha kuwa maenezi yalitokana na shughuli za watawala na watawaliwa.

Lengo letu la kutumia Nadharia hii ni kutathmini ukweli kuwa lugha ni watu na hivyo ni mfanyiko wa kijamii. Tukizingatia mada ya utafiti, tuliweza kubaini iwapo maingiliano kati ya wageni hasa Waarabu, Waswahili na Wakoloni huko Mumias na kisha upanuzi wa utawala kwa jamii jirani ambazo zilitawaliwa ulichangia matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa makundi haya. Utafiti huu ulinuia kudhihirisha iwapo makundi haya yalitegemea kundi kubwa lililokuwa na ushawishi mkubwa na kwa kufanya hivyo ama walishurutishwa au kumotisishwa kutumia lugha ya kiswahili. Utafiti huu basi ulitathmini iwapo utawala wa Nabongo Mumia ulitumia ushawishi mkubwa ili kuhakikisha kuwa sera ya lugha inafanikishwa kama ambavyo inadhihirika katika vigezo sita muhimu vya nadharia hii. Utafiti huu pia ulichunguza ikiwa maingiliano kati ya makundi aliyoyatawala Nabongo Mumia yalipitia mapito anuwai yanayoainishwa na mifanyiko hii sita, hasa kupitia asasi ya utawala, dini, biashara, ndoa na elimu. Kwa hivyo nadharia hii ilituwekea msingi wa kuelewa mifanyiko ya kijamii ambapo lugha ni kigezo mojawapo.

### 1.6.2 Nadharia ya Utegemezi

Nadharia hii ina misingi katika Umarxi ambao ulizuka kule ulaya. Mitafaruku ya kiuchumi ilizuka kati ya vikundi mbalimbali vya wanajamii vilivyojihusisha katika uzalishaji wa mali. Umarxi mpya ni uhamishaji wa nadharia hii hadi

maeneo mengine ya dunia. Tabaka linalomiliki baraste kuu za uchumi hutegemewa na matabaka ya chini kwa njia zozote zile. Kwa hivyo umarx-mpya ni zao la Umarx mkongwe wa kirasimi. Hali ambapo taifa moja hujikuta katika hali ambayo linazidiwa nguvu ni utegemezi na kama ambavyo Prebisch asema akinukuliwa na Mbaabu (1996) "Matokeo huwa nchi kama hii haiwezi kujiamulia ya kufanya au ya kutofanya".

Shida ya kijami na kimuundo katika mataifa yanayoendelea, hasa Afrika hujikuta katika picha na maandishi ya Wamarekani wa kilatini ambao walichukizwa sana na hali halisi ilivyokuwa katika mataifa yanayoendelea. Waandishi hawa walitiliwa upondo na mwana Umarxi-mpya Paul Baran. Andre Gunder Frank (1969) alitazama uhusiano kati ya marekani ya kaskazini na kusini akitumia lensi za Baran. Mtazamo wake ulianisha hali ya kibepari ambapo dunia imegawika katika matapo mawili.

(i) Kitovu, tapo linalohusisha mataifa yaliyoendelea kiuchumi.

(ii) Pembezoni, tapo la mataifa yanayoendelea hasa marekani kusini na Afrika. Kutokana na dhana hii ndipo mihimili ya nadharia ya utegemezi hujipambanua. Ukuaji wa nadharia hii ulianzishwa na uundaji wa tume ya kiuchumi ya Umoja wa Kitaifa mwaka wa 1948, chini ya Raoul Prebisch ili kutoa misaada ya kiteknolojia kwa mataifa ya Marekani kusini. Utegemezi ni zao la ubepari wa kimataifa ambao uliletwa barani Afrika. Nadharia hii, imetumiwa hapa Afrika na Samir Amin (1974, 1976), Walter Rodney (1972) na Immanuel Wallersterin

(1972). Nchini Kenya, baadhi ya waliotumia nadharia hii ni Leys (1974) na Mbaabu (1996).

Leys, (1974:8) anasisitiza chanzo cha nadharia hii barani Afrika wakati mataifa ya bara hilo yalivyoingizwa katika uchumi wa Ubepari. Nadharia hii hushikilia kuwa utegemezi si hali halisi ya Afrika lakini ni zao la mfanyiko wa historia wa upanuzi wa ubepari ambao ulisababisha ukuaji wa mataifa ya kimagharibi na huku Afrika inanyonywa – Mataifa ya ulaya yalinyonya rasilmali za asili huku Afrika ikibaki wazi. Unyonyaji huu ulianza kabla ya majilio ya ukoloni hasa tukizingatia biashara ya Waarabu na Waswahili katika Afrika Mashariki. Unyonyaji huu basi ulianza wakati huu ambapo shughuli za biashara ziliwanufaisha hawa wageni kuliko Waafrika, basi kuweka misingi ya unyonyaji na utegemezi. Swai (1984:18) anasema kuwa misingi hii ilijidhirihisha wakati wageni hawa nchini Kenya waliungana na watawala wa makabila mbalimbali. Makabila haya yaliwasaidia kuendeleza sera zao huku wakihujumu tawala za Kiafrika na uchumi wao. Watawaliwa waliachwa wategemezi. Kuungana na watawala hawa kulisababisha ukuaji na uendelezaji wa vitovu vya siasa na uchumi mfano utawala wa Nabongo Mumia huko Mumias.

Kwa hivyo, mataifa yanayoendelea hutegemea uuzaji wa raslimali zao kwa mataifa yaliyoendelea ambayo huamua bei na kuyafanya kutoendelea na kuendelea kuyategema kiuchumi, kisiasa, kiuchumi na teknolojia-Mbaabu (1996:2). Mazrui A. (1980) ametofautisha kati ya utegemezi wa kimuundo

(uchumi, siasa) na utegemezi wa kitamaduni ambao huathiri maadili, maarifa na fikira za wanajamii. Utegemezi wa kitamaduni ni muhimu kwa mujibu wa utafiti wetu. Utegemezi huu wa kitamaduni hukuzwa kupitia.

(i) Vyombo vya habari na elimu.

(ii) Lugha za kikoloni zilizorithiwa na mataifa yanayoendelea – Kiingereza, Kihispania, Kifaransa na Kireno.

Mbaabu (1996) anasema kuwa lugha hizi ziliendeleza utegemezi kiisimu, kiutamaduni na kiuchumi. Lugha hizi ziliweka misingi ya kikoloni na kuigawa Afrika katika makundi matatu ya utawala. Makundi haya yalikuwa ya Kireno, Kifaransa na Kiingereza, bila kuzingatia lugha za kienyeji na mipaka yao. Lugha hizi za kikoloni zilitawala lugha za wenyeji na kusababisha ukuaji wazo kimataifa, huku lugha za wenyeji zikikosa nafasi.

Mbaabu (1996:7) anasisitiza kuwa matumizi ya lugha hizi – Kiingereza, Kifaransa, Kireno – ilikuwa njia moja ya:

- Kujipatia kazi nzuri katika utawala wa kikoloni
- Kisomo cha juu
- Mapochopocho yaliyohusiana na utamaduni na anasa za ukoloni mfano:- Kujipatia maadili mapya – mavazi, vyakula, dini, maongezi, kutazama video, filamu na kubadilika kwa majina ya watu binafsi ili kujinasibisha na wakoloni.

Kachru (1986) aangalia lugha za kikoloni kama jazanda, hasa anapozinasibisha na silaha ambapo maswala yahusuyo lugha hizi hasa Kiingereza ni zaidi ya kiisimu kwani hujikita katika historia, jamii, mitazamo ya wanajamii na siasa na uchumi. Nguvu ya lugha ni nguvu ya jamii hiyo mahsusi ambapo hujionyesha kupitia ushawishi, pembelezi na hata kulazimisha jamii husika kwa mujibu wa kukandamiza lugha moja, huku nyingine ikipewa hadhi.

Apendeza nadharia mbili kuhusu lugha ya kiingereza: ukubalifu wa lugha ya kiingereza hutokana na sababu za kiisimu zinazokubaliwa kimataifa na pili lugha hupata nguvu za ushawishi mkubwa kupitia njia kadhaa na basi kupelekea kuielewa. Nguvu hizi ni za unyonyaji na ukoloni.

Hali hii basi yashadidia utafiti wetu maana kama asemavyo Kachru 1986 (128-129) lugha hupata makali kimatumizi katika jamii kwa sababu:

- Hupanua jamii ya wazungumzaji lugha
- Kama chombo cha kustaarabisha jamii zilizo nyuma kimaendeleo
- Huleta fasihi ya kimagharibi
- Huzua manufaa ya kiuchumi
- Husaidia katika kutawala maswala ya elimu
- Huchangia katika ulaghai ili kundi moja liweze kupata linalokusudia.

Vigezo hivi vyote vyachangia wazo la utegemezi na basi utafiti huu ulitathmini ni vipi Kiswahili kama Kiingereza kilikuwa na ushawishi mkubwa sana. Je, mtawala alitumia kila hila kuhakikisha matakwa yake yanatimilika kupitia lugha? Utafiti huu basi katika misingi hii ulitathmini ni vipi lugha ya Kiswahili ilienea kutoka kitovu ambacho kilikuwa Mumias hadi eneo la Babukusu na maeneo mengine Mumia alikotawala. Je, Kiswahili kilichukua hadhi kubwa kuliko Kibukusu ambapo kutumia lugha hii barabara kulihakikisha watumizi, kazi bora, vyakula bora, usilimishwaji na nafasi ya kuoa wanawake warembo kutoka tabaka tawala kama nadharia hii inavyodai? Tulichunguza hali hii ya utegemezi ambapo lugha inayotawala huwa kama nyenzo muhimu ya uzalishaji wa mali na uchumi na basi kutegemea watumizi wake. Utafiti huu basi ulichunguza ikiwa huo ndio mkondo uliochukuliwa katika eneo la Babukusu na basi kupelekea uenezaji wa lugha ya Kiswahili wakati wa utawala wa Nabongo Mumia.

Kwa hivyo, nadharia hii ilisaidia utafiti huu kuchunguza kuwa kuenea kwa Kiswahili kutoka kitovu cha utawala wa Mumia hadi Ubukusuni kulijikita katika dhana ya utegemezi. Nadharia hii basi ilituwekea msingi bora katika utafiti wa mada hii.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Utafiti kuhusu kuenea kwa Kiswahili hasa katika eneo la Babukusu haujafanywa, hasa katika misingi ya asasi kama ya utawala na dini. Hata hivyo watalamu wengi wamefanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Massamba

(1987, 1992) anasema kuwa suala la siasa kati ya watawala na watawaliwa lilisaidia sana katika maenezi ya Kiswahili. Furaha (1991), anamnukuu Duran (1975) aliyefanya utafiti katika jamii yenye lugha nyingi huko Lumbwa. Utafiti huu unatofautiana na wetu ambapo aliangalia nafasi ya Kiswahili miongoni mwa lugha za kiasili kama Kijaluo, Luhya, Kikuyu, Kalenjin katika sehemu ya mashambani katika bara ya Kenya. Ulijikita katika mahusiano ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika za bara ya Kenya.

Uchunguzi mwingine wa matumizi ya Kiswahili nchini Kenya ulifanywa na Parkin (1974) Bujra (1974) na Nearle (1974) ambapo maelezo yao yalichapishwa na kuhaririwa na Whiteley (1974). Uchunguzi huu ulihusisha matumizi ya lugha katika mitaa michache ya jiji la Nairobi. Furaha (1991) naye alichunguza matumizi ya Kiswahili mjini Malindi, sehemu iliyo na watu wa asili mbalimbali kwa hivyo jumuiya ya kugha nyingi. Utafiti wetu una mchomo wa kutaka kuelewa maenezi ya Kiswahili katika sehemu za bara hasa katika kipindi cha utawala wa ukoloni.

Abdulaziz (1982) ameelezea matumizi ya lugha mbalimbali nchini Kenya ambapo wamisheni walijigawa katika makundi mawili, kundi la kutumia lugha za kikabila katika mahubiri na la pili lililotumia Kiswahili maana kilikuwa kimetangaa sana. Whiteley (1974) alieleza jinsi jamii mbalimbali zilivyotumia Kiswahili nchini Kenya. Alifikia uamuzi kuwa kilitumika sana kuliko za kiasili kwa mawasiliano.

Aliota mfano wa uwanja wa biashara kati ya makundi mbalimbali kama chombo kilichosaidia sana katika maenezi.

Mbaabu (1996) anaangazia ukuaji wa makazi ya waarabu katika pwani ya Afrika mashariki na baadaye kuingiliana na wenyeji wa pwani na wa kazi wa bara kibiashara na kidini. Maingiliano haya kibiashara, dini na hata ndoa yalichangia sana maenezi ya Kiswahili katika bara ya Kenya. Utafiti huu ni muhimu sana kwa utafiti wetu maana kazi zao zote zina umuhimu wa kuiwekea mada yetu msingi thabiti.

Suala la utawala wa Nabongo Mumia limetafitiwa sana na wanahistoria. Murunga (1998) anawanukuu Obudho na Waller (1976) ambao walishughulikia ukuaji wa miji katika eneo la magharibi mwa Kenya kama vile Kisumu na Mumias, lakini hawajashughulikia swala la lugha.

Aseka (1989), Ogutu (1979) na Memon (1976) wanaangalia kwa jumla historia ya ukuaji wa Mumias kabla na wakati wa mkoloni. Aseka (1989) anaonyesha umuhimu wa Mumias kama kitovu cha kibiashara kabla na wakati wa ukoloni. Naye Ogutu aonyesha hadhi ya Nabongo katika ukuaji wa kitovu hiki. Memon (1976) anaeleza Mumias kama kitovu kikuu cha utawala katika eneo hili la Magharibi mwa Kenya.

Osogo (1966) na Were (1967), wanaainisha historia ya Waluyia kwa jumla, ambapo Sakwa M'sake (1971) na Dealing (1974) wanaonyesha historia ya jamii ya Abawanga namna walivyounganika chini ya Nabongo. Dealing (1974) anaongezea kuwa ushirika wa Abawanga na wakoloni ulikuwa na nia ya kunyamazisha jamii hasimu kama Babukusu na Wajaluo ili mkoloni atimize matakwa yake, huku himaya ya Abawanga ikiwa chini ya ulinzi wa wakoloni. Utafiti huu ni muhimu sana kwa mada yetu maana hutuangazia hali ilivyokuwa katika himaya hii na sababu za ushirika wa Nabongo na mkoloni na basi kurutibisha utafiti wetu. Osogo (1967) na Kenyanchui (1992) pia wanachangia utafiti huu maana wanatoa historia ya maisha ya Nabongo Mumia (1910-1949). Maisha ya Nabongo Mumia na mustakabala wa eneo la Magharibi mwa Kenya ni muhimu sana katika utafiti wetu.

Abdalla (1971) anaonyesha maingiliano ya Waarabu na Waswahili katika himaya hii na basi ukuaji wa utamaduni wa Waswahili, Mumias. Aseka (1989) pia anashughulikia swala la Waarabu na Waswahili na baadaye wakoloni na kutoa athari za uhusiano wa wageni hawa kwa wenyeji na jamii zilizozunguka Abawanga. Huu basi utatusaidia katika kuwekea msingi utafiti wetu.

Wagner (1949) aliangalia miundo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ya Babukusu kabla na wakati wa mkoloni. Were (1966 & 1972), Wipper (1971 & 1977) na Shimanyula (1978) walitazama uibuzi wa Dini ya Msambwa miongoni mwa Babukusu ambapo wote walishughulikia mwanzilishi wa dini hiyo Elijah Masinde

na kumchora kama mtetezi na aliyepinga dhuluma za mkoloni. De wolf (1971) alishughulikia mabadiliko katika dini na jamii miongoni mwa Babukusu hasa wakati wa ukoloni. Tafiti hizi za sally (1972), Makila (1982), Nangulu (1989) zimeonyesha jinsi jamii ya Babukusu ilivyopigana na mkoloni mwaka wa 1895 katika vita yva Lumboka na Chetambe. Utafiti huu ni muhimu kwani ni baada ya vita hivi ndipo Babukusu walitawaliwa chini ya Nabongo na mkoloni ambapo *'Chingoopa'* zilibomolewa. Wandibba (1972) anashadidia umuhimu wa *Chingoopa* kwa jamii hii ya Babukusu. Wesonga (1985) naye anaonyesha miundo ya kijeshi na kisiasa ya Babukusu nao Sakwa M'sake (1971), Dealing (1974), licha ya kuandika historia ya Abawanga, wametoa athari za dini na elimu ya kikoloni, hasa katika wakati wa ukoloni kwa jamii zote za Abaluyia kiuchumi na kijamii lakini hasa wakirejelea Babukusu. Utafiti huu unadhamiria kuangalia swala la kijamii ambalo ni lugha, hasa jinsi ambavyo walihusiana na majirani hasimu.

Utafiti wa hivi karibuni ambao unashadidia mada yetu ni wa Murunga (1998) na Wafula (2000). Murunga (1998) anaelezea athari ya Waarabu na Waswahili katika 'itookho' ya Abawanga na uwezo wao katika kushinikiza ukuaji wa himaya ya Nabongo Mumia kisiasa, kibiashara, kiuchumi na kidini. Anaelezea kuingia kwao katika eneo hilo tangu utawala wa Nabongo Shiundu ambapo 'itookho' hii ilipewa jina 'Kwa – Shiundu' na baadaye upanuzi wake ukiathiri jamii zilizoizunguka moja kwa moja. Wafula (2000) alizingatia siasa na uzalendo wa Babukusu baina ya miaka ya 1894 – 1963 dhidi ya dhuluma ya wageni, hasa

wakoloni. Kazi yake inaangazia chimbuko na makazi ya jamii hii katika kipindi hiki, uhusiano na Abawanga, Waarabu na Waswahili, Wakoloni na jamii jirani kwa jumla. Utafiti wa Wafula (2000) na Murunga (1998) una mchango mkubwa sana kwa mada yetu kwa kuwa ulitupa mwangaza kijumla kuhusu jamii hizi mbili, mahusiano yao na kutuwezesha kuzungumzia pengo kuhusu uenezaji wa lugha ya Kiswahili katika misingi hii ya maingiliano. Licha ya tafiti hizi, ni dhahiri kuwa utafiti kuhusu swala la maenezi ya lugha ya Kiswahili katika misingi ya utawala wa Nabongo Mumia katika jamii ya Babukusu haujafanywa. Utafiti huu ulidhamiria kufidia pengo hili. Utafiti kuhusu jamii za Babukusu na Abawanga umekuwa tu katika misingi ya kihistoria.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

### 1.8.1 Utafiti Maktabani

Utafiti huu uliegemea katika usomi maktabani. Utafiti huu ulizingatia historia ya jamii hizi mbili – Abawanga na Babukusu –ambapo tulizingatia waandishi mbalimbali walioandika kazi zao kuhusu jamii hizi. Utafiti huu ulizingatia waandishi wa historia ya jamii hizi, waandishi kuhusu historia ya Kiswahili, majarida, magazeti na mtandao na pia uandishi kuhusu nadharia za utafiti ili kuziimarisha kwa mujibu wa vipengele muhimu vinavyochangia mada yetu ya utafiti hasa utawala, dini, biashara miongoni mwa vingine.

### 1.8.2 Utafiti wa Nyanjani

Utafiti huu ulitumia vifaa vifuatavyo ili kukusanya data kamili:-

(i) **Hojaji**-Hojaji mbili ziliandaliwa, hasa zikilenga jamii hizi mbili- Abawanga na Babukusu. Kila jamii ilikuwa na hojaji mahsusi. Lengo la hojaji hizi ni kukusanya data inayoafiki matakwa ya mada hii. Wajibu kutoka jamii hizi mbili walihojiwa kwa mujibu wa swala la utafiti.

(ii) **Mahojiano** – Tulihoji wazee wenye tajriba kutoka jamii hizi mbili na pia watawala waliostaafu kutoka jamii hizi. Viongozi wa kidini walioishi kipindi hicho walihojiwa.

(iii) **Sampuli** - Tulizingatia sampuli maksudi hasa maeneo mahsusi katika jamii hizi mbili tukizingatia kundi la wazee wenye tajriba katika jamii hizi. Sampuli ya wahojiwa ilihusisha wazee kutoka sehemu nne mahsusi – Mumias, Bungoma, Kimilili na Malakisi. Takribani wazee kumi tano watahojiwa. Wazee hawa walikuwa na tajriba katika maswala ya dini, biashara na utawala.

(iv) Baadhi ya vifaa tulivyotumia ni Kamera, hojaji, vinasa sauti, kalamu na daftari za kutosha.

(v) Njia ya utafiti ulihusu mahojiano hasa kwa wale wazee wasioweza kusoma na kuandika. Hojaji iliwafaa wazee waliokuwa na uwezo wa kusoma na kuandika.

### 1.8.3 Kuchanganua Data

- Kusoma kazi za waandishi maktabani kuhusu jamii hizi mbili ili kupata mwanga ufaao kwa utafiti.
- Data ya pili changishi iliyokusanywa kutokana na mahojiano, hojaji, tasnifu na mtandao itachanganuliwa kwa kuchunguza vigezo vya utawala, ndoa, mahakama, biashara, elimu na asasi nyinginezo ili kuyaweka katika maandishi.
- Mada ilichanganuliwa kwa kuzingatia misingi ya nadharia za utegemezi na lugha kama mfanyiko wa jamii. Lugha hutagusanisha watu wa jamii tofauti.
- Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kupitia maandishi ya nathari, maelezo, picha na ramani. Maelezo yametumiwa kwa kutanguliza na kutamatisha kila sura. Ramani zimeainisha maeneo mahsusi yaliyozingatiwa kwa utafiti huu. Picha zinaonyesha baadhi ya wale waliohojiwa na wale ambao licha ya wao kufa, lakini mchango wao maishani, ulishadidia utafiti huu.

**Kiishilio**

Sura hii ikiwa tangulizi, imetoa maelezo ya kimsingi kuhusu mada ya utafiti kwa ujumla. Imeangazia na kupambanua dhamira na swala la utafiti, nadharia tete pamoja na mbinu za utafiti. Ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data umeelezwa. Nadharia za utegemezi na lugha kama mfanyiko wa jamii ndizo

zilizoongoza shughuli za utafiti ili kubainisha nafasi ya utawala miongoni mwa asasi nyingine katika kueneza lugha ya Kiswahili Ubukusuni.

# SURA YA PILI

## 2.0 HISTORIA YA BABUKUSU NA ABAWANGA

Sura hii itashughulikia historia ya jamii hizi mbili, Babukusu na Abawanga. Historia ya Babukusu ni muhimu kwa sababu ni kundi mojawapo lililotawaliwa katika himaya ya Nabongo Mumia. Uelewa na ukuaji wa jamii ya Abawanga pia ni muhimu kwa sababu jamii hii ndiyo ilikuwa kitovu cha utawala katika enzi ya ukoloni katika eneo la Kavirondo ya Kaskazini.

### 2.1 Jamii ya Babukusu

Babukusu ni jamii mojawapo ya Abaluyia iliyo na makazi yake katika wilaya ya Bungoma, mkoani Magharibi. Baadhi ya Babukusu wamejenga makao yao katika wilaya jirani za Trans – Nzoia, Kakamega, Busia, Teso, Mt. Elgon, Malava na Lugari. Wilaya ya Bungoma hupatikana kusini mwa Mlima Elgon, hupakana kaskazini magharibi na taifa la Uganda na kaskazini mashariki na wilaya ya Trans-Nzoia. Ramani ya Kenya hapo chini inaonyesha nafasi ya wilaya ya Bungoma nchini.


Abaluhya hujumuisha makundi mbalimbali ambayo hutambulika kwa kuchunguza lahaja zao. Mchoro ufuatao unaainisha baadhi ya makundi haya ya Abaluhya wa eneo la magharibi mwa Kenya.

## LOCATION OF BUNGOMA IN KENYA




Prepared by CBS,1999 Pop.Census

This map is not an authority over administrative boundaries





Aseka (1989:77) anaongezea kuwa Abaluyia ni watu wa 'moto mmoja'. Tafsiri yake ni kuwa walikuwa watu walioshiriki, kufaidi, na kutumia boma moja, kwani kila jioni waliota moto pamoja. Dhana hii iliwaunganisha pamoja. Utawala wa mkoloni uliwaweka katika eneo la Kavirondo lililohusisha Abaluyia, Wajaluo, Abagusii, Abakuria, Wakalenjin na Ilchemus.

Bungoma ina tarafa saba – Kanduyi, Webuye, Sirisia, Kimilili, Tongareni na Bumula-na mitaa thelathini na tisa na vijiji tisini na tatu (Devt. Plan, 1997:5). Bungoma ya sasa imegawanywa katika maeneo manne mapya ya utawala. Bungoma Kaskazini, Bungoma Kusini, Bungoma Mashariki na Bungoma Magharibi. Ni asilimia ishirini na tano ya Mkoa Magharibi ikiwa na ardhi ya takribani 2063 kilomita mraba na idadi ya watu kulingana na takwimu ya 2001 ifikayo 763, 689. (Devt. Plan, 1997:9).

Kabla ya mwaka wa 1963, Mikoa ya Nyanza na Magharibi ilikuwa Mkoa mmoja kwa jina la Kavirondo ya kaskazini (North Kavirondo) na makao makuu yalikuwa Kakamega. Kati ya miaka ya 1956 - 63, wilaya mpya ilianzishwa - Elgon Nyanza – ikijumuisha Bungoma na Busia huku mji wa Bungoma ukiwa ndiyo makao makuu (De wolf: 1971). Bungoma kabla ya 1959, ilihusisha lokesheni nne – Malakisi, Kimilili, Elgon na South Bukusu (Nabutola, J. M 2008). Awali kabla ya 1927, South Bukusu ilijulikana kama South Kitosh, nayo North Kitosh ilijumlisha Malakisi, Kimilili na Elgon chini ya himaya ya Chifu mmoja, (De Wolf: 1971). Ramani ifuatayo inaonyesha maeneo mahsusi ya utawala wilayani Bungoma. Mipaka ya utawala ilichorwa wakati wa kipindi cha utawala wa mkoloni akiwa na mshirika wake Nabongo Mumia.

BUNGOMA DISTRICT (Administrative Boundaries)




Prepared by Central Bureau of Bureau of Statistics


Historia ya awali ya Babukusu imezua mjadala mkubwa, hasa kuhusu chimbuko lao, uhamaji na baadaye kujenga makazi katika wilaya ya Bungoma. Utafiti uliofanywa umeegemea sana katika ngano ambazo huelezea chimbuko la jamii hii kutoka maeneo ya ajabuajabu ambapo jamii hii ilionekana kuwa safarini kila mara. Maswali tunayojiuliza ni kwa nini? Je, hizo safari ndefu ndefu zilitukia kweli? Je, kuna ushahidi wowote wa kihistoria wa kiakiolojia na ya kiisimu kuhusu madai haya ya kuhamahama hadi kufika maeneo ya sasa?

Ushahidi simulizi unaonyesha kuwa jamii hii ilitoka katika sehemu iliyoitwa Esibakala, Msiri kama chimbuko lao.[1] Kabla ya kuingia kwenye eneo hili, jamii hii ilitoka Esiumbwa Ebung'ole (eneo linaloaminiwa ndilo chanzo cha uumbaji wa binadamu), kisha wakahamia Esituluku kwa kipindi kifupi ndipo baadaye wakajenga makao ya Esibakala kwa miaka mingi sana. Esibakala au Misiri huzua maswala makubwa ya kihistoria maana jamii nyingi za Kenya hueneza madai kuwa zilitoka huko (Were 1967). Mifano ya hizi ni jamii ya Kikalenjin (Kipkorir, 1970: 10-11), na Abagusii (Ochieng 1974:11) miongoni mwa jamii nyingi.

F. E. Makila (1982:28) anaainisha ramani ya nchi walizopitia Babukusu hadi kufika nchini Kenya kutoka makao yao ya asili ya Esibakala. Mundu alikuwa kiongozi akiongoza kundi mojawapo liloitwa Babayi (wafugaji). Katika ujirani wa Mundu, kulikuwa na jamii ya Barwa (Wakalenjin), Bamia (Wateso), Banyifwa (Wajaluo) na Nabibia (Wahabeshi). Watoto wa Mundu walipaita

[1] Mahojiano na Manguliechi tarehe 2.4.2008

mahali walipofugia mifugo wengi Embayi na wao wenyewe wakijiita Babayi. Masaaba, mtoto wa Mundu alizaa Mukisu na Mubukusu.




F. E. Makila (1982:132) anaonyesha maeneo mahsusi waliyopitia na kujenga makao yao ya muda hadi kuingia nchini Kenya. Maeneo haya ni muhimu kwa sababu Babukusu walijigawa katika makundi mahsusi chini ya kiongozi mmoja. Mfano Mubukusu na Mukisu walihamia Sengeli kutoka Embayi na kujiita Babayi Basengeli. Baadaye, walijigawa katika makundi mawili Bamasaba na Babukusu.

Kutoka Sengeli, hadi kufika makazi yao ya leo, Babukusu walijigawa katika koo mbalimbali chini ya viongozi wao. Koo sita kubwa zilijitokeza zikihusisha koo zingine ndogo ndogo. Koo hizi ni Basilikwa, Bamwalie, Bamalaba, Baneala, Banabayi na Bakikayi. Inakisiwa kuwa jamii ya Babukusu ina zaidi ya koo mia moja ambazo ndizo viambajengo vya koo hizi kubwa sita.




*Mapito ya Babukusu kutoka Esibakala*

Ushahidi simulizi na maelezo ya Makila (1982) humeonyesha ukuruba fulani licha ya tofauti ya majina ya makazi ya Babukusu tangu watoke Esibakala hadi kufika Kenya ya kisasa. Kufanana kwa maelezo haya licha ya tofauti ni ishara kuwa jamii hii ilitoka mahali pamoja hadi kufikia makazi yao ya sasa.

Umuhimu wa Msiri kihistoria unatokana na dhana kuwa kabla ya uvamizi wa Waarabu, wakazi wa Misiri walikuwa weusi na hadi sasa kusini mwa Misiri kunakaliwa na watu weusi hadi kaskazini mashariki na kaskazini magharibi mwa Sudan.

Kipindi kirefu cha ukame na njaa kilichangia Babukusu kuhama kutoka kwenye sehemu hii wakiandamana na Bamasaba na Bagisu hadi Embayi na baadaye Silikwa (Manguliechi, W. 2.4. 2008, Makila 1978) ambapo waliingiliana na baadhi ya jamii ya Kikalenjin ambayo ni Tugen, Keiyo na Marakwet (Wandibba S. 1985: 20). Vita baina ya Babukusu na Wakalenjin iliwalazimu kuhamia Lokitang kwenye mpaka wa Turkana na Karamojong. Baadaye walihamia Musengeli na kisha kuingia Kukumai nchini Uganda kati ya karne ya kumi na sita na kumi na saba. Kutoka Kukumai, walihamia Yembe kisha Musolokho hadi kufika Namarare kupitia Mafutu (Sabuni W. D. 2008). Waandishi wengi wa kihistoria wanashadidia kuwa jamii nyingi za Abaluyia, wakiwemo Babukusu ziliishi mashariki mwa Uganda kwa kipindi kirefu kabla ya kuvuka kingo za ziwa Viktoria kuelekea makazi yao ya sasa (Were 1967: 59).

Kulingana na W. Manguliechi (2008), Babukusu walivuka hadi Namatotoa kupitia Nabumali, Mubukusu na Mubwayi (Amukura). Kwa sababu ya vita kati yao na Wateso pale Masielo na Kimaeti, Nabii wa Babukusu Namabii, aliwashauri Babukusu kuhamia makazi wanayokalia hadi leo.

Babukusu wana takribani koo mia mbili ambazo kando na makazi yako ya Bungoma, hupatikana pia Uganda katika wilaya za Bugisu, Sebei na Mbale (katika eneo la Yembe na Cheptui). Jamii hii iliamini katika muumba mmoja-Wele Khakaba (Mungu mpaji) ambaye alisababisha mbingu (*likulu*) na ardhi (*Waneloba*) kuungana na basi kusababisha kuzaliwa kwa *Mundu.* Mundu alizaa *Mwambu* na *Sela* ambapo hawa wawili walimzaa Masaaba, babake Mubukusu-aliyeaminika kuwa ndiye alizaa Babukusu wote (Manguliechi N. 2008). Wele Khakaba alisaidiwa na Wele Murumwa (Mtumwa) na Wele Mukhobe (Msemaji alitwikwa majukumu ya vita na amani).

Kulingana na Wafula (2000), Babukusu walijulikana kama Babambayi ambao wakiwa bado Uganda walisafiri hadi kingo ya ziwa Victoria (Enyanja ya Walule) kutoka milima ya Bukusu kwa ajili ya biashara. Wenyeji wa maeneo hayo waliwapa jina "babandu be bukusi" (watu wa bei) na hadi leo jina hilo likapata mashiko. Ni jamii iliyoishi pamoja, ardhi ilikuwa ya jamii wakiongozwa na wakuu wa koo mbalimbali katika ngome za jamii hii. Babukusu waliishi katika nchi ya rotuba wakikuza mimea na mifugo licha ya ukulima wa mtama (*Kamaemba*), wimbi *(Bulo),* mihogo (*Kimioko*), viazi tamu (*Kamapwondi*) na

baadaye mahindi (1920) na kahawa huenda ndiyo sababu iliyopelekea wakoloni kuwadhulumu Babukusu hasa katika vita vya Lumboka na Chetambe (1894- 5) na kisha baadaye kunyang'anya ardhi yao na kuwatia chini ya himaya ya utawala wao, (KNA, DC/NN/10/1, 1940).

### 2.1.1 Uhusiano na Waarabu na Waswahili

Kumbukumbu za historia zinaonyesha kuwa Waarabu walikuwa wageni muhimu sana katika Pwani ya Afrika Mashariki. Kufikia karne ya tisa (1000 A.D BM/BK), dini ya Kiislimu na biashara vilikuwa vimekita mizizi katika Pwani ya Afrika Mashariki. Vituo muhimu vilikuwa Kilwa, Zanzibari, Mombasa, Malindi na Lamu. Biashara za watumwa na pembe za ndovu zilipelekea wao kuoana na Wabantu na hivyo kujenga jamii ya Waswahili. Wakati Wareno walipofika, karne ya 15, Waarabu walikuwa wamepanua biashara hadi barani kwa kufungua barabara tatu kuu:

- Barabara iliyoelekea Ukambani hadi Mlima Kenya
- Barabara ya katikati iliyopitia Mumias hadi Ziwa kuu la Nyasa.
- Barabara ya Kusini iliyoelekea Tabora – Ujiji.

Jamii ya Babukusu haikuwa na uhusiano mzuri na utawala wa Nabongo Mumia. Kuingia kwa Waarabu na Waswahili kulihakikishia Mumia usalama dhidi ya mahasimu wake Babukusu, wakiwemo Wajaluo wa Ugenya. Uhasama huu ulichangia kuigawa jamii ya Babukusu. Urafiki wake na ukoo wa Bakhoone ulichangia kuteuliwa kwa viongozi wa utawala. Namachanja wa Khisa

aliyetueliwa akawa kiongozi wa hata koo zingine na basi kufungua barabara ya Waarabu na Waswahili kuingia Ubukusuni kwa mujibu wa biashara. Walitafuta watumwa, pembe za ndovu miongoni mwa bidhaa mbalimbali. Kwa sababu ukoo wa Bakhoone ulihakikishia misafara hii usalama, walifaidi kwa kupewa zawadi na kunusurika kuchukuliwa baadhi yao kama watumwa.

Wafanyibiashara haswa Waarabu na Waswahili kupitia himaya ya Abawanga waliwasaka watumwa kutoka kwa Babukusu na kujenga uhasama kati ya Ababukusu na Abawanga (Were 1967: 144). Sudi wa Pangani na Abdulla bin Hamid wa Mombasa waliongoza misafara ya kuwasaka watumwa kwa nguvu. Babukusu walijenga 'chingoopa' (ngome) na kununua bunduki ili kujihami kutokana na mahasimu hawa.

### 2.1.2 Uhusiano na Wazungu

Baada ya safari ya wageni wa kwanza (Waarabu) na Wazungu, hasa wafanyibiashara, wasafiri na wamishenari kama vile Joseph Thompson na J. Martin (1883), waliingia Mumias na baadaye kuingia nchi ya Babukusu wakiandamana na Waarabu na Waswahili. Babukusu walishuku kuingia kwao, hasa ikikumbukwa kuwa walitokea Mumias (Mutoro 1976:7). Abawanga na Waarabu waliwashawishi Wazungu kuwa lazima jamii ya Babukusu inyamazishwe kwa vile walifikiriwa kuwa wabaya, watukutu, na mahasimu (Dealing, 1974:30). Abawanga walichukuliwa kama jamii yenye ushawishi na iliyostaarabika katika eneo la Kavirondo (KNA DC/EN/3/11/7- 1930). Mapatano

kati ya F. Jackson na Mumia kulingana na Were (1967: 157) yalifanya eneo la magharibi mwa Kenya kuwa chini ya himaya ya Kikoloni. Kutokana na Mkataba wa Heligoland (1890), jamii ya Babukusu iliwekwa chini ya himaya ya Uingereza.

Friedrick J. Jackson, akiandamana na Gedge, wote wafanyakazi wa kampuni ya IBEA, walikuwa na amri ya kunyamazisha viongozi wa makabila ambayo yangepinga utawala wao. Machifu kama hawa walishikwa, kufungwa ama kuuawa. Mifano mizuri ni ya Chifu Waiyaki wa Hinga (Kikuyu Kusini) na Orkoiyoit, Koitalel arap Samoei (Nandi). Jackson ni muhimu hapa kwa kuwa ndiye aliyeshughulikia kutia sahihi ya mapatano kwa niaba ya kampuni ya IBEA huko Mombasa, Mumias hadi Mengo katika himaya ya Kabaka (Uganda). Malengo ya kampuni hii yalikuwa:

- Kuwa na uhuru wa kufanya biashara
- Kuendeleza utawala mwema kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya Waafrika, kustawisha ustaraabu, kusimamisha biashara ya utumwa na kufungua maeneo ya bara kwa makundi halali ya biashara.

Ni muhimu kutaja kuwa, eneo la Kavirondo lilipata jina hili kutokana na jamii ya Waluhyia. Neno 'Murundu' ni bunduki. Neno Kavirondo ni istilahi iliyoundwa kutokana na vifo vingi vya jamii ya Wajaluo kutokana na kuuawa na Wazungu wakitumia bunduki. Wajaluo walipinga utawala wa mkoloni na hivyo

kulazimishwa kunyamaza kupitia 'Murundu' au bunduki na ndio basi kustawisha istilahi ya Kavirondo kama eneo la utawala.

Vita vya Chetambe (1895) viliwalazimu Babukusu kurudisha silaha zote, kukubali utawala wa chifu wa kikoloni, kuvunjilia mbali ngome zao, kuhakikisha kuwa wanafanya kazi zote za umma hasa za kujenga barabara na daraja miongoni mwa shughuli nyingine (Nangulu, 1986: 62-63). Namachanja, mkuu wa ukoo wa Bakhoone alichaguliwa kuwa mkuu wa koo zote za Babukusu na kuamuriwa kuhakikisha utiifu wa Babukusu na kuendeleza sera za kikoloni (Makila 1978). Nabongo Mumia naye aliteuliwa kuwa Chifu Mkuu ili kutawala jamii zote za Abaluyia. Ushawishi wake ulikuwa sawa na Kabaka wa Buganda (Osogo, 1975). Utawala wa Nabongo Mumia ulileta jamii zote za Abaluhya chini ya utawala wake. Aliweka mikakati mahsusi ya utawala hadi mashinani. Alikusanya kodi, kuajiri waliofanya kazi za lazima, na kuhakikisha amani na sheria inadumishwa. Nabongo Mumia aliteua jamii na marafiki zake kuwa machifu wa maeneo yasiyo ya Abawanga (Ogot, 1963, Osogo, 1966). Baadhi ya maeneo haya yalikuwa ya Babukusu, Bakhayo, Luo, Kabras, Marama, Samia, Abanyala na Batsotso. Eneo la Maragoli halikutawaliwa kwa njia hii, labda kwa sababu za kisiasa. Kati ya jamii hizi Ababukusu na Ateso, Abanyala na Luo wa Jo- Ugenya na Jo- Gem ndio walikuwa mahasimu wakuu ambao walihatarisha usalama wa himaya ya Nabongo Mumia.

Mumia alifaulu hasa kwa kutumia Jeshi la Mumia lililohusisha Wasomali na Wanubi waliokuja na Wazungu. Alipotawazwa kuwa Chifu Mkuu, Nabongo Mumia alichora mipaka yote ya utawala wake na kuhakikisha kuwa sera na mapendekezo yote ya kikoloni yanatekelezwa isipokuwa mikakati yote ya kikatiba iliyokuwa chini ya uongozi wa kikoloni (Mamdan 1996: 9). Kufikia mwaka wa 1910, mji wa Mumias ulikuwa umekuwa kitovu cha biashara, dini ya Uislamu na utawala ambapo mkoloni alitumia kitovu hiki ili kuendeleza sera zake.

Kutokana na historia hii, daraja la maingiliano lilijengeka katika misingi ya biashara na utawala. Mtagusano wa makundi ya Waarabu, Abawanga, Wazungu na jamii ya Babukusu ulitoa nafasi ya kuwasiliana kwa kutumia lugha ya biashara na utawala. Kwa hivyo, sera za utawala wa biashara zilikiwekea Kiswahili msingi wa kukua.

## 2.2 Jamii ya Abawanga

Abawanga ni jamii mojawapo ya Abaluyia katika eneo la Magharibi mwa Kenya. Jamii ya Abawanga iliingia Kenya kutoka Uganda na kuweka makazi yao ya muda huko Tiriki. Jina Wanga linatokana na mwanzilishi wa jamii ya Abawanga aliyeitwa WANGA. Ugomvi kati ya ndugu yake juu ya utawala ulisababisha kuhama kwake kutoka Tiriki hadi Imanga kupitia Eshibaka karibu na Bukura (Wamukoya A. 2008). Muima, mfalme wa Abamuima alimwajiri Wanga kama mchunga mifugo, lakini baadaye akagundua kuwa Wanga alikuwa mfalme kupitia

kwenye ishara ya bangili ya kifame aliyokuwa nayo na kupanga njama ya kumuua. Hata hivyo, kuwasili kwa wafuasi wa Wanga wa ukoo wa Abashitsetse ulimwezesha kunusurika. Muima alimwambia Wanga ahamie Mushikulu. Hapo ndipo alipojenga makao yake (Wamukoya 2008). Wanga alikuwa Nabongo wa kwanza baada ya Abashitsetse kuchukua hatamu ya uongozi kutoka kwa Abamuima. Muima alikuwa na makao yake Imanga. Nabongo Wanga aliunganisha koo zingine- Abakolwe, Ababuka, Abarunga, Abatsoke, Abang'ale, Abashike na Abashikawa chini ya Abashitsetse na hivyo kuunda himaya tajika chini ya uongozi wake.

Kuongezeka kwa idadi ya watu kulileta shida baina ya Muima na Wanga. Vita vya maneno na uhasama ukazuka kwa sababu ya kung'ang'ania ardhi na malisho. Kwa sababu Wanga alikuwa ameendelea kivita katika makao yake, Eshikulu, aliweza kumshinda Muima huko Imanga na kuishirikisha himaya yake chini ya uongozi wake. Kwa kufanya hivyo, alipanua eneo la utawala wake. Ushawishi mpya aliopata Wanga ulimpa uwezo wa kuwashinda majirani na mahasimu wake. Ndipo jina Nabongo likachukua hadhi kuu kama kiongozi wa utawala, kidini na utamaduni wa jamii ya Abawanga (Dealing 1974:82).

Kabla ya kifo cha Wanga, alifungua stesheni mpya ya 'Elureko' iliyokuwa karibu na Mumias ya sasa. Kwa mujibu wa Murunga (1998), Elureko (kuteka) ilikuwa stesheni ya kuwateka watumwa, hasa kutoka Ubukusuni katika kipindi cha biashara ya Waarabu na Waswahili. Kwa mujibu wa Were (1967), mahasimu wa


Abawanga wakati huo walikuwa Wateso, Babukusu na Wajaluo. Nabongo Netya aliungana na Wakwavi (Maasai) kwa sababu ya uwezo wa Wakwavi kivita ili kuwapiga maadui wa Abawanga. Naye Osundwa aliwatumia Wamaasai kunyang'anya mali ya maadui. Osundwa alihodhi mali iliyonyang'anywa kutoka kwa maadui wao na pia kuanzisha sera ya biashara na Basamia na Basoga kutoka Uganda (Manya, R. 16.4. 2008). Stesheni ya Elureko ilipata umaarufu wakati wa Nabongo Shiundu (1841), hasa kipindi cha kuingia kwa Waaarabu na Waswahili. Wageni hawa walitoa jina jipya la Kwa-Shiundu (Aseka, 1990). Kufikia mwaka wa 1866, Shiundu alikuwa amejenga ngome (Itookho) tatu - Elureko, Matungu na Eshikulu. Waarabu na Waswahili walitumia Kwa-Shiundu kama kitovu cha kukusanyia mali waliyopata kwa kutumia nguvu kutoka kwa Wajaluo, Babukusu na Wateso. Walijenga makazi yao na nyumba zao zikawa tofauti na za Abawanga ambazo walitumia kuhodhi mali hiyo. Kwa-Shiundu kukawa ni kitovu cha hujuma na dhuluma kwa jamii jirani (Makila: 1982), hasa Babukusu. Kutokana na kutendewa dhuluma, Babukusu walimchukia yeyote aliyetokea eneo la Kwa-Shiundu. Nabongo Mumia alipochukua hatamu za uongozi, aliendeleza sera za babake, huku akishirikiana na Waarabu na Waswahili. Ushahidi wa kihistoria waonyesha kuwa kufikia mwaka wa 1908 biashara za pembe za ndovu zilinawiri kwa sababu ya ushawishi wa kutawala wa Mumia akishirikiana na Waarabu na Waswahili (Aseka, 1989). Utawala wa Nabongo katika jamii ya Abawanga tangu zamani ulipewa hadhi kuu na kulingana na baraza la wazee la Abawanga – Kwalulukha kuloma – uongozi huu lazima uendelee na kutambuliwa (Nyangweso K.R. 12.4. 2008). Abawanga wana uhusiano wa karibu na Baganda, hasa orodha

ya watawala walioweka katika kumbukumbu yao ikuchunguzwa (Nyangweso K. R. 12. 4. 2008).

| | |
|---|---|
| Mutesa | 342- 445 |
| Kamaanyi | 445 – 535 |
| Muwanga | 535 – 645 |
| Mbwoti | 645 – 740 |
| Muwanga II | 740 – 860 |
| Wamoyi | 860 – 950 |
| Muwanga III | 950 – 1050 |
| Wanga | 1050 – 1140 |
| Wabala | 1140 – 1190 |
| Muswi | 1190 – 1274 |
| Chibwire | 1274 – 1354 |
| Masindalo | 1354 – 1464 |
| Chitechi | 1464 – 1554 |
| Netya | 1554 – 1617 |
| Osundwa | 1617 – 1717 |
| Wamukoya | 1717 – 1797 |
| Shiundu | 1797 – 1880 |
| Mumia | 1880 – 1949 |
| Shitawa | 1949 – 1980 |
| Mumia II | 1980 – hadi sasa. |

Abawanga wanajivunia wafalme ishirini kabla ya Nabongo Wanga. Kulingana na ushahidi simulizi, wafalme wa kwanza walitanguliwa na Mutesa I ambaye kwa mujibu wa baraza la Wazee wa Abawanga alitoka Misri na nduguye Simbi. Alimwacha Simbi kule Ethiopia na kuelekea hadi Uganda katika karne ya tano. Baadaye Abawanga wakaingia Kenya na kujenga makao yao katika eneo la Tiriki (Nyangweso R. K. 2008). Haya yanatokana na simulizi na yanahitaji ithibati ya kihistoria.

# BUTERE – MUMIAS DISTRICT




*Ramani inayoonyesha eneo kubwa la Abawanga, mkoani Magharibi, Kenya*

### 2.2.2 Uhusiano na Wageni

Maingiliano ya karibu kati ya Abawanga, Waarabu na Waswahili yalitokea katika miaka ya kwanza ya 1800. Abdalla (1971: 23) anatoa mifano ya baadhi ya hawa wageni kama Mwinyi Kombo Wazongo, Mwinyi Amanzi, Juma Ananga, Sheriff Hassan na Sheriff Omar (Wasiali, A 13: 4.2008). Sheriff Hassan alikuwa kiongozi wa dini, ya uislamu, huko Mumias akisaidiwa na Sherif Madhora, Sherif Omar na Sherif Sudi. Walimu hawa wa dini walichangia kukita mizizi kwa dini ya Kiislamu huko Kwa-Shiundu na kufikia mwaka wa 1904, ushawishi wa dini hii ulishinda nguvu za wamishenari wa Kikristo. Ukuaji wa dini hii ulikita Mizizi kwa sababu ya Shiundu na Mumia. Mumia alistahi sana mavazi ya kiislamu, chakula cha Uswahilini na hivyo akasilimu. Suleiman Fwaya, mtoto wa Eshibwabo alikuwa wa kwanza kusilimu, akifuatiwa na nduguze Mumia - Kadima, Murunga na Mulama. (Wasiali, A. 13:4.2008). Kwa hivyo, familia ya kifalme ilihusika pakubwa katika kujenga utamaduni wa Waswahili, mavazi, na lugha hapo Kwa-Shiundu na baadaye huko Elureko. Kufikia wakati wa kuingia kwa wakoloni, jamii ya Waislamu ilikuwa imepanuka pakubwa katika mji wa Mumias ikihusisha Abawanga, Wanyamwezi, Wamaasai, Wanubi, na Wasomali. Jamii ya Waisilamu ilijenga makazi yao yaliyoitwa 'Mjini'. Mzungu Joseph Thompson aliyefika mnamo mwaka wa 1883 alipendezwa na Mumia, hasa kwa ukarimu wake. Ithibati zilizopo zinaonyesha kuwa mabaki ya mwili wa Askofu Hannington aliyeuawa kule Luba, Busoga (Uganda) yalizikwa kwa heshima kule Mumias (Nyangweso R. K. 2008)[2]. Kulingana na Dealing (1974: 304), kwa sababu ya ukarimu huu na pia kwa sababu ya mahali pazuri pa eneo la Mumias,

---

[2] Mahojiano na Mzee Kandwi R. Nyangweso, Machi 2008

liliwavutia watawala wa kikoloni kama Dkt Carl Peters, Fredrick Lugard na Captain Smith. Wazungu hawa walipata nafasi kwa kuwa Mumia alikuwa ameweka mikakati imara ya utawala. Hivyo, kufanya Mumias kitovu mahsusi cha utawala wa eneo la Magharibi mwa Kenya na Uganda. Kamishna wa Uganda, Colville alimtuma Valet F. Spire kama mtawala huko Mumias. Kufikia mwaka wa 1895, Mumias ikawa sehemu mojawapo ya utawala wa Uganda katika mkoa wa mashariki chini ya uongozi wa Hobley (Osogo 1966: 129). Hobley aliweka sera kabambe ya utawala mojawapo ikiwa ni kuwanyamazisha maadui wa himaya ya Nabongo Mumia na utawala wa kikoloni kwa kijumla. Wajaluo wa Ugenya, Wateso, Wakabras, Babukusu ndio waliolengwa na kilele cha sera hii ya kunyamazisha maadui ilikuwa vita dhidi ya Babukusu vilivyotokea huko Chetambe na Lumboka mnamo mwaka wa 1895 (Makila, 1982). Kufikia mwaka wa 1910 mikakati ya utawala ilikuwa imekita mizizi na Mumia alitawazwa kuwa chifu mkuu wa eneo lote la Magharibi mwa Kenya.

Kutokana na historia hii, jamii ya Abawanga walikuwa kama kivukio. Wazungu na Waarabu waliwatumia ili kutimiza mahitaji yao. Babukusu walijikuta chini ya makundi yenye ushawishi mkubwa wa utawala. Babukusu wakalazimika kufuata na kutumikiza sera za mkoloni. Isitoshe, utawala ukaleta maingiliano zaidi ya jamii hizi na basi kusababisha mifanyiko ya kijamii. Lugha ya Kiswahili ikawa ndicho chombo mahsusi cha mifanyiko hii na kuanza kupenyeza Ubukusuni.

### 2.3.0. Kiishilio

Historia ya jamii za Babukusu na Abawanga ni msingi bora unaotuwezesha kufafanua na Kuainisha uhusiano uliojengeka baina yao katika misingi ya kuelewa nafasi ya utawala wa Nabongo Mumia katika kufanikisha uenezi wa lugha ya Kiswahili katika himaya yake, hasa eneo la Ubukusuni.

# SURA YA TATU

# DHIMA YA UTAWALA WA NABONGO MUMIA KATIKA KUENEZA KISWAHILI

## 3.0 Utangulizi

Sura ya pili ilishughulikia historia ya Ababukusu na Abawanga na namna jamii hizi zilivyoingiliana na athari ya maingiliano hayo. Uhusiano na athari ya mahusiano yao na jamii za kigeni-Waarabu, Waswahili na Wakoloni pia ulijadiliwa. Sura hii nayo itaainisha utawala wa Nabongo Mumia tangu maingiliano hasa na Waarabu na Waswahili hadi kufikia wakati wa wakoloni alipotawazwa kuwa Chifu Mkuu wa eneo la magharibu mwa Kenya. Sura hii basi katika kuchunguza utawala huu, inadhamiria kushughulikia nafasi ya utawala katika maenezi ya Kiswahili.

Sura hii itaonyesha namna maingiliano baina ya jamii hizi yalivyochangia kukieneza Kiswahili. Vile vile, utawala na mikakati aliyoweka Nabongo Mumia katika kufanikisha utawala wake ndio ulichangia pakubwa katika maenezi ya lugha ya Kiswahili.

## 3.1 Nabongo Mumia

Nabongo Mumia mwenyewe hakusoma katika shule za kawaida. Akiwa mtoto wa Mfalme, Nabongo Shiundu, alibahatika kukutana na wageni wa kwanza, Waarabu na Waswahili, walioingia katika himaya ya babake, Kwa - Shiundu . Ushahidi uliotolewa unaonyesha kuwa Shiundu alikuwa mzungumzaji wa

Kiswahili kwa sababu ya maingiliano haya na wageni (Wasiali, 2008), (Wamukoya, 2008), (Nyangweso, 2008).



The late Nabongo Mumia Shiundu of the Wanga kingdom.

Mumia alipata msingi bora na Kiswahili kuwa mamake alikuwa kati ya wale waliopendwa na Nabongo Shiundu. Mumia alikumbatia dini ya Kiislamu na kuisaidia kukita mizizi. Wasiali anasema kuwa Omuwanga wa kwanza kusilimishwa ni Suleiman wa Fwaya mtoto wa Eshibwabo. Kazi yake ilikuwa kuwabebea Waswahili na Waarabu mizigo. Kusilimu kwa Mumia kulichangia kusilimishwa kwa ndugu zake wote – Kadima, Murunga, na Mulama. Dini ya Kiislamu ilichangia pakupwa sana katika kueneza lugha ya Kiswahili.

Nabongo akiwa katika nafasi yake ya utawala kama chifu mkuu aliweka mikakati mahsusi ambayo ilichangia kukua kwa Kiswahili. Kwanza, aliwateua watawala waliokuwa na ufahamu katika lugha ya Kiswahili. Wale watawala walihakikisha sera ya lugha ilitiliwa maanani na ilifaulu – "LAKE NENO NDILO" - kama alivyojulikana Nabongo Mumia. C. Hobley anakiri katika kitabu chake kuwa ingawa Mumia hakusoma, alikuwa shupavu na ananukuliwa hivi kama alivyosema Wamukoya, A, (2008).

> 'Ni mtu aliye na elimu ndiye anayeweza Mumia'[3].

Utawala wake ulistahiwa na Mkoloni maana aliharakisha utekelezaji wa baadhi ya sera za mtawala kwa kutumia 'Mabalozi wake' huku lugha ya Kiswahili ikichukua kuwasilisha ujumbe. Hivyo basi mikakati iliyowekwa ya utawala na sifa zake za kimsingi zilichangia pakubwa maendeleo ya lugha ya Kiswahili barani. Mumia alitumia akili na hata ujanja kuhakikisha anatimiza malengo yake. Kisa ambacho alipanga njama na wasichana wa Kiwanga ili kujamiana na Waswahili cha ajabu. Walipofanya mapenzi na wasichana hawa wengine walipata mimba na kuwalazimu Waswahili kujenga makaazi ya kudumu huko Mumias. Hii inaashiria uhusiano aliokuwa nao wa karibu na hawa wageni waliochangia kupalilia matumizi bora ya lugha ya Kiswahili kwa Abawanga na watawaliwa wengine kama Babukusu.

---

[3] Mumia needs a well educated person

### 3.2 Misingi ya Utawala wa Nabongo Mumia

Nabongo Mumia alikuwa mtoto wa Nabongo Shiundu aliyetawala kati ya Miaka ya 1841-1882. Shiundu ndiye aliyejenga mizizi na Waarabu na Waswahili katika misingi ya dini, biashara na utawala. Ukuaji wa asasi hizo tatu ulichangia pakubwa upanuaji wa makazi yake ya Kwa-Shiundu na Elureko. Uhusiano huu na wageni hawa yaani Waarabu, Waswahili na baadaye Wakoloni ulitokana na sababu kubwa ya kudumisha usalama kwani milki yake ilizungukwa na jamii hasimu, wakiwemoa Wajaluo na Babukusu (Nyangweso K.R.12.4.2008).

Nabongo Mumia (1849-1949) alipochukua hatamu za uongozi mnamo mwaka wa 1882, aliendeleza sera hizo hizo za babake. Alijenga hata zaidi uhusiano huu, hasa na Waingereza. Kufikia Mwaka wa 1895 Makao makuu ya utawala wake yalikamilika huko Mumias.

Makao haya yalikuwa muhimu kwa Mwingereza kwa sababu yatahakikisha kuwa shughuli za utawala hazitatiziki, hasa na jamii hasimu na pia misafara ielekeayo Uganda ya kibiashara, wamishonari na wasafiri haitatiziki. Wageni waliotembelea eneo hili kama Joseph Thompson na J. Martin (1883), Fredrick Johnson na Ernest Gedge (1889), Dr Carl Peters (1890), Fredrick Lugard (1889), Captain Smith (1891), Sir Gerald Portal 1893 (Dealing 1974:300-4,Were 1967:156) walihitaji usalama.

Nafasi nzuri ya kijiografia (ukatikati wa mji huu) iliweka msingi bora wa utawala maana Uganda ilitegemea Mji huu kwa upande wa bidhaa kutoka pwani kama vile bunduki na mavazi. Eneo hili la Mumias pia lilizalisha vyakula kama mahindi, mawele na maimbi miongoni mwa biashara ya mifugo vilivyosafirishwa hadi Uganda. Mumias ukawa mji mwingine wa muhimu baada ya Machakos na Fort Hall.Uhusiano wa awali na Waswahili ulisaidia kupanua mji huu. Hivyo kufikia wakati wa kuingia mkoloni, ulikuwa kitovu cha utawala, biashara na utamaduni wa kistaarabu (Stitcher 1982:10-12, C.Hobley, 1970:79-81). Hobley, (1970:81) anukuliwa akisema.

> Kama kijiji chake kilivyokuwa tangu utawala wa babake 'Sundu',
> kitovu cha biashara kwenye barabara kuu ya kwenda Uganda,
> mji huu ulikuwa mahali pazuri pa kujenga stesheni ya utawala.

Mumias ikawa makao makuu ya utawala wa eneo la magharibi mwa Kenya chini ya Kampuni ya IBEA. Mumias ikawa kitovu cha utawala chini mkoa wa mashariki ya Uganda.

Kwa nini Mumia aliukumbatia utawala wa mkoloni? A. Wamukoya (4.4.2008) atoa baadhi ya sababu zilizomfanya Mumia kuungana na Wakoloni. Mumia alitazamwa kama kiongozi mwenye ukarimu kupelekea kupendwa na Wakoloni. Hii ilitokana na kuzikwa kwa mwili wa Askofu Hannington (1870) aliyeuliwa kule Uganda. Mabaki yake yalihaulishwa hadi Mumias na hadi sasa kaburi la Hannington limehifadhiwa kule Mumias. Kitendo hiki kiliinua hadhi yake na basi kuwa kiongozi wa kutegemewa. Pili, ushirika wao uliotokana na haja ya kiusalama.

Himaya yake ilikuwa hatarini kwa sababu ya Wajaluo na Babukusu ambao uhasama wao ulisababisha kukwamisha shughuli za usafiri, biashara, na utawala katika eneo hili. Kwa hivyo mkoloni alikuwa katika nafasi nzuri ya kuwanyamazisha maadui hawa.

Tatu, Mumia alikuwa na lengo la kulipiza kisasi. Babukusu waliwaua askari wake wenye asili ya Kinubi na Kisomali walipokuwa wanajaribu kunyang'anya Babukusu bunduki walizokuwa wameuziwa hapo awali. Nne, Mumia alitarajia kupata zawadi na misaada zikiwemo bunduki kutoka kwa Mkoloni. Tano, Milki ya Abawanga ilikuwa kwenye barabara kuu kuelekea Uganda, eneo lenye rutuba, vyakula na kwa bei nzuri. Sita, kulikuwa na ushindani juu ya utawala na nduguye Sakwa na hivyo alitarajia kupata msaada wa mkoloni ili kuimarisha mizizi yake ya utawala. Ushindani huu ulitokana na sababu kuwa awali babake Nabongo Shiundu alimwona kama aliyekosa sifa za uongozi na utawala. Mumia alitawazwa kutokana na njama za mamake. (Kenyanjui, 1992:16, Osogo 1967). Sakwa M'sake (1971) ana mtazamo ufuatao kuhusu ushirika wa Nabongo Mumia na wageni mbalimbali, hasa Waarabu kwa Wazungu. Anukuliwa hivi:

> Swali kwamba Mumia alikuwa akifanya vizuri au vibaya kwa kushirikiana na Waarabu na baadaye Wazungu ni la kiakademia lililokuwa muhimu kwake ni ama achague kupoteza milki yake kwa Wajaluo au akubali msaada wa Wazungu .Uhai wa himaya yake ilihitaji jicho lake pevu.

Ingawa Mumia alihitaji msaada wa wageni hawa itakuwa vizuri pia kukubali kuwa hata hawa wageni walihitaji msaada wa Nabongo Mumia. Mzungu alihitaji kutekeleza majukumu yake ya utawala. Sera zake zingefanikiwa tu kutokana na

ushirika wa Nabongo Mumia kwa sababu ya umuhimu wa himaya yake katika eneo hilo la Magharibi mwa Kenya.

Kulingana na P. M. Nanjiira (2008), Mumia alitawala kutoka Jinja (Uganda) hadi Naivasha (Kenya) akipakana na Chifu Kinyanjui. Eneo hili lilifikiriwa kama mojawapo ya mkoa wa Mashariki wa Uganda (1895) kutokea wakati Mumia alipotawazwa kuwa Chifu Mkuu mnamo 1910. Kutawazwa huku kulitokana na kamishina wa Uganda, Colonel H. Colville kumtuma Valet F. Spire kama mtawala 1894. Mwaka wa 1895, C.H. Hobley alichukua nafasi ya Spire. Mumias ukawa mji wa kupanga mashambulizi na mwaka huo huo, 1895, akaongoza mashambulizi dhidi ya Babukusu na kuwashinda katika vita vya Chetambe, 1895 ambapo Babukusu wengi waliuawa na kukubali utawala wa Mkoloni (Mutoro, 1976)


Baada ya Nabongo Mumia kutawazwa kama Chifu Mkuu alianzisha mikakati ya haraka ya kuwatawala hawa mahasimu wake kwa kuwa sasa jamii zote, hasa za Magharibi mwa Kenya zililetwa chini ya utawala mmoja wa Nabongo Mumia (Aseka, 1989:184) na kujenga ngazi ya utawala kati ya mwaka wa 1902 hadi mwaka wa 1914. Kwanza, aliwatuma marafiki na ndugu zake kuwa Machifu katika maeneo haya:

| **Eneo** | **Chifu** |
|---|---|
| North Bukusu | Suleiman Murunga. |
| South Bukusu | Sudi Namachanja |
| Luo | Mwanza |
| Marama | Mulama |
| Samia/Nyala | Kadima |
| Tachoni | Shiundu Makenga |
| Tsotso | Ambani Sakwa |

Kwa Mujibu wa Wamukoya (2008) na Nyangweso (2008), hawa machifu waliitwa 'Mabalozi' wa Nabongo Mumia. Uteuzi wao ulifanywa kutokana na sababu kwamba wao walikuwa Waislamu na weledi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hii sababu ya pili ni muhimu maana sera za kikoloni hazikuwa budi kuendelezwa katika lugha ya Kiswahili. Mabalozi hawa waliingiliana hapo awali na Waarabu na Waswahili hivyo kukifahamu Kiswahili. Eneo la Ubukusuni liligawanywa katika sehemu mbili kwa sababu ya ukubwa wake - South Bukusu na North Bukusu.

Maeneo haya mawili yaligawanywa katika maeneo madogo ili kukidhi mahitaji ya watawaliwa. Kugawanywa huku kulitekelezwa mwaka wa 1959 South Bukusu iligawanywa katika maeneo mawili ya utawala. Maeneo haya yalikuwa East Bukusu na West Bukusu. Eneo la North Bukusu liligawanywa katika maeneo matatu ya utawala. Maeneo hayo yalikuwa Kimilili, Bokoli na Ndivisi. Kuyagawa maeneo haya kuliwezesha uajiri wa machifu wapya chini ya utawala wa Nabongo Mumia.

**Eneo la Utawala Ubukusuni**




*(Mchoro huu unaonyesha watawala wa Babukusu hasa wakati wa Ukoloni - kwa mujibu wa mahojiano kati ya mtafiti na P. Nabangi tarehe 26.4.08 na A. Wamukoya tarehe 4.4.08)*

Ngazi ya utawala wakati huu ilikuwa imechorwa mahususi kuanzia kwa Wakoloni hadi kwa Waafrika kwa mfano:

P.C (Wazungu)

↓

D.C (Wazungu)

↓

Chifu Mkuu (Mwafrika- Nabongo Mumia)

↓

Chifu (Mwafrika)

↓

Lukongo (Naibu wa Chifu)

↓

Mulango (Waafrika)

↓

Kisoko (Waafrika)

*(Kumbuka nafasi ya D.O ilibuniwa baadaye tu)*

"Mulango" alikuwa na hadhi kuu kuliko Kisoko. Jina hilo linatokana na kazi yake maana yeye huelewa kila mlango wa watu anaowatawala na kusaidia kurahisisha utawala. Kisoko alikuwa kama Tarishi au anayetumwa kokote kule na Mulango ili

kupasha ujumbe kutoka kwa watawala wakubwa. Jina lake latokana na hali yake ya kutoka mlango mmoja hadi mwingine kwa mujibu wa kupasha ujumbe (*Asoka busa*)[4] ili kutekeleza sera za Mkoloni (Webi J. 2008, Cheloti. H. N. 2008).

Itakuwa bora kuchunguza misingi ya kuchaguliwa kwa Watawala hawa, hasa katika enzi hii ya Ukoloni. Wengi wa watawala hawa walichaguliwa katika misingi ya uhusiano wa karibu na wakoloni na Nabongo Mumia.

Sudi Namachanja alizaliwa katika familia ya watawala. Babake Sudi, Namachanja wa Khisa kutoka ukoo wa Bakhoone ndiye alikuwa kiongozi wa kwanza wa Babukusu kuchaguliwa na Mkoloni. Uteuzi wa Namachanja wa Khisa ulitokana na uhusiano wake wa karibu na Nabongo Mumia. Babake Sudi mara kwa mara alipokea wageni katika Ikulu yake kutoka Mumias na ikamlazimu kumwajiri mwalimu wa kibinafsi ili kumfunza Sudi Kiswahili. Mwalimu wake Sudi, Matere wa Mbita, alikuwa mzungumzaji mzuri wa Kiswahili. Ueledi wake ukapelekea Sudi kutilia makali Kiswahili chake. Kwa sababu mamake ndiye aliyewapokea wageni kutoka Mumias hasa Waswahili, Abawanga na Waarabu Sudi akaingiliana nao sana. Baada ya kifo cha babake Sudi, Maelo alichukua uongozi huku Sudi akiwa askari wake. Hata hivyo, Sudi ndiye alikuwa akifanya shughuli zote za utawala kwa niaba ya Maelo. Mkoloni na Mumia walimpendelea yeye na kumtawaza kuwa Chifu, 1907 (Makila F. E., 1978:215: Nabangi P. 2008). F. Makila (1978:209) anasema kuwa jina Sudi lilitokana na Mswahili

[4] Mtawala wa kiwango cha chini kabisa katika himaya na Nabongo Mumia. Istilahi hii ya Kikubusu huonyesha kuwa, kazi yake ilikuwa ni kuzungukazunguka kutoka nyumba moja hadi nyingine.

aliyekuwa mfanyi biashara wa watumwa kwa jina Sudi wa Pangani. Lakini Nabangi (2008) anasema kuwa awali aliitwa Saidi lakini jina hilo likabadilika kutokana na matamshi ya Wakoloni na kuwa Sudi ingawa aongezea kuwa ni jina la msimbo tu au la ujana. Katika misingi hii ya maingiliano na wageni Sudi alisilimu kusaidia kukita mizizi dini ya Kiislamu. P. Nabangi (2008) anapinga madai haya. Ingawa Sudi aliingiliana na Waswahili, hakusilimishwa na wakati wa kifo chake (1971), Sudi alikufa kama Mkatoliki kwa jina Joseph Peter Sikata.

Mawazo haya ya mwisho labda yanapotosha ukweli. Ushahidi simulizi na maandishi ya Historia yanashadidia uhusika wa Sudi katika dini ya Kiislamu na kwa hivyo madai kama haya ni ya ubinafsi ikikumbukwa kuwa familia hii ilijaliwa kuwa na Kadinali wa Kikatoliki Maurice Otunga na kwa hivyo kuhalalisha msimamo wa familia kuwa hakusilimu. Kwa hivyo kuchaguliwa kwa Sudi kunadhirisha mambo haya: Sudi alizaliwa katika ukoo wa utawala ambapo babake ndiye alikuwa kiongozi wa kwanza wa Babukusu. Babake Sudi basi akamtayarisha kupanda ngazi ya utawala. Alikubali na kutoa ushawishi mkubwa kuhusu dini ya Kiislamu. Ushawishi wake ulisaidia kukita kwa mizizi ya dini ya Kiislamu na hii inadhihirika hasa alipoyapendelea sana mavazi ya Kiislamu. Sudi kabla ya kuchukua uongozi, alikuwa askari mwaminifu kwa mkoloni na Mumia kuchangia kuchaguliwa kwake. Msingi alioupata katika kujifunza lugha ya Kiswahili na mwingiliano na wageni mbalimbali ulimsaidia kurahisisha na kufanikisha sera za kikoloni. Sifa hizi zilimpa nafasi bora ya uongozi na kuwa kiongozi mtajika.

Mfano mwingine mzuri ni wa Musa Amtalla (Abdullah) (1879-1973) mtoto wa Lukongo Mayeku wa Pepela. Musa Amtalla hakupelekwa shuleni lakini aliajiriwa mwalimu wa kibinafsi ili kumfunza lugha ya Kiswahili na akakimudu ipasavyo. Sifa hii ilimfanya kuajiriwa na Mzungu mmoja huko Mumias ili kufanya kazi za nyumbani (Omubenderi au Omutopi) ambapo aliboresha uelewa wake zaidi wa lugha ya Kiswahili. Mwaka wa 1916, alisilimishwa na baadaye aliajiriwa kama askari Kanga wa Nabongo Mumia. Alijifunza kuendesha baiskeli na kumwezesha kusafirisha ujumbe wa Mumia alikotumwa. Amtalla alipandishwa cheo na kuwa Lukongo huko Bokoli baada ya babake kung'atuka uongozini. Mwaka wa 1929, Chifu Waluchio wa North Bukusu alipofukuzwa na Babukusu, Amtallah alichukua nafasi yake, (Amtallah Pwoka W. 30.3.2008)[5]. Mifano hii miwili – Sudi na Amtalla – inadhihirisha kuwa kuzaliwa katika ukoo unaotawala, ueledi katika matumizi ya Kiswahili na kukumbatia dini ya Kiislamu ni masuala muhimu yaliyochangia kuchaguliwa kuwa viongozi. Musa Amutalla na Sudi Namachanja ni viongozi walioweka misingi ya utawala Ubukusuni kwa sababu ya uaminifu, utiifu na ukuruba wao kwa mkoloni na Nabongo Mumia.

Watawala wote waliofuatia walikuwa ama ni watoto wa Sudi na Musa au wanajamii. Ushawishi wao ulijenga mizizi hadi katika karne ya ishirini na moja. Musa Amtallah aliyetawala North Bukusu alituzwa medali kwa kazi yake nzuri na Sir Robert Brooke (8.6.1939).

---

[5] Mahojiano na Amtalla Pwoka mwezi Machi, 2008.

Hebu tuchunguze majukumu ya hawa Watawala na namna majukumu haya yalivyoendeleza lugha ya Kiswahili. Utawala wa Mkoloni kupitia Watawala hawa Waafrika uliendeleza sera zifuatazo:

- Kuhakikisha amani inadumishwa na sheria inafuatwa kama ilivyoandikwa.
- Kuhimiza maingiliano baina ya jamii zilizotawaliwa, na hasa zilizojenga uhusiano wa karibu na mkoloni kupitia katika utawala wa Nabongo Mumia.
- Kuhakikisha mimea mahsusi inapandwa ili kutimiza mahitaji ya mkoloni, ambapo Waafrika hawakuruhusiwa kupanda mimea fulani fulani kama kahawa na majani ya chai.
- Kuhimiza kwamba ustaarabu na maadili mema yanayokubaliwa na jamii na hasa yanayoegemea tamaduni za mkoloni, yanazingatiwa.
- Kuwalazimisha watoto kwenda shuleni, huku machifu wakisaidia katika kujenga baadhi ya shule.
- Kukusanya ushuru.
- Machifu kusimamia kamati ya maendeleo ya Lokesheni hasa katika Sekta ya Elimu, afya ya umma, kilimo, utamaduni, ujenzi wa miradi za serikali mfano daraja na barabara.
- Pia Machifu kuwakilisha mkuu wa wilaya katika kiwango cha Lokesheni, na hivyo kuwa kiunganishi cha utawala wa mkoloni na umma (Waafrika).

Majukumu haya yalitekelezwa katika himaya ya Nabongo Mumia. Itakuwa vyema kuyachunguza ili kuainisha namna yalivyochangia katika kueneza Kiswahili.

Wakoloni, hasa watawala, walipelekea kujifunza lugha ya Kiswahili na baadaye kutahiniwa katika lugha hiyo katika kiwango cha kitaifa kwanza ndipo waajiriwe kama watawala katika maeneo mbalimbali nchini Kenya (Cheloti, H.W.2008). Watawala, hasa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, walikifahamu Kiswahili kwa sababu ilikuwa lugha ya utawala. Waliandaa mikutano yao na wananchi- Baraza - na wao walitumia Kiswahili huku '*Mtapita*' (Mkalimani) akitafsiri katika Kiluhya. Okumu ndiye anayejulikana kama mkalimani mkuu kutoka makao makuu - Kakamega. Aliheshimiwa kwa sababu ya uelewa wake wa Kiingereza na Kiswahili. Hii ilipelekea kila chifu kuwa na 'Mtapita' wake na katika historia ya Babukusu, Wabomba na Matere waliokielewa Kiswahili vizuri wakapata hadhi hii ya '*Utapita*; ikikumbukwa kuwa Matere ndiye alikuwa mwalimu wa Sudi Namachanja. Taarifa zozote kutoka kwa LEGCO ziliandikwa katika Kiswahili ili kuwafikia Machifu wote.

Ni muhimu kusema kuwa watoto waliozaliwa wakati wa siku ya mikutano na mabaraza waliitwa Baraza. Sera hii ya utawala ilizua misamiati mingine kama ushuru, nyongeza, karani, Juma, mlango. Watoto waliozaliwa Ubukusuni wakachukua majina haya – Busuru, Nyongesa, Karani, Juma na Matifari.

Mtawala aliitwa Mulango kwa sababu alielewa kila mlango wa watu aliowatawala.

Kila chifu alipaswa kuwa na Baraza lake kila Jumatatu maana ujumbe kutoka kwa utawala wa mkoloni uliwafikia kila wiki. 'Lukongo' na 'Kisoko' walihakikisha kuwa kila mtu anahudhuria baraza la Chifu. Kisoko waliingia kila mlango kuwajulisha Babukusu. Ilikuwa muhimu kwa sababu yeyote aliyekosa kuhudhuria baraza alikiuka sheria na alipaswa kuadhibiwa vikali na askari wa Chifu. Waliokaidi walipata kichapo cha mbwa-koko.

Baraza la chifu lilikawa kitovu cha elimu kwa wananchi. Ujumbe mpya uliwafikia wananchi kwanza kwa lugha ya Kiswahili na kisha mkalimani akawafahamisha katika Kibukusu. Ingawa Wamukota (31.4.2008), anasema kuwa Babukusu walihimizwa kukitumia Kiswahili kupitia baraza za Chifu, H.W Cheloti (2008) anasisitiza kuwa ilikuwa lazima Babukusu kutumia Kiswahili maana walilazimishwa kununua mavazi hasa ya kaniki na kanzu ili kuyavaa na basi kuanza kuingiza msamiati mpya wa Kiswahili katika mazungumzo yao. Hata hivyo P. Wamukota (31.4.2008), anasema kuwa heshima waliyompa '*Mtapita*' hasa kwa sababu ya ujuzi wake katika lugha hii na hadhi yake katika jamii, iliwachochea wengi wao kupandwa na mshawasha wa kukizungumza Kiswahili kwa sababu kilikuwa na hadhi kuliko Kibukusu.

Baraza za watawala hawa basi zilichangia nao katika kukikuza Kiswahili muda baada ya muda kuanzia baraza la Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya hadi kwa Machifu. Swala la amani na kuzingatia sheria lilikuwa muhimu sana. Abawanga waliwaita Babukusu '*Nywele Ngumu*' labda kutokana na tabia yao ya kuachilia nywele ndefu iliyopakwa udongo mwekundu na kwamba hawakuwa rahisi kufuata amri ya Nabongo Mumia na Machifu wake. Babukusu wanakanusha madai haya kwa kusema kuwa askari wa Nabongo Mumia na Murunga walikuwa '*Wangisieki*' yaani walafi na walaghai. Vitendo hivi vya kikatili dhidi ya Babukusu vilivyogunduliwa ndipo basi Mkoloni na Mumia wakawachukia tu na basi kuwaita 'Nywele ngumu'. Kwa hivyo baraza la Machifu lilikabiliana na baadhi ya Babukusu waliokaidi amri ya kukata nywele na kufuata mkondo wa utawala.

Waliovuruga utawala walichapwa na askari wa Machifu, Murunga, mfano, Murunga, Amtallah na Sudi kwa amri ya Nabongo Mumia na hata wengine kufungwa jela. Katika baraza kama hizi za kudumisha amani na sheria ndipo walipopata mafunzo ya ustaarabu na ya lugha ya Kiswahili.

Utawala huu pia ulihimiza maingiliano mema na jamii zilizotawaliwa. Jamii ya Wasabaot na Babukusu walihimizwa kuingiliana. Maingiliano yalisaidia kubuniwa kwa lokesheni mpya ya Elgon, 1946, ambapo Chifu Jacob Cheptek Tendet Kiptek alichaguliwa kama chifu, jambo lililoungwa mkono na Babukusu maana eneo hili lote lilikuwa chini ya Chifu Amtallah. Ushirikiano huu ulizalisha

maendeleo karibu na watu-Wasabaot-hasa kiongozi mpya aliyewaletea mapya kupitia hizo baraza na kustawisha lugha. Maingiliano kati ya Babukusu na Wasabaot hasa kibiashara, ndoa na hata katika shughuli ya utawala, yalisaidia matumizi ya Kiswahili baina ya jamii hizi mbili na kukikuza polepole (Naibei H 2008).

Ukusanyaji wa ushuru ulikuwa jukumu la Machifu. Kila Chifu alikuwa na karani wa ukusanyaji kodi au ushuru. Utawala wa mkoloni uliajiri karani katika msingi wa kuwa amesoma vizuri hadi kiwango fulani cha elimu. Wanafunzi wa shule za msingi wakati huo walitahiniwa katika darasa la nne na kufanya mtihani wa pamoja wa kuingia darasa la tano (C.E.E.) na mtihani wa darasa la nane (KAPE). Karani wa kodi alipaswa kuwa amepitia kiwango hiki, anakielewa Kiswahili na Kiingereza ili kutekeleza majukumu yake barabara.

Makarani hawa walikuwa na ushawishi mkubwa enzi hizo, kwani wengi wao walipandishwa cheo na kuwa Machifu. Mifano mizuri ni ya Nabutola J.Muganda aliyekuwa karani wa kodi wa Lukongo George Henry Kerre na Chifu Sudi Namachanja. Nabutola alipanda cheo baadaye na kuwa chifu wa eneo la West Bukusu. Ni msomi aliyetahiniwa mtihani wa 'C.E.E.' na baadaye 'KAPE' hivyo basi kuwa na msingi bora wa kuajiriwa. Kiswahili kilitahiniwa kama somo.

Chifu Ali Wamukoya, awali aliajiriwa kama Karani wa Korti na baadaye karani wa kodi huko South Wanga (1937-9). Alipata elimu yake katika shule ya serikali

ya Kakamega. Isitoshe Chifu Richard Manya aliajiriwa kuwa karani wa kodi (1948-1960) na baadaye kupandishwa cheo kuwa Chifu wa eneo la Matungu. Alisoma hadi darasa la tatu na baadaye kujiunga na jeshi (KAR) ambapo alishiriki katika vita vya pili. Manya anasema kuwa waliwalipisha wananchi kodi ya senti hamsini.

Ushahidi huu uliokusanywa kutoka kwao wenyewe walidhihirisha umuhimu wa jukumu la utawala hasa lilipowaajiri waliotekeleza sera ya kitawala. Elimu katika Kiswahili na Kiingereza ilisaidia kutekeleza majukumu yao hasa kwa jamii ambazo hazikuelewa Kiswahili.

Walikuwa mstari wa mbele katika mabaraza ya watawala kuanzia mkuu wa mkoa hadi kwa machifu. Walihakikisha wanatembelea kila boma chini ya ushawishi wao. Maingiliano haya yalichangia kukuza lugha ya Kiswahili. Machifu ndio walikuwa wenyekiti wa kamati ya maendeleo katika kila lokesheni. Kila Lokesheni ilikuwa na kamati iliyoundwa ikihusisha maafisa wa serikali kutoka kila sekta chini ya chifu kama mwenyekiti. Walijitwika jukumu la kuhakikisha kuwa maendeleo yanatekelezwa kuashiria makali yao uongozini. Kwa hivyo waliitisha mikutano au mabaraza ambapo wananchi walielimishwa juu ya kushiriki katika maendeleo. Mikutano au mabaraza haya yaliongozwa na Chifu huku akisaidiwa na maaafisa wa serikali waliohusika na, kila sekta mfano maafisa wa elimu, afya, ujenzi, kilimo, maji. Maafisa hawa waliajiriwa katika misingi ya wao kuelimika na walitoka jamii mbali mbali katika magharibi mwa Kenya .Kwa

hivyo shughuli zote ziliendeshwa katika lugha ya Kiswahili huku 'Mtapita' akitafsiri kwa Kibukusu basi kukifanya Kiswahili kupata hadhi maana shughuli zote za serikali zilihusisha Kiswahili kama chombo cha mawasiliano. Hata baada ya vikao vya Machifu maafisa wanaohusika katika kila sekta ya maendeleo walitembelea wananchi nyumbani kwao na kuwahusisha moja kwa moja kwa yale waliyoafikiana hasa mfano namna ya upanzi wa mimea fulani kama vile kahawa, au ujenzi wa barabara na hivyo kuchangia maingiliano zaidi. Kwa kufanya hivi wananchi wakaanza kuwa na mazoea ya kutumia Kiswahili Ubukusuni. Katika sekta ya elimu, chifu alihakikisha kuwa lokesheni yake ina shule.

Aliwahusisha wananchi kujenga na pia kusaidiwa na Wamishenari. Chifu alipaswa kuhakikisha kuwa wazazi wanawapeleka watoto shuleni na yeyote aliyekosa kupeleka mtoto shuleni, kulingana na R. Manya (2008), alichapwa viboko hadharani au kutupwa gerezani kwa mwezi mmoja. Chifu Suleiman Murunga labda alichukiwa na Babukusu kwa jitahidi zake za kuwalazimisha kuwapeleka watoto wao shuleni na hata kuwafunga baadhi yao. Mchango huu wa Machifu ulisaidia sana kupitia mizizi Kiswahili maana kilifunzwa shuleni nakuchangia maenezi yake.

Machifu wote Ubukusuni walikuwa 'sikio na jicho' la Mkoloni kupitia Nabongo Mumia. Mradi walikuwa wawakilishi wa serikali, basi walikuwa ni kiungo muhimu katika maswala yote ya serikali yaliyopaswa kutekelezwa. Chifu aliyezembea kazini alifutwa kazi maana kulingana na A. Wamukoya (2008),

Nabongo Mumia alistahiwa, na methali hii '*Lake Neno Ndilo*' ndiyo ilikuwa kama kigezo cha utekelezaji kazi. Nabongo Mumia aliwatia moyo Machifu wake kila mara katika mikutano yake kwa methali '*Panapo na nia pana njia*'. Wananchi waliokiuka amri basi chifu alipaswa kutumia sheria ya chifu kutekeleza kazi yake. J. M. Nabutola (2008), anakumbuka kwamba katika mwaka wa 1959 ambapo Babukusu wa Malakisi walikataa kulipa kodi, Nabutola na Mkuu wa Wilaya Bwana Windsor, wakiandamana na askari kumi na wawili waliwalazimisha Babukusu wa Malakisi kulipa kodi. Kwa upande wake, Lukongo akiachishwa kazi kwa kukosa kutekeleza majukumu yake.

Maswala ya Mashamba na kodi yalikuwa muhimu sana katika utawala huu wa Mkoloni na chifu alistahili kuhakikisha yanatekelezwa. Machifu walipaswa kuwa wazungumzaji wazuri ili kuwashawishi wananchi kutekeleza sera za kikoloni kwa vyovyote vile. Uadilifu lilikuwa swali muhimu. Mfano mzuri ni wa Lukongo Maruti kukali wa Webuye aliyekosa kutekeleza wajibu wake, akasababisha kufutwa kazi (Pwoka Amtalla, 2008). Ushahidi huu unaonyesha wazi kuwa watawala hawa kutokea kwa Wazungu hadi kwa Waafrika walikuwa na majukumu makubwa ambayo katika utekelezaji wake walitumia lugha ya Kiswahili, ikapata kuenea katika eneo la Ubukusu. Madokezo haya ya utawala yanaonyesha kuwa sera ya elimu nchini ilisaidia kueneza Kiswahili kwa sababu ya kutahiniwa katika mtihani wa KAPE. Babukusu watajika walijifunza Kiswahili na hivyo kukitumia katika shughuli za utawala. Mkalimani alizuka kuwa mtu muhimu katika jamii ya Babukusu kwa sababu ya weledi wake wa Kiswahili.

Isitoshe, baadhi ya maneno ya Kiswahili yalitoholewa na kuwa sehemu ya msamiati wa Kubukusu. Haya yalichangia maenezi ya Kiswahili Ubukusuni.

**Kiishilio**

Ni muhimu kukumbuka kuwa Kiswahili kilikuwa chombo mahsusi cha kutekeleza majukumu ya serikali. Machifu katika kutekeleza majukumu ya utawala walikitumia Kiswahili kama lugha rasmi ya serikali, Kiswahili kikapata nafasi ya kukua muda baada ya muda. Watawala hawakupendelea matumizi ya lugha za kienyeji maana zingekwamisha shughuli muhimu za biashara, kortini, utawala na maendeleo. Kwa jumla, walitetea ustawishaji wa Kiswahili maana kilivuka mipaka ya kisiasa na kiisimu na basi kutumiwa na watu wengi.

# SURA YA NNE

# NABONGO MUMIA NA ASASI NYINGINEZO KATIKA MAENEZI YA LUGHA YA KISWAHILI

## 4.0. Utangulizi

Katika sura iliyofafanua, tulichunguza dhima ya utawala wa Nabongo Mumia katika maenezi ya lugha ya Kiswahili Ubukusuni. Katika kueleza mikakati ya utawala katika kufanikisha sera za mkoloni, tulionyesha namna mikakati hiyo ilivyosaidia kuendea kwa misingi lugha ya Kiswahili.

Sura hii itachanganua asasi za siasa, dini, biashara, elimu, michezo, muziki, ndoa, korti za Kiafrika, reli, ajira na usetla katika maenezi ya lugha ya Kiswahili.

## 4.1 Uzalendo, Mwamko wa Kisiasa na Kitaifa Ubukusuni

Jamii ya Babukusu inajulikana katika historia kama wazalendo waliotetea utaifa wao. Jambo hili linabainika tunapomulika vita vyao vya kijasiri huko Lumboka na Chetambe, mnamo mwaka wa 1894 hadi mwaka wa 1895 dhidi ya mkoloni. Babukusu walikuwa na 'Manabii' waliotabiri kuingia kwa mkoloni na baadaye kunyang'anywa kwa uhuru wao.

Baadhi ya Manabii waliotukuka ni kama Maina wa Nalukale mtoto wa Mukitang'a na Wachiye wa Naumbwa. Kipindi cha unabii wa Maina wa Nalukale na utawala wa Babukusu ushuhudia umoja wa koo zote za Babukusu ambapo alijenga makao yake mahali alipopaita 'Sikulu sya Bukusu' (Mlima wa

Babukusu). Alitabiri kuingia kwa mkoloni na Manguliechi (2008)[6] anamnukuu hivi:-

> Enyi Babukusu, mtaendelea kuhamahama huku mkipigana na wageni. Mtazunguka Mlima Masaaba (Elgon) mara mbili ambapo mtakutana na joka kubwa –Yabebe- litakalowazuia kuhama zaidi na baadaye vita vikubwa vitazuka.



*Wanyonyi Manguliechi katika mavazi yake rasmi*
*(Mzee wa Baraza mtajika wa Babukusu)*

Utabiri huu ulithibitishwa katika kushindwa kwa Babukusu na Bamia (Teso), Barwa Bakwabi, na baadaye wakashindwa na Mkoloni katika vita vya Chetambe. Joka alilotabiri lilikuwa reli iliyojengwa kupitia nchi ya Babukusu kuelekea

[6] Mahojiano na Mzee Manguliechi tarehe 2.4.2008

Uganda. Baada ya utabiri huu, Maina alipotea ghafla na kigoda chake cha utawala.

Vita vya Chetambe na Lumboka (1894-5) vilizalisha kizazi cha kwanza cha wazalendo wa Kibukusu waliotumia kila mbinu kuleta uhuru wa nchi yao. Utabiri wa Maina wa Nalukale na baadaye utabiri wa Wachiye wa Naumbwa (Wa Ukoo wa Omutukwika Mukwangwa) ambaye alikuwa akitabiri matokeo ya vita kabla ya vita hivyo kutokea, uliwatia wazalendo moyo wa kujihami. Mmoja kati ya mashujaa wa kizalendo alikuwa Wakoli Okhwa – Mukisu. Wakoli Okhwa Mukisu ni kielelezo cha Wazalendo waliogundua kuwa mkoloni alikuwa na nguvu. Kwa hivyo, ilihitaji kutumia mbinu za kijanja, akili na ujasusi ili kumshinda. Wakoli alikuwa mtoto wa shujaa wa kivita Mukisu Lufwalula wa ukoo wa Omuyemba Mukhayama.

Ili kutegua kitendawili cha kumwelewa mkoloni vizuri, alijifunza Kiganda, Kisoga, Kiwanga na Kiswahili. Lugha hizi nne zilikuwa tegemeo lake. Alianza mikakati ya kidiplomasia na ujasusi kwa kufanya urafiki na Abawanga na Waswahili katika ngome ya Nabongo Mumia huko Mumias. Urafiki huu aliojenga ulisababisha kuajiriwa kazi kule Mumias kwa Mswahili aliyeitwa Namisi. Namisi alidhani kuwa Wakoli alikuwa Mganda maana Waganda walikuwa washirika wa Nabongo Mumia.

Wakoli aligundua jinsi Babukusu walivyochukiwa na mkoloni, Abawanga, Baganda, Bakhayo miongoni mwa jamii zingine zilizowazunguka. Huduma yake ilimsaidia kutilia makali na utumizi ya Kiswahili na kujenga urafiki na wageni wengine huko Mumias. Namisi, mwajiri wake, alimwamini na kumwonyesha mbinu za kisiri zilizoandaliwa kumwangamiza Mbukusu. Urafiki huu ulipelekea askari wa Namisi aliyeitwa Okwara Dindi, kumfunza Wakoli namna ya kutumia bunduki. Baadaye Wakoli aliiba bunduki na kuificha kule Lumboka. Baada ya Wakoli kufanya hivi, mikakati ya kununua bunduki na kujenga jeshi kisirisiri kule Lumboka. Alipohakikisha ameelewa mbinu za adui, alitoweka na kuanza kutetea nchi ya Ubukusu. Alikaribisha baadhi ya wanajeshi wa Mumia ambao hawakuridhika na hali ya maisha kule Mumias. Walibadilishana bunduki na vyakula na wakati mwingine waliwanyang'anya walinzi wa Mumia bunduki. F. Makila (1978: 234) anaonyesha jinsi askari sita waliokuwa wamejihami kwa bunduki wakielekea stesheni ya Ravine walivyotorokea Ubukusuni. Kamanda Spire aliyetaka bunduki hizo zirudishwe hakufaulu kwa sababu Babukusu walikataa.

Juhudi za Wakoli za kuwaleta Babukusu pamoja zililalisha matunda. Babukusu wakawa wanaingiliana na askari wa kigeni. Kwa sababu Babukusu walikuwa na uelewa wa Kiswahili, walifaidi mafunzo ya kijeshi. Spire alipotuma jeshi la Wasudan na Wazanzibari thelathini na mmoja, wote waliuawa isipokuwa mmoja tu. Huu ni ushahidi wa umoja wa Babukusu na mafunzo bora ya Wakoli. Katika mwaka wa 1895, Fredrick Jackson alituma jeshi la Wasudani 150, Waganda 500,

Wamaasai 200 chini ya kamanda William Grant. Ingawa Babukusu wengi waliuawa na kutorokea ngome ya Chetambe, Wakoli aliwaua Namisi na Okwara wa Tindi. Hadi leo Babukusu wanakumbuka juhudi zake za kizalendo kwa kutumia akili yake, urafiki na lugha ya Kiswahili katika kupeleleza, kuingiliana na maadui na kuwafunza wenzake, ili kuelewa maadui wao. Hadi sasa, Babukusu Wanamkumbuka Wakoli kwa wimbo waliomsifia nao:

> "Okhwa Mukisu Khamupa engeche, Okwara wa Tindi"
> "Mtoto wa Mukisu alimpiga Okwara wa Tindi kwenye goti lake"[7]

Ushujaa na maono ya hawa mashujaa ni jambo la kujivunia na ni kitovu cha motisha na la kujivunia kama wanajamii. Hawa ndio waliopalilia mbegu za mwamko wa utaifa uliotuletea uhuru barani Afrika. Hata ingawa Wakoli alikufa mwaka wa 1912, juhudi zake ziliendelezwa na mtoto wake Pascal Nabwana aliyezaliwa mnamo mwaka wa 1900. Nabwana ndiye alikabidhiwa na Wakoli vifaa vya kifalme vya utawala – 'Ekutusi, Lichabe na Ekhorere'[8]. Nabwana alitawala siasa la Mkoa wa Magharibi kati ya 1926 hadi miaka ya 1960. Ukoo wa Bayemba umeweka historia katika maisha ya Babukusu. Mbunge wa sasa wa Bumula, Bifwoli Wakoli, ni mjukuu wa shujaa Wakoli Okhwa-Mukisu (A. Khatambi (2008[9], W. Manguliechi, 2008, M. Tumbu, 2008[10], Makila F.E. 1978:224).

---

[7] Okwa Mukisu Khamupa engeche, Okwara wa Tindi
[8] Vifaa vya utawala miongoni mwa Babukusu
[9] Mahojiano na Mzee Khatambi Khasolo mwezi wa nne mwaka wa 2008
[10] Mahojiano na Mzee Tumbu Masinde mwezi Aprili, mwaka wa 2008

Ushujaa na ukakamavu wa viongozi hawa watangulizi ulipaliliwa na maono ya manabii wa awali waliohimiza kukataa kuingia kwa 'watu wekundu' watakaoabiri katika vyombo mfano wa 'stoo'. Manabii walikuwa wamesema kuwa, watu hawa wekundu wangebadilisha nchi yao kabisa kwa kuwa mila na tamaduni zao ni tofauti sana na Babukusu. Wakoli na mashujaa wengine waliomfuata walielekezwa na nguvu hizi za manabii katika jamii ya Babukusu.

Licha ya Wakoli kuwa kielelezo cha ushujaa, alitumia akili na ujuzi wa mkoloni na mshirika wake Mumia, ili kutetea nchi yao. Kiswahili kama chombo cha utawala, kilitumiwa vyema na Wakoli kwa kuwaunganisha Babukusu. Lugha hii ikawa silaha dhidi ya mtawala.msingi huu alioupalilia Wakoli ukawezesha Kiswahili kuenea Ubukusuni.



*Wanyonyi Manguliechi na Mtafiti wa kazi hii*

Mbegu hizi za uzalendo zilichipukia tena kwa shujaa Elijah Masinde Wanameme Okhwa Mwasame. Alizaliwa katika mwaka wa 1908 huko Chekulo. Baadaye walihamia Maeni karibu na Kimilili. Elijah anatazamwa na Babukusu kama nabii wa kizazi cha pili na shujaa aliyekuja kuokoa umma kutokana na dhuluma za ukoloni. Ushahidi wa kusimulia, unaonyesha kuwa alisoma katika Shule ya Msingi ya Chekulo na baadaye walipohamia Kimilili akajiunga ya misheni ya Jamii ya Marafiki ya Kamusinga (Friends African Mission). M. Tumbu (2008)[11] anasema kuwa Masinde alikuwa mchezaji hodari wa kandanda. Kutokana na jambo hili aliwavutia wafuasi wengi. Kati ya mwaka wa 1938 na 1942, aliajiriwa katika korti ya Kabuchai kama askari, lakini akakataa kufanya hivyo aliposhuhudia dhuluma dhidi ya Babukusu. Tumbu anaongezea kuwa muda alioutumia Elijah kama askari wa korti ulimsaidia kumsoma mkoloni na njama zake. Kwa kutumia kipawa chake cha uzungumzaji, alijenga kundi kubwa la wafuasi. Mnamo mwaka wa 1943, aliungana na Walumoli ili kujenga misingi thabiti ya Dini ya Musambwa. Inaaminika walisafiri hadi Lukulu kwa Masaaba (Mlima Elgon) ili kuzungumza na Wele Khakaba. Waliporudi, walipiga vita dhuluma za mkoloni kupitia migomo, fujo na mikutano ya hadhara, huku Elijah akijiita Omurumwa wa Nyasaye – Mtumwa wa Mungu (kulingana na kitabu cha Malaki 4:1 katika Agano la kale). Jukumu la Masinde basi lilikuwa ni kuletea Umma mwangaza ili kujinasua kutoka minyororo ya mkoloni. Dhuluma hizi zilikuwa kulipishwa ushuru, kazi ya lazima kwa malipo duni sana, kufanyishwa kazi katika miradi ya lazima kama ujenzi wa barabara, kunyang'anywa mali yao, hasa ng'ombe na mashamba na muhimu, walidai uhuru wa Mwafrika.

---

[11] Katika mahojiano yaliyofanywa kati ya Tumbu na mtafiti mwezi Aprili, 2008



*Elijah Masinde Okhwa Nameme, Kiongozi wa Dini ya Musambwa*

Kilio hiki cha Masinde kiliunganisha jamii ya Babukusu pamoja na jamii nyingine nyingi. Tumbu anakiri kuwa ufasaha wake wa kuzungumza Kiswahili na akiwa na kipawa cha kuzungumza kulimfanya kupata wafuasi kutoka Pokot, Uganda, Nandi, Kabras, Abanyala. Wakipsigis waliunda tawi lao waliloliita Dini ya Mbosho. Elijah Masinde akaibuka Kama kitovu na tegemeo la dini ya Musambwa iliyoleta jamii tofauti pamoja wakitumia dini kama kigezo kikuu cha kujinasua minyororoni. Kiswahili kikatumiwa kama chombo cha mawasiliano na kulingana na Simiyu V. (1997:45), Masinde aliwafikia Wakikuyu, mwaka 1947, kwa kuwatumia ujumbe kuwa waharakishe mapambano dhidi ya mkoloni maana Babukusu wameshajenga mikakati ya kumwondoa mkoloni. Ni mwaka huo, 1947, ambapo wafuasi wengi wa Dini ya Musambwa, wakiongozwa na Gabriel Wangila, Sichangi Khaoya na Wekuke waliuawa kule Malakisi na Mzungu aliyejulikana kama 'Khwa Namunyu Mujerumani' kwa kupigwa risasi. Walikuwa wanapinga dhuluma za mkoloni. Wakati huo huo Masinde alishikwa na kuwekwa jela kwa sababu Mkuu wa Wilaya, Bwana C.J Denton, alimwona

Masinde kama tishio kubwa kwa utawala wa mkoloni. Kushikwa kwake kulihamasisha wafuasi wake zaidi. Mwaka 1950, Wapokot walipinga kushikwa kwa Masinde. Matokeo yalikuwa kuuawa kwa Wapokot mia tatu kule Kolloa Affray na wengine kufungwa jela, ishara kuwa vuguvugu hili lilikuwa limeshika makali kama sauti ya kidini na kisiasa. Mkoloni akapiga marufuku kundi hili, 1948, na kushikwa na kushtakiwa kwa wafuasi wakuu kama vile Lukas Pkech (Kalenjin) aliyehukumiwa kifungo cha maisha na jaji Thacker, 1949. Huyu Jaji ndiye alimfunga Mzee Kenyatta. Pascal Nabwana alishikwa kwa sababu wakati huo alikuwa Rais wa muungano wa Babukusu na Bakisu na alituhumiwa kuwa alikuwa nyuma ya njama hizi za kuangamiza mkoloni. Wengine walioshikwa walikuwa Walumoli, Sitawa na Wekuke.

Masinde alifungwa Lamu, Kitale na Kisumu lakini hata hivyo, wafuasi wake hawakusita kushinikiza kufunguliwa kwake. Mahakamani, kwa sababu ya kipawa chake cha kuzungumza na matumizi mazuri ya Kiswahili, alijitetea ipasavyo. Mfano: (Mahojiano na Sajenti Kamitu Waitu)

A. **Masinde:** Tangu kuanza kwa D.Y.M, umeona nikiingia katika kambi ya serikali ya Malakisi?

   **Waitu:** Nimesikia tu, lakini sijakuona

   **Masinde**: Kule Malakisi, Watu walikuwa na mikuki?

   **Waitu**: Sikuona mikuki.

   **Masinde**: Nilikuwa katika fujo ya Malakisi?

   **Waitu** : Hapana.

### B. Mahojiano na Hakimu Cyril Herbert Williams

**Masinde**: Tangu nianzishe D.Y.M, nimempiga mtu yeyote kwa fimbo?

**Williams**: Hapana, sijasikia umempiga mtu.

**Masinde**: D.C ameniona mimi tangu aingie katika Wilaya hii?

**Williams**: Hapana, alikuona tu wakati uliposhikwa.

**Masinde**: Kuhusu ushuru, umeangalia daftarini na kugundua kuwa sijalipa ushuru?

**Williams**: Hapana, sijahakikisha.

**Masinde**: Kabla kuja nyumbani kwangu, mlisikia kuwa mimi napinga machifu wenu?

**Williams**: Sijui, nilisikia kuwa umekuwa na misururu ya mikutano tu.

*(Simiyu V. G. 1997:24-25)*

Hii ni dhahiri shahiri kuwa Masinde alikuwa shujaa aliyejawa kipawa cha kutetea walio wengi na alijitetea katika lugha ya Kiswahili. Mbegu yake ilichipuza na kuzalisha viongozi wengine wa miaka ya 1960 walioongoza shughuli za utaifa. Hili lilikuwa kundi la wasomi kama Masinde Muliro, Oginga Odinga, Tom Mboya, Ronald Ngala, miongoni mwa wengine ambao nao walishinikiza kufunguliwa kwa Jomo Kenyatta na wafungwa wengine wa kisiasa. Hizi zilikuwa juhudi za Masinde Muliro Mei, 12, 1960 akiwa LEGCO. Juhudi zake zilifanikiwa wakati mkoloni alipoondoa ilani ya hali ya hatari na kisha kuwafungua Kenyatta, Achieng Oneko, Paul Ngei, Wekuke na Elijah Masinde miongoni mwa wengine, (Simiyu V. 1997:26-7).

Ni dhahiri kuwa muungano wa wanajamii ni nguvu, hasa uongozi ukiwa thabiti. Masinde alijitwika mzigo huo ili kuwakumbusha wananchi haki zao. Vuguvugu kama Nomiyo Luo, Dini ya Musambwa, Dini ya Mbosho zilitetea msisimko miongoni mwa Wakenya, kupandisha shinikizo ili mkoloni alete mabadiliko, wakitetea uhifadhi wa tamaduni za Mwafrika, huku waking'ang'ania uhuru wa mtu mweusi. Mchango kama huu hauwezi kupuuziwa mbali. Ingawa vuguvugu kama hizi zilijikita katika jamii mahsusi, lakini zilipanuka kiasi cha kufikia jamii jirani. Maingiliano haya yalitokana na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Elijah Masinde alikuwa mweledi wa Kiswahili na wafuasi wake wote hadi sasa hutumia Biblia, hasa Agano la Kale katika mahubiri yao. Agano la kale limeandikwa katika lugha ya Kiswahili na Kibukusu wakati huu, ili kurahisisha mawasiliano kwa hadhira inayokusudiwa. Kando na kuwa Kiswahili kilitumiwa katika mahubiri, kiliwaunganisha Wapokot, Wanandi, Wakabras, Babukusu na Wanyala. Muungano huu ukawafungua macho kuwawezesha kupigania haki yao. Ingawa Masinde alikuwa adui wa mkoloni na wale machifu ambao walichaguliwa na Nabongo Mumia, alipata ufuasi mkubwa ambao ni wa kipekee. Mazishi yake, Juni 15, 1987, yalishuhudiwa na watu anuwai kutoka taifa hili la Kenya.

Madai kuwa Masinde alikuwa nabii au hapana ni ya kifalsafa ambayo ilijikita katika imani ya watu. Ni ajabu kuwa kando na Babukusu, jamii nyingine zilikuwa na imani na Masinde kama nabii na hunukuu Malaki 4:5

> Tazameni, nitamtuma Nabii Elijah, kabla ya sikukuu ya kuingia Jehovah……

Babukusu walishadidia kuwa Elijah Masinde alitabiri kuondoka kwa mkoloni na alikuwa na uwezo wa kutabiri ushindi wa timu ya kandanda. Waliofungwa naye jela, walimwamini kama nabii kwa sababu ya nguvu zake za kiajabu ajabu kwa hadhira yake. Masinde alikuwa mtanashati ajabu kwani mavazi yake yote yalikuwa meupe.

Kwa jumla, basi, Masinde ni zao la ukoloni katika historia ya Kenya. Utaifa wake ni zao la ukoloni, kwani wazazi wake walikuwa miongoni mwa kizazi cha mashujaa wa kwanza cha Lumboko na Chetambe. Masinde alikuwa kiongozi, mtu wa dini, mwanafalsafa na nabii aliyewakilisha sauti ya utaifa na uzalendo na kuingia katika historia ya Kenya kama shujaa mkubwa. C.W. Hobley (1929) anashadidia kuwa jamii ya Babukusu ilikuwa na mashujaa waliopigana kama 'wanaume'. Hobley ndiye aliongoza jeshi la mkoloni na kuwaangamiza Babukusu katika ngome - *Lukooba* ya Chetambe, mnamo mwaka 1895. Kwa Babukusu jina '*Hobilo*'[12] huashiria kifo, dhuluma na harufu ya utawala wa mkoloni.

Kutokana na ushahidi huu, Elijah Masinde ambaye awali alifanya kazi katika korti za Kiafrika, alielewa kuwa Kiswahili ndicho chombo pekee cha kuwaunganisha wazalendo ili kuondoa ukoloni. Vita alivyopigania vilipinga utawala wa Nabongo Mumia dhidi ya Babukusu. Mambo mawili muhimu yaliibuka :

[12] Mkorogano wa jina Hobley kama lilivyotamkwa na Babukusu

(i) Tamaa ya Nabongo Mumia kuwatawala Babukusu kwa kutumia Kiswahili

(ii) Tamaa ya Babukusu kujipatia uhuru kwa kutumia Kiswahili kama chombo cha umoja kati yao na jamii jirani.

Masinde kwa utanashati, uwezo wa kuvuta hadhira kwa ufasaha wake, upendo wake wa kandanda na cheche za kutaka waafrika wajikomboe, ulichochea fikira, matamanio na nguvu ya watu kuamini katika filosofia yake iliyowaleta pamoja na hivyo kuchangia katika maenezi ya lugha ya Kiswahili Ubukusuni.

## 4.2 Mahakama za Kiafrika

Utawala wa mkoloni ulishuhudia utumizi wa vifaa mbalimbali vya kutekelezea na kufanikisha sera zao za kikoloni. Mahakama za Kiafrika (African Court Tribunals) ni mojawapo ya asasi zilizofanikisha malengo ya mkoloni. Mpangilio wa Mahakama hizi ulifuata mkondo huu :

Afisa wa korti za Kiafrika (Mzungu)
↓
Rais wa korti (Mwafrika)
↓
Makamu wa Rais (Mwafrika)
↓
Wazee wa korti (Waafrika)
↓
Karani wa korti (Mwafrika)
↓
Askari wa korti.

Korti hizi za Kiafrika zilitekeleza majukumu yafuatayo :

- Kushughulikia maswala ya mashamba.
- Kuhusu kesi za kijamii, mfano ulipaji wa mahari.
- Kushughulikia kesi zilizohusiana na utamaduni wa Waafrika.
- Kuhusu kesi zingine kama wizi, mauaji na uhalifu mwingine kama ukiukaji wa sera za chifu.

Uteuzi wa Rais wa korti hizo ulifanywa na Mkuu wa Wilaya (D.C). Rais na makamu wake waliteuliwa katika misingi ifuatayo:

- Wengi walikuwa rika ya *Kananachi*[13] na *Kikwameti*[14] na kwa hivyo tajriba ilikuwa muhimu sana. Tajriba ilijikita katika ufahamu wa utamaduni wa jamii mahsusi na masuala ya jumla juu ya maisha.
- Walikuwa na kisomo kilichowawezesha kuendesha vikao vya mahakama. Mfano Mzee Naibei aliyezaliwa 1907, alisoma hadi darasa la tano katika shule ya Misheni ya Marafiki ya Kaptola.

[13] Kananachi ni vijana waliopashwa tohara kati ya miaka ya 1924 hadi 1934
[14] Kikwameti ni neno linaloashiria vijana waliopashwa tohara kati ya miaka ya 1912 hadi 1922



Samuel Naibei Kimkung, OBE, SS
1907 TO 28-08-05

- Uelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili na kwa kiasi fulani Kiingereza.
- Wengi, licha ya kutimiza haya, waliteuliwa kutegemea ukuruba wao na utawala wa kikoloni wa wakati huo. Nabongo Mumia aliwateua washirika wake wa karibu waliomsaidia katika kufanikisha sera ya mkoloni ya utawala. Kuteuliwa kwao ilikuwa kama zawadi kwa utiifu wao. Nyingi ya familia zilizokuwa na uhusiano wa karibu na Nabongo Mumia zilifaidi kwa kuteuliwa katika nafasi muhimu na watoto wa familia hizi kupata elimu. Baada ya uhuru, familia hizi zimekuwa na ushamishi mkubwa Ubukusuni.

Idadi ya wazee wa korti ilikuwa saba au nane katika korti moja. Kila chifu aliwakilishwa angalau na mzee mmoja. Isitoshe, kila jamii iliwakilishwa kwa mfano, wazee kutoka jamii za Babukusu, Wateso, Wasabaot na Bakhayo, kwani wao pia walisaidia kufafanua baadhi ya maswala ya kila jamii. Wao pia walitumia Kiswahili na lugha zao za kwanza. Karani wa korti sharti awe na

kiwango cha elimu kisichopungua KAPE, mweledi katika Kiswahili maana kilikuwa ndicho chombo cha mawasiliano kortini na kwa Kiingereza. Karani wa korti alihojiwa na D.C ambapo walipoajiriwa, Rais wa Korti, makamu wake na karani, walipitia mafunzo ya miezi miwili, huku wakitilia makali uzungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Utawala wa Nabongo Mumia ulitilia maanani elimu katika himaya yake. Machifu walihusika moja kwa moja katika ujenzi wa shule. Shule hizi ndizo zilizosaidia kuwekea Kiswahili msingi Ubukusuni. Kwa hivyo, uteuzi wa wafanyikazi wa mkoloni katika himaya hii ulitegemea ufahamu mzuri wa Kiswahili. Makarani wa Korti, askari wa Korti na wafanyikazi wengine mahakamani walistahili kutosheleza mahitaji haya ya uelewa wa Kiswahili.

Kiswahili ndiyo ilikuwa lugha iliyotumiwa mahakamani. Uamuzi ulitolewa katika Kiswahili. Karani aliandika uamuzi katika Kiswahili na Kiingereza. Karani wa korti alikuwa muhimu sana kwa sababu alishauri mahakama juu ya maswala ya kisheria. Uandishi wa uamuzi wa mahakama uliendelea kwa Kiswahili na Kiingereza hadi mwaka wa 1965 ambapo korti ziliwekwa chini ya hakimu ambaye aliandika uamuzi katika Kiingereza. Makarani wa korti wakabakia kama watafsiri na wakalimani tu, huku yote yaliyoendelea mahakamani yakiandikwa katika Kiingereza (Naibei H., 2008)[15].

Mahakama za Kiafrika zilikuwa chini ya Mahakama Kuu ya Rufani (African Courts of Appeal). Aghalabu mahakama hizi ziliendeshwa na Waafrika wasomi

[15] Mahojiano na Mzee Hesbon Naibei mwezi Aprili, 2008

kama Pascal Nabwana aliyekuwa Rais wa korti za Kiafrika za Rufani. Korti hizi zilishughulikia kesi zilizoshinda mahakama ndogo.

Shughuli za mahakama ziliendeshwa kwa Kiswahili. Ikiwa mshukiwa alikosa uelewa wa lugha hii, basi ilitafsiriwa kwake. Kwa sababu uajiri wa makarani wa korti ulitegemea usomi, walioajiriwa Ubukusuni wachache walitoka katika jamii jirani. Jeremiah Nyangule (Mmarama), kwa mfano, alikuwa karani huko Kabuchai. Uajiri wa maafisa kama hawa kutoka nje ya Ubukusu ulisaidia kutilia mizizi Kiswahili kwa sababu ililazimu watumie Kiswahili katika shughuli zote. Jamii kama za Bakhayo na Bamarama walitetea utawala wa Nabongo Mumia. Hii ndiyo sababu ya kuteuliwa kwa baadhi ya wanajamii kutoka jamii hizi. Uteuzi huu ulikuwa shukrani kwa usaidizi wao katika kuendeleza sera ya ukoloni. Kwa hivyo, walioteuliwa walikuwa vikaragosi wa Nabongo Mumia. Korti za Kiafrika zilikuwa na jukumu la kuendeleza utawala wa Nabongo Mumia na mshirika wake mkuu, mkoloni. Kiswahili kilipata hadhi hii hasa korti nyingi zilizopofunguliwa mfano wa korti hizi ni;

| **Korti** | **Rais** |
|---|---|
| Kabuchai | Muganda Namachanja |
| Amukura | Joseph Papa, baadaye, E. Osikuku. |
| Nambale | Eric Kokonya |
| (Kamtiong Kimilili) | Samwel Naibei. |

Pascal Nabwana alisimamia Mahakama ya Kiafrika ya Rufani huko Kabuchai. Baadhi ya Marais wa korti hizi walikuwa Philip Mwangale, Biketi na Shadrack Malo (Omuwanga) aliyesimamia korti ya Kakamega, huku Zechariah Indulah akisimamia Mahakama ya Kiafrika ya Rufani ya Tiriki (Wandati N. 2008)[16]. Kwa sababu ya umuhimu wa korti hizi katika kutekeleza majukumu ya utawala, mkoloni alifungua korti nyingi katika eneo la North Kavirondo. Baadhi ya korti hizi zilikuwa Lurambi, Khwisero, Nambale na Mumias. Kwa hivyo, utawala wa mkoloni akishirikiana na Nabongo Mumia ulichangia pakubwa kukita mizizi kwa Kiswahili kupitia korti hizi. Kiswahili kilipewa hadhi kuanzia afisa wa korti za Kiafrika, mzungu, ambaye alizungumza Kiswahili vizuri hadi kwa askari wa korti. Misingi ya kuwaajiri maafisa hawa wa korti kutegemea Kiswahili ilichangia pakubwa ukuaji wake kwa taratibu katika eneo la Ubukusu

.

### 4.3 Ndoa ya Mseto

Wakati huu wa ukoloni ulishuhudia kuingiliana kwa jamii za North Kavirondo sababu ya utawala wa Mumia. Kuingiliana kwa jamii hizi kwa sababu ya utawala, biashara na dini kulisababisha ndoa kati ya kabila mbalimbali. Ubukusu ilikuwa nchi ya rasilimali nyingi kwa sababu ya rotuba ya eneo hili. Kulingana na Wangala I. (2008)[17] ni wakati wa kipindi cha njaa (1940-1943) ambapo ililazimu jamii kama ya Maragoli 'kuwauza' wasichana wao katika nchi ya Ubukusu kwa gunia moja ya mahindi au wimbi . Kanisa la Marafiki ndilo lilipanga shughuli hii ambapo wasichana walipelekwa katika vituo maalum vilivyoitwa "Quaker Points"


---

[16] Mahojiano na Mzee Nandasaba Wandati, Aprili 2008
[17] Mahojiano na Mzee Isaac Wanjala, Aprili, 2008

kama Chwele, Chesamisi, Kamusinga, na Lugulu. Shughuli hii iliongozwa na wazee wa dini kama Daniel Amudavi (Mmaragoli aliyekuwa mwalimu wa dhehebu la Marafiki na wa shule, kule Kimilili) na Hezekiah Ngoya. Kipindi hiki kikasababisha ndoa baina ya jamii hizi mbili. Kiswahili kikapata nafasi ya kupanuka kwa sababu si rahisi Mbukusu kuelewana kitamshi na Mmaragoli. Kwa sababu viongozi wa dini ndio walikuwa wakiongoza shughuli hii, basi walikuwa wamewekea mizizi matumizi ya lugha ya Kiswahili. Viongozi wa dini walishirikiana na utawala wa Nabongo Mumia. Wasichana walioleta kutoka Maragoli, walipelekwa hadi 'Quaker Points'. Maeneo haya yalikuwa karibu na kampi za machifu ambao walitoa ulinzi. Vilevile, utawala wa Nabongo Mumia ulishirikiana na viongozi wa dini kwa sababu, waliunga mkono utawala wake. Madhehebu haya yaliteta utawala huu kwa kuanzisha shule mbalimbali na kwa hivyo, kuendeleza sera ya elimu. Dini na elimu ikachangia pakubwa swala la ndoa ya mseto kati ya jamii hizi zilizongiliana.

Kwa sababu ya maingiliano kidini kati ya Wakatoliki au Marafiki, wafuasi wa dini hizi walihimiza watoto wao kuoana bila ya kujali kabila. Mfano mzuri ni wa dini ya Marafiki ambapo watoto walioenda kusomea Kaimosi kutoka Ubukusuni wakati huo walioa wanawake kutoka jamii tofauti, mfano Chifu Timona Masinde wa Kimilili alioa msichana kutoka Maragoli kutika msingi ya kidini. Maingiliano hayo ya watoto wasomi wa wafuasi wa kwanza dini hizi kutoka Ubukusu yalichangia usomi wa uendelezaji wa lugha ya Kiswahili.

Utawala wa Nabongo Mumia ulichangia maenezi ya ukuaji wa Kiswahili katika msingi wa ndoa. Mumia kulingana na A. Wamukoya (mhj) (2008)[18] alitumia ujanja wakati Waswahili na Waarabu walipotaka kurudi kwao. Alinukuliwa akiwaambia 'MZURI MTAKWENDA TU.' Aliwachelewesha kurudi huku akiwaambia Abawanga kuwapa chakula cha bure na wasichana warembo. Muda si muda walijikuta wameoa wasichana hao, wamezaa nao na basi hawakurudi hadi leo. Mumia alikuwa na sababu za kibinafsi, hasa alijua umuhimu wa Waswahili kwa upande wa usalama. Watawala waliotumwa Ubukusuni kutawala, walishika wasichana Babukusu kwa nguvu na kuwafanya wake zao, hasa wasichana warembo.



*Nyanya Recho Nelima Wekhwela, mmoja wa waliohojiwa kutoka jamii ya Babukusu kuhusu swala la Marafiki. Arusi za wakati huo ziliitwa 'Siselelo'*

Utawala huu ulisisitiza matumizi mazuri ya Kiswahili. Wavulana Babukusu waliokuwa na uwezo wa kujieleza barazani mwa chifu, walipewa wasichana kutoka Wanga.

[18] Mahojiano na Mzee Ali Wamukoya mwezi Machi, 2008

Motisha hii ikachochea vijana wengi kujifunza Kiswahili ili kujipatia jiko. Baadhi ya askari wa Kinubi pia walioa Uluyiani na Ubukusu kama asemavyo Mzee Mnubi Jabir[19], mkazi wa mjini Bungoma. Msururu wote wa watawala chini ya Nabongo Mumia walijihusisha katika ndoa mseto, mfano:

- Mzee Samwel Naibei wa kijiji cha Chepkarai (Mlima Elgon) alioa Mteso, Mukhayo, Mbukusu, Muwanga na Wasabaot.
- Chifu Sudi Namuchanja alioa mtoto wa Mumia aliyeitwa Shiundu miongoni mwa wasichana wengine Wawanga.
- Nduguye Chifu Sudi, Mang'eni alioa msichana wa Mulama nduguye Mumia.
- Chifu Musa Amtallah alioa msichana wanne kutoka Wanga na Mnyala mmoja.
- Chifu Jonathan Barasa alioa Mtachoni.
- Chifu Nabutola alioa msichana kutoka jamii ya Abatura.
- Chifu Wamukoya alioa Mbukusu na Mganda.
- Chifu Manya alioa Mbukusu.
- Chifu Kerre alioa Mmaragoli.
- Chifu Timona Masinde wa Kimilili alioa Mmaragoli.

Kule Malakisi Wahindi wawili – Kiria na Musa - walioa wasichana wa Abawanga. Maingiliano yao na Abawanga na Babukusu hasa, kibiashara, yalichangia ndoa kama hizi, hadi vifo vya Wahindi hawa miaka sita iliyopita.

[19] Mahojiano na Mzee Jabir Aprili 2008, mkazi wa Mjini Bungoma

Maingiliano haya ya ndoa, hasa kwa watawala wa enzi hizo yalichangia pakubwa ustawi wa Kiswahili. Ni muhimu kukumbuka kuwa Kiswahili kilikuwa chombo cha utawala ambapo shughuli zote za utawala zilitumia lugha hii. Ndoa za mseto basi zilisaidia kuimarisha Kiswahili miongoni mwa jamii hizi mseto Ubukusuni.

## 4.4 Biashara Ubukusuni

Biashara katika kipindi cha kabla na kuingia kwa ukoloni vilichukua nafasi kuu katika kutilia mizizi ukuaji wa Kiswahili. Shughuli za biashara kutoka Pwani zilipanuka sana kuanzia mwaka wa 1832 katika himaya ya Sayyid Said, Mbaabu (1996:42). Msafara ilipenya barani kuanzia Mombasa na Malindi hadi kufikia Ziwa kuu la Nyanza. Katika eneo la North Kavirondo, Mumias ilipanuka kama mji ulioathiriwa na maingiliano kati ya wenyeji na wageni wa awali - Waarabu na Waswahili- kabla ya kuingia kwa mkoloni.

Waarabu na Waswahili walipiga kambi Mumias baada ya kukaribishwa vyema na Nabongo Shiundu na baadaye Nabongo Mumia. Elureko kama Mumias ilivyojulikana hapo awali, ikawa kitovu cha biashara katika eneo la magharibi mwa Kenya na misafara ielekeyayo Uganda. Waswahili na Waarabu wakisindikizwa na askari wa Nabongo Mumia - Wanubi, Wamaasai na Wasomali, walipenya Ubukusuni wakielekea hadI sehemu ya Mlima Elgon. Waswahili, Waarabu na Abawanga walitafuta pembe za ndovu, ngozi, watumwa na mifugo. Licha ya upinzani kutoka kwa baadhi ya koo za Babukusu, ukoo wa Bakhoone chini ya Namachanja wa Khisa ulihakikisha misafara hii ilikuwa salama. Ushahidi

simulizi waonyesha kuwa Wanyamwezi, Wayao, Wang'indo, Wasukuma, na Wazaramo walikuwa miongoni mwa makundi haya ya wafanyi biashara.

Kulingana na P. Wamukota (mhj) (2008)[20] makundi haya ya wafanyi biashara yaliingia katika boma za watu, lakini sababu walikosa kuwasiliana kimatamshi walianza kwa kuwazungumza kwa ishara. Baada ya muda Babukusu walianza kushika neno moja moja na kuanza kuzungumza Kiswahili, 'rongorongo'- (si fasaha). Ingawa kulikuwa na ugumu katika ujifunzaji, walianza kushika maneno hasa ya bidhaa zilizoletwa na Waswahili. Utumizi wa wakalimani wakati mwingine ukasaidia kurahisisha mawasiliano. Wageni hawa walileta viungo, tumbaku, sukari, chumvi, shanga, bunduki, vitambaa, na kaniki. Nabongo Mumia alipotawazwa kama chifu mkuu na kuweka mikakati mahsusi ya utawala alipanua masoko ya kufanyia biashara. Mumias ndiyo ilikuwa soko kuu. Masoko mengine yakafunguliwa Ubukusuni. Nayo ni: Watoya, Kimilili, Lugulu, Harambee, Chwele, Webuye, Malakisi, Kwa Dorofu, Kamukuywa na Myanga - Soko hizi zote zilipatikana North Bukusu na South Bukusu. Jambo la kutilia maanani ni kuwa soko hizi zote zilikuwa katika makao makuu ya chifu labda kwa sababu ya usalama. Biashara iliathiri lugha ya Kibukusu. Baadhi ya majina ya Kiswahili yalitoholewa moja kwa moja kwa Kibukusu ikiwa ni ishara kamili ya mwingiliano huo. Maneno kama *engubo, lilirinda, lishati, esukari, kamachani, lisasi, chumbe na matafali* (matafari) ni baadhi ya majina yaliyotumiwa katika lugha ya Kibukusu. Hii inaonyesha athari ya biashara na namna ilivyosaidia

---

[20] Mahojiano na Mzee Polisi Wamukota, Aprili, 2008

maendeleo ya Kiswahili. Utohozi hu unaonyesha kuwa Kiswahili kilikuwa na ushawishi mkubwa Ubukusuni.

Licha ya Waarabu na Waswahili, jamii zilizozunguka Babukusu ziliingiliana na jamii hii kibiashara. Jamii hizi zilikuwa Abawanga Wateso, Wasabaot (Ndorobo), Abanyala, Abatachoni na Abasamia. Eneo la Babukusu lilijaa vyakula, mifugo, na bidhaa kutoka kwa Ndorobo vilivyoitwa -'Bitasia na chinego' ambayo ni aina ya vikapu na teo, bidhaa ambazo Babukusu waliwauzia jamii jirani. P. Nabangi (Mhj) (2008) anasema kuwa ingawa Sudi Namachanja alikuwa chifu, lakini alipenda biashara sana, hasa ya mifugo. Alipeleka mifugo yake hadi Busia kuwatafutia soko. J. Nandeyoka (mhj) (2008), anasema kuwa nyingi ya masoko haya yalifunguliwa kati ya mwaka wa 1940 hadi 1947 na awali wafanyi biashara walikutana katika makao ya Chifu, hasa siku ya jumamosi.

Maingiliano haya yalikuwa na athari kubwa. Mazoea ya biashara kati ya jamii hizi mseto yalisababisha uenezaji wa lugha ya Kiswahili kwa sababu lugha hii iliunganisha kundi hili la watu lililokuwa na nia na maslahi mamoja-Biashara. Kiswahili kikawa lugha ya biashara barani. Isitoshe, katika eneo la miji, kukawa na mitaa iliyoitwa Mjini ambapo wanawake Waswahili na Waarabu walianzisha uokaji wa mahamri na uuzaji wa maziwa kwa wakazi wa miji.

Kule Malakisi Wahindi wa kwanza Musa na Kiria waliuza chumvi, viberiti, na kaniki katika maduka yao. A. Khatambi (mhj, 2008) anasema kuwa, kwanza

ilikua vigumu kuelewana, lakini baadhi ya wafuasi wa dini ya Kiislamu walijaribu kuelewana na Wahindi hawa polepole. Ninamnukuu;

**Mhindi**: Veve taka nini? (Wewe unataka nini?)
**Mbukusu:** Mpa hiyo! (Nipe hicho kitu!)

Malakisi iliibuka kuwa soko kuu ambapo Waarabu pia walipojenga makao yao. Waarabu wa kwanza walikuwa Mohammed, Sefu na Shaeri. Mohammed Hirsi na Yusuf Abdi ni baadhi ya Wasomali walioweka makao yao Malakisi kwa mujibu wa biashara. Mji huo basi ukawa mchanganyiko wa Babukusu, Wateso, Abawanga, na Wakhayo. Mseto huu wa watu ulichangia sana uenezi wa Kiswahili kutoka mji huu hadi viunga vyake. Biashara ilichukua nafasi muhimu sana katika kuchangia maenezi ya Kiswahili Ubukusuni. Mseto wa jamii hizi katika mji wa Malakisi uliwekana kwa sababu ya suala la utawala. Nabongo Mumia alituma watawala katika eneo hili kutoka jamii zilizotetea uongozi wake. Nabongo Mumia akiwa Mwislamu, aliwapa motisha wafanyi biashara wa Kihindi na Kiarabu ili kujenga makazi huko Malakisi. Mchanganyiko huu ulikipatia Kiswahili mihimili mikubwa ya kuenea Ubukusuni.

## 4.5 Nafasi ya Dini za Kiislamu na Kikristo

Dini ilichukua nafasi kubwa sana katika himaya ya Nabongo Mumia. Katika sehemu hii, tutachunguza nafasi ya dini ya Kiislamu na za Kikristo,hasa Wakatoliki na dhehebu la Marafiki katika kuchangia maenezi ya lugha ya Kiswahili.

### 4.5.1 Wamishenari wa Kikristo

Mumias ilipokea Wazungu wa kwanza hasa wamishenari, watalii na wafanyi biashara miaka ya 1880. Huu ni wakati Joseph Thompson na J. Martin, Bishop Tucker, Dr Carl Peters, Fredrick Lugard na Bishop Hannington waliingia Mumias. Joseph Thompson alipita nchi ya Ubukusuni akiandamana na Waarabu na Waswahili ambao tayari walikuwa wamejenga uhusiano katika eneo hili. Bishop Hannington naye aliingia Ubukusuni akiandamana na askari wa Mumia waliohakikisha usalama wake. Kufikia mwaka wa 1902, Wamishenari wa Marafiki (Friends Church) walikuwa wamejenga makazi yao huko Kaimosi.

Misheni ya Marafiki wa Kiafrika (Friends African Mission) iliingia Ubukusuni kufikia mwaka wa 1913 na kuweka makazi hapo Lugulu. Wamishenari wa kwanza walikuwa J. W. Ford na Dkt. A. B. Astock. Miongoni mwa walimu wa dini wa kwanza wa Kimaragoli huko Lugulu, walikuwa ni Daniel Amudavi ambaye baadaye alihamishwa na kuchukua nafasi ya Yakobo Andede ambaye alimtangulia huko Kimilili F.A.M. Juhudi za Mishenari ya Marafiki zilionekana katika kuanzishwa kwa shule, hospitali na kanisa. Kufikia mwaka wa 1930, North Bukusu ilikuwa na shule hamsini na wanafunzi elfu moja na mia nane. Kila shule iliambatanishwa na kanisa, lugha iliyotumiwa katika shughuli za kufunzia dini kanisani hasa ilikuwa Kimaragoli na Kibukusu. J. Nandeyoka (mhj, 2008) anasema Wamishenari hawakupendelea kutumia Kiswahili kwa sababu kilihusishwa na dini ya Kiislamu. Shuleni, Kiwanga na Kimaragoli, zilipewa nafasi kuu. Mtawala naye alisisitiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli zake

na kwa hivyo baada ya muda Kiswahili kilipata nafasi katika mafunzo shuleni na basi kupenyeza hadi makanisani. Baadaye lugha ya Kiswahili ilipata mashiko. Wakati ulifika ambapo ingawa waliimba kwa Kiwanga na Kimaragoli kanisani, lakini baadhi ya nyimbo zilitungwa kwa Kiswahili mfano:-

> Jesu Msalaba wangu
> Sasa nimejitwika
> Ni kwandame bwana wangu
> Wengine nawaepuka

Nandeyeko anasema kuwa nyimbo za Kiswahili zilikuwa na hadhi na mahadhi mazuri zaidi kuliko za Kiwanga. Wanafunzi wakaanza kuzipendelea na basi kuchangia matumizi ya Kiswahili na baada ya muda kupata umaarufu.

Wakatoliki walijenga mizizi kule Mumias, lakini kufikia mwaka wa 1925 hadi 1935 walikuwa na ushawishi mkubwa katika South Bukusu. Kanisa la Kibabii lilijengwa 1931, na baadaye kuingia North Bukusu ambapo Misheni ya Misikhu ilifunguliwa 1940 na baadaye kupanuka kuelekea Kiminini, Kitale (Mitume Centre) hadi Tartar (Wolf 1977:114). Kufikia mwaka wa 1932, wafuasi wa Kikatoliki walifikia idadi ya elfu mbili lakini kufikia mwaka wa 1945, walikuwa elfu kumi na moja. Kando ya kanisa, walijenga shule na hospitali.

Wakatoliki walihimiza matumizi ya Kiwanga na Kilatini. Kilatini, kilitahiniwa katika kiwango cha "C.S.E". Lugha za Kiwanga na Kilatini zilichukua nafasi kuu kanisani kuliko Kibukusu na Kiswahili katika makao ya kwanza huko Kibabii chini ya Mmishenari Paulard mwaka wa 1931. Hata hivyo, walimu hawa kutoka Mumias hawakuwa na la ziada baadaye, kwani walilazimika kutumia Kiswahili.

Hii ilitokana na sababu kuwa wengi hawakuelewa Kibukusu vizuri na kwa vile Kiswahili kilikuwa kinafunzwa shuleni, basi kikapata nafasi katika kanisa. Ubatizo katika dini hii hupitia hatua nyingi kuanzia kusoma sala, ukatekismu, kusoma amri za Mungu na baadaye ubatizo. Kupitia hatua hizi kulisaidia Kiswahili kwa kiasi fulani maana kilikuwa kinatumiwa katika hatua hizi zote licha ya matumizi ya lugha za Kilatini na Kiwanga. Baadhi ya wafuasi wa Kikatoliki Ubukusuni, walikuwa Pascal Nabwana, Nicholas Maruti, Remi Lutilo, na Anjelimo Makhanu. Baadaye wahubiri na maaskofu walianza kupata mafunzo yao katika vyuo vya kidini na maingiliano kama hayo yalichangia Kiswahili kupata nafasi. Wanafunzi wa dini kutoka jamii mbalimbali walipokutana katika vyuo hivi waliwasiliana katika Kiswahili na baadaye kufikia miaka ya 1950-1960, Kiswahili kilipata nafasi katika mahubiri (Pst. P. Kibuli 2008)[21].

Madhehebu mengine kama ya Kiangilikana na Jeshi la Wokovu yalitia mizizi katika maeneo ya Butonge na Kolanya ingawa hayakuwa na ushawishi mkubwa sana. Madhehebu haya yote yalifanya kazi yao katika himaya ya Nabongo Mumia. Nabongo Mumia alikaribisha madhehebu yote bila kubagua. Hii ni kwa sababu makundi haya ya kidini hayakupinga sera za mkoloni na mshirika wake, Nabongo Mumia. Uhusiano huu mzuri na utawala ulisaidia maingiliano ya uongozi wa kidini, utawala na jamii ya Babukusu. Uhusiano huu ukasaidia maenezi ya Kiswahili Ubukusuni.

[21] Mahojiano na Pastor, P. Kibuli wa Kanisa la Marafiki, Mei 2008.

### 4.5.2 Uislamu

Dini ya Kiislamu ilipata nguvu yake kule Mumias chini ya uongozi wa Sheriff Hassan Abdallah ambaye alisaidiwa na nduguye Sheriff Omar Bin Abdallah. Wawili hawa walianzisha mikakati ya pole pole ya kuwasilimisha Abawanga huko Kwa-Shiundu, 1903. Kipindi hiki kilishuhudia dini hii ikichukua nafasi kubwa katika himaya ya Nabongo Mumia. Abawanga walipendelea mavazi ya Kiislamu. Wengine wakaolewa na Waarabu na Waswahili. Mpango huu alianzisha Nabongo Mumia mwenyewe. Kwa mfano, Mswahili Khamisi alioa dadake Mumia, Wamakobe. Sheriff Omar alimuoa Masakhwe msichana wa Kalelwa kutoka Eshisumo karibu na Shianda. Ndoa kama hizi zilichangia kusilimishwa kwa Abawanga na basi kuanza kustahi njia za kistaarabu za Waislamu- Mavazi, Vyakula na lugha - (Kenyanchui, 1992:35, Abdalla, 1971:23, Wamukoya, 2008)[22].

'Mabalozi' wote waliotumwa kutawala nje ya Abawanga walisilimu kwanza kwa mfano Murunga aliitwa Suleiman na Mulama akapewa jina la Omar. Watawala hawa wote walistahi njia zote za Uislamu, ikiwemo lugha. Suleiman Murunga ndiye alitumwa Ubukusuni kutawala. Vituo vyote alivyopitia kabla ya kutulia hapo Kimilili vilipata athari kuu ya Uislamu kuanzia Machakusi, Malakisi, Bukokholo, Chwele na baadaye makao yake makuu Kimilili.

---

[22] Mahojiano na Mzee A. Wamukoya, Aprili, 2008

Kule Malakisi walimu wa dini walikuwa Omar Mashaka (*Omutanganyika*) na Omar Ngoro kulingana na Mzee A. Khatambi (2008)[23]. Wazee waliokuwa wa kwanza kusilimu walikuwa Ibrahim Wangulu na Murunga wa Matili.

Miji ya Bungoma, Malakisi na Kimilili ndiyo ilipata athari kuu ya dini hii ya Kiislamu. Sudi Namachanja aliyekuwa Chifu wa South Bukusu, aliomwomba msomi wa dini hii Sheriff Omar kuweka mizizi ya dini hii katika himaya yake. Sheriff Omar akamtuma mwalimu wa dini Mzee Bakari Mkumba (Mtanganyika) ambaye alifuatiwa na Mzee Sagana, Kisero na Ali Majesh. Wao ndio walijenga Uislamu katika mji wa Bungoma.

Suleiman Murunga, na baadaye Musa Amutallah, walichangia ukuaji wa dini hii kule Kimilili. Kufikia mwaka wa 1940, baadhi ya waliosilimu walikuwa jamii ya karibu ya watawala, marafiki wao, wafanyikazi, hasa wale waliotangulia kufanya kazi Mumias na hasa wale waliotamani kuoa wasichana kutoka kwa jamii ya Abawanga. Kumwoa msichana wa jamii hii kulikuhitaji usilimu kwanza na uwe mzungumzaji mzuri wa Kiswahili. Wandabwa Syuma, Kerre, Musa Amutallah, Athman Waswa, Hassan Sakari na Salim Mbule ni kati tu ya wazee wa kwanza waliokumbatia Uislamu wakati huo. Mwarabu Ali Abdul aliyefungua biashara yake Kimilili katika miaka ya 1920, ni mmoja wa wale waliosaidia dini hii kupanuka (A. Pwoka (2008)[24]. Waumini wa dini hii wakiri kuwa ingawa Kiarabu kilitumiwa katika Madrassa, lakini Kiswahili ndicho kilitumiwa

---

[23] Mahojiano na Mzee Khatambi Khasolo, A. Aprili, 2008
[24] Mahojiano na Mzee Pwoka Amtallah, Mei, 2008

kupambanua Kurani tukufu. Mafunzo ya dini hii pia yalirahisishwa, hasa wakati ambapo Kurani ilitafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Abdalla Saleh Al-farsy (The Islamic Foundation, 1984).

Maingiliano ya ndoa na biashara hati ya jamii zilizotawaliwa katika kipindi hiki yalichangia ukuaji wa dini hii. Kwa mfano Sura Al Bagarah (2) Mstari 221 wa Kurani tukufu unasema kuwa msichana wa Kiislamu hawezi kuoa Kaffir. Hiyo ni amri. Aliyeolewa au kuoa lazima asilimishwe ndiyo iwe ndoa takatifu. Ukuaji wa wafuasi wa dini hii ulichangia pakubwa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mafunzo ya watoto wa Kiislamu yalianza wakiwa na umri kati ya miaka sita hadi kumi na tano ambapo 'Maalim' aliketi chini ya mti akiwa na korani na kiboko huku watoto wameketi kwenye nusu duara.

Mafunzo ya kurani yalianza kwa kuimba na kukariri sura fupi fupi za korani. Watoto walifurahia kuimba hata wakiwa nyumbani. Korani imegawiwa katika sehemu sitini au "Esus", kila sehemu na sura zake.

Hatua ya pili ilihusu alfabeti za Kiarabu zilizo na hati ishirini na sita. Hatua iliyofuata ilikuwa ni uundaji wa silabi kwa kutumia irabu. Kuandika na kusoma Kurani kulifuatia baada ya watoto kufahamu hatua hizo za awali. Mtoto aliyefaulu alijiunga na shule ya 'ilm' – mafunzo ya kiwango cha juu kama Bakari Juma, (2008)[25] anavyosema.

---

[25] Mahojiano na Mzee Bakari Juma, Mei, 2008

Kwa hivyo hatua kama hizi zilimsaidia mtoto kuelewa dini yake, hasa Kiswahili kilipotumiwa kupambanua Kurani tukufu iliyoandikwa katika Kiarabu. Hivyo dini ya Kiislamu ilijenga misingi thabiti katika maeneo ya Bukusu na kuchangia maenezi ya Kiswahili katika eneo la Ubukusuni. Uhuru wa kuabudu uliotekelezwa na utawala wa Nabongo Mumia ulichangia maenezi ya lugha ya Kiswahili.

**4.6. Reli**

Mkoloni aliweka mikakati ya utawala wake, hasa kwa kupanua miundo - mbinu. Reli na barabara vilipanuliwa. Mumias, mwaka wa 1895 ilitambuliwa kama kituo cha utawala cha mkoloni. Hivyo basi mkoloni aliweka miundo - mbinu ili kukidhi mahitaji ya watawala hawa. Katika kipindi hiki reli ilikuwa imeelekea Port Florence (Kisumu) na kisha baadaye kujengwa kuelekea Butere hadi Mumias. Barabara ya Sclater ilikuwa inapanuliwa kuelekea Mumias kutoka Fort Maxsted (Kakamega) mwaka wa 1895.

Kufikia mwaka wa 1925 hadi 1928 reli iliingia nchi ya Kitosh, yaani Ubukusu kuelekea Uganda. Babukusu walilazimishwa kujenga reli. Jamii zingine zilizohusishwa katika ujenzi ni: Abawanga, Wajaluo na Wakhayo. Wajenzi wakuu walikuwa Wazungu na Wahindi walioitwa "Indian Coolies".

Lazima ya kujenga reli kwa jamii ya Babukusu iliwalazimu kutumia Kiswahili kwa sababu ya mseto wa wajenzi waliotoka jamii mbalimbali. Katika historia ya

Babukusu baadhi ya watoto waliozaliwa wakati huo waliitwa MAJENGO kutokana na ujenzi wa reli. 'Majengo' hutokana na kitenzi kujenga na kwa hivyo ni ishara kamili kuwa wajenzi wa reli hasa Babukusu walikuwa na lazima ya kukitumia Kiswahili. Baada ya kumalizika kwa ujenzi wa reli, muundo msingi huu, ulikuwa kitovu cha biashara na usafirishaji wa watu na bidhaa. Mchanganyiko wa watu- wafanyi biashara na wasafiri- waliosafiri kutoka maeneo mengine nchini ulileta maingiliano ya watu hawa na Babukusu basi kuisaidia kueneza kiswahili kama chombo cha mawasiliano. Reli pia ikafungua sehemu za mashambani kwa mfano Sudi Station na Myanga Station, stesheni ambazo zilifunguliwa biashara na Duka wallahs- wale wahindi waliokuwa wakijenga reli - Biashara mashambani ikachangia maingiliano ya wakazi hawa na waekezaji wa rasilmali katika sehemu hizi basi kupanua matumizi ya lugha ya Kiswahili. Baadhi ya Babukusu waliajiriwa kama wapakiaji au wapakuaji mizigo kwenye stesheni hizi. Walitangamana na wasafiri wengi ambapo lugha ya mawasiliano ilikuwa Kiswahili. Upanuzi wa miundo misingi huendeleza maeneo ya mashambani na kuchangia maingiliano ya watu mseto na kwa kufanya hivyo kujenga uhusiano unaoendelezwa kwa kutumia chombo cha mawasiliano –lugha ya Kiswahili (J. Nabutola, 2008[26], P. Nabangi, 2008)[27]. Muundo – msingi huu ulidhamiria kurahisisha usafiri na upanuzi wa maeneo ya bara. Upanuzi wa eneo la Ubukusu ulisaidia katika kurahisisha utawala wa Mumia na mshirika wake mkoloni. Watawala walisafirishwa barani ili kuhakikisha usalama unadumishwa ili kuwezesha asasi kama dini na biashara kuendeshwa bila wasiwasi. Nabongo

[26] Mahojiano na Mzee Nabutola, J. Muganda, Aprili, 2008
[27] Mahojiano na Mzee Peter Nabangi, Aprili, 2008

Mumia alihakikisha waekezaji hawa salama chini ya mwavuli wa utawala. Maingiliano haya ya watu kutoka sehemu mbalimbali ulifanikishwa kwa sababu ya reli. Lugha ya Kiswahili basi ikapata nafasi ya kuenea Ubukusuni.

## 4.7 Ajira

Ajira katika serikali ya mkoloni ilitegemea mambo kadhaa. Ajira iliyohusiana na utawala hasa Chifu, manaibu wao, na askari ilitegemea mambo mawili muhimu - uhusiano na jamii tawala na kujieleza vyema katika Kiswahili. Ushahidi simulizi unadai kuwa, Babukusu walilazimishwa kutumia Kiswahili na pili, Babukusu hawakulazimishwa kuzungumza lugha ya Kiswahili. Labda dai la kwanza ni kweli hasa kutokana na shuruti kuwa watoto wapelekwe shuleni na uhudhuriaji wa lazima wa vikao vya machifu. Ikiwa uajiri ulitegemea uelewaji na matumizi bora ya Kiswahili, basi inaweza kuwa kweli kuwa baadhi ya wanajamii- Babukusu – walilazimika kujifunza Kiswahili bila shuruti. Kiswahili kiliendesha shughuli zote za utawala wa mkoloni na basi yeyote aliye kuwa na mshawasha wa kuajiriwa hakuwa na budi bali kujifunza lugha hiyo. Webi J. (mhj) 2008[28], anasema kuwa baadhi ya watawala wa kwanza walijifunza Kiswahili wakiwa kazini na atoa mifano ya Machifu, Makhaso, Jeremiah Kukubo, na Jonathan Barasa. Anaongeza kuwa kote Ubukusuni (North Kitosh na South Kitosh), watawala walikuwa na ufahamu wa Kiswahili na atoa mifano ifuatayo ya *'Lukongo'*:

[28] Mahojiano na Mzee Jestimore Webi, Aprili, 2008.

| Lukongo | Eneo la Utawala |
|---|---|
| Omar Cheloti | Bokoli |
| Jesse Bisuche | Webuye |
| Namisi Murumba | Ndivisi |
| Petro Makali | Chwele |
| Yona Mukile | Kamukuywa |
| Mayeku Muganda | Kimilili |
| Stefano Wekunda | Malakisi |
| Tendet Kipteek | Elgon |

Askari wa Machifu, Lukongo, na wa kortini aghalabu walichaguliwa na Machifu. Ingawa wengi walikuwa wa jamii zao lakini walisisitiza stadi bora za mawasiliano ili kutekeleza majukumu yao.

Maafisa wa serikali kulingana na R. Manya (2008)[29], walipewa mafunzo maalum ya miaka miwili. Maafisa wa elimu, Kilimo, Afya, Ushirika, barabara walipata mafunzo maalum katika serikali ya mkoloni. Wao walikuwa washika dau muhimu katika baraza la Chifu yeyote yule. Kazi yao muhimu ilikuwa ni kuendeleza sera za serikali katika kila sekta. Ingawa walikuwa wasomi wazuri wa Kiingereza lakini walitumia Kiswahili katika kutekeleza majukumu yao. Walipowatembelea umma katika maboma yao, walijaribu kuwasiliana katika Kiswahili ili kufanikisha malengo yao.

[29] Mahojiano na Mzee Richard Manya, Aprili, 2008

Wazungu walijifunza Kiswahili na hata kupasi mtihani na basi ilikuwa changamoto kubwa sana kwa Babukusu. J. Nandeyoka (2008)[30], akumbuka mkaguzi wa shule Bwana Tellor aliyekuwa mtumizi mzuri sana wa Kiswahili alipokuwa anakagua shule mbalimbali. Alikuwa kichocheo kwa Nandeyoka ambaye alihakikisha kuwa anajifunza kukimudu Kiswahili kama Bwana Tellor. Baadhi ya Babukusu waliofanya kazi za hadhi kwa kupitia kwa mafunzo maalum ni kama:

- Jestimore Webi - afisa wa ushirika aliyepata mafunzo yake, K. I. A, huko Kabete 1946-1948 awali alishiriki vita vya pili.
- Nandeyoka J. Amudavi – 'Financial Manager' aliyepata mafunzo yake huko Jeans School, Kabete katika somo la biashara na uhasibu, 1948-1950. Alishiriki hapo awali katika vita vya pili.
- Philip Sambu, mwalimu aliyepata mafunzo yake Kaimosi.

Mifano hii inaashiria kuwa uajiri wa afisa wa serikali ulihitaji mafanisi mema katika mitihani na mafunzo maalumu katika taaluma mahsusi. Maingiliano ya wafanyikazi hawa na raia wakiwafunza hali ngeni ya maisha katika kila sekta kulichangia upenyezaji wa lugha ya Kiswahili Ubukusuni.

### 4.8. Michezo

Michezo ilikuwa kiungo muhimu sana katika utawala wa Nabongo Mumia. Kila lokesheni iliwakilishwa na timu hasa kandanda miongoni mwa michezo mingine.

---

[30] Mahojiano na Mzee Jamini Nandeyoka, Aprili, 2008

Chifu wa kila lokesheni ndiye alikuwa mfadhili huku Nabongo Mumia akiwa mfadhili mkuu. Baadhi ya michezo ilikuwa kuvuta kamba, kandanda, riadha. Timu hizi zilishindana hadi kiwango cha Afrika Mashariki. Kimilili, kulingana na Naibei H. (mhj. 2008)[31], ilikuwa timu bora zaidi katika kuvuta kamba, eneo la North Kavirondo, huku Elgon ikishinda katika riadha.

Eneo la North Kavirondo lilishindania kombe la "Ndege chai of North Kavirondo". Kila lokesheni ilishiriki kombe hili ambapo timu za kandanda zilizokuwa nzuri zilikuwa za North Bukusu, Bunyore na Malakisi F.C (South Bukusu). Malakisi F.C ikiongozwa na Opicho Munialo waliwashinda Bunyore F.C mabao 5-2 katika mwaka wa 1957. Timu ya kandanda iliyosifika sana ilikuwa ya Kimilili Simba, Elijah Masinde akiwa nahodha, huku wakufunzi walikuwa Daniel Amudavi na Festus Machasio chini ya ufadhili wa chifu Musa Amutallah, aliyekuwa mfadhili wa timu hiyo. Kwa sababu ya ufundi wa Elijah Masinde katika kandanda aliitwa 'Skurubu', istilahi iliyoswahilishwa. Neno hili latokana na neno la Kiingereza 'Screw'. Mikwaju yake Masinde iliwatatiza walinda lango labda ndiyo sababu akapewa jina hilo. Timu hii ilicheza na 'Idakho Locational Team', 1941 na kabla ya hapo alishiriki katika kombe la "All Star Kenya Gossage Cup Team" kuanzia mwaka wa 1930-1938. Timu ya Kimilili Simba hii ilijenga wachezaji wengine kama Phares Mangoli, Rusell Mulongo, Elam Nabangi, Jotham Cheloti. Maingiliano ya wachezaji hawa na wenzao kutoka timu za nje ziliwasaidia kutangamana na basi kuthamini masomo na hadi sasa uzao wao wote ulisoma. Kwa hivyo, maingiliano ya timu hizi za lokesheni

[31] Mahojiano na Mzee Naibei Hesborn, Aprili, 2008

kote North Kavirondo hadi kushiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki kulikuwa na athari yake. Lugha iliyotumiwa na wachezaji ilikuwa Kiswahili na basi kupata misingi iliyobora. Nabongo Mumia alipokuwa akihudhuria baadhi ya michezo hii alitoa hotuba yake katika lugha ya Kiswahili hasa katika kiwango cha mkoa na wilaya. Mwelekeo huu ulipelekea Kiswahili kupata nafasi Ubukusuni hasa timu kama za Bunyore, Tiriki, na Idakho zilipowatembelea na hata wao pia kucheza nje ya Ubukusu. Michezo basi ilichukua nafasi kuu katika kuchangia maenezi ya lugha ya Kiswahili katika eneo la Ubukusu

## 4.9 Muziki

Utungaji wa muziki wakati huu ulitungwa katika lugha za kwanza. Baada ya muda baadhi ya wanamuziki walianza kutunga kwa lugha ya Kiswahili. Mwanamuziki wa kwanza Ubukusuni aliitwa Bwana Masinde Nalobile aliyetunga miaka ya 1940-1950. Wengine kutoka eneo la magharibi mwa Kenya walikuwa John Mwale, Wijenje, Nzenze na hata Daudi Kabaka, Jacob Luseno na Jesse Sabwami na Fundi Kondo kutoka Pwani.

Baadhi ya wahojiwa kama Jamin Nandeyoka, Jestimore Webi na Henry Cheloti wakumbuka baadhi ya nyimbo zilizoimbwa na wanamuziki hawa kama ifuatavyo:

Fundi Konde

*Jambo , jambo sigara x 2*
*Sigara baridi*

John Mwale

*Jumbe nipeleke kwetu*
*Jumbe nimelewa sana*
*Sina pa kulala*
*Jumbe nipeleke kwetu x 2*

Ubukusuni bendi ya 'Misikhu Bayinda Ochestra Club' ndiyo ilitukuka na walitunga nyimbo zao katika lugha ya Kibukusu na Kiswahili. Wimbo wao mmoja wa Kiswahili ulikuwa ni:

*Nililala chali ,nikaota ndoto*
*Mji wa Mombasa*
*Unawaka moto x2*

Mwaka wa 1946, mwanamuziki Mbukusu, Jesse Sabwani, alitunga wimbo kwa Kiswahili.

Jane na Peter walipendana
Ross na Jeff walipendana
Zimebaki siku chache
Watachukuana

Kisha akiongezea Kibukusu :

Sipurupuru na simwemwe x 3
Omukhasi mulala kumtambo

(Vipepeo na vimuli muli x 3
Mwanamke mmoja ni umaskini)

Kando na hawa bendi zingine nchini zilizoimba kwa Kiswahili zilichipuka mfano Tamnyole na Kipanga, Kiko Kids (1946). Kiko Kids ndio walitumbuiza wanajeshi baada ya vita vya pili, hasa baada ya kushinda vita. Nyimbo hizo ziliimbwa na wanajeshi Waafrika hata baada ya kurudi nyumbani, mfano:

1. Hurrah x 2 Saimanga
   tutarudi nyumbani kwetu
   tutaoa bibi
2. Taliano mjinga x 2
   Bwana mkubwa kupiga fire x 2
   taliano mjinga.
   Japani mjinga x 2
   Bwana mkubwa kapiga fire x 2
   Japani mjinga

Mpangilio wa nyimbo hizi ulikuwa mzuri usiotatiza kuimbwa. Walioshuhudia waliwasifia watunzi hawa na kufanya utunzi katika Kiswahili kupendwa na wengi, kupelekea watu wengi kuenzi kutumia lugha ya Kiswahili. Watunzi hawa walisifu utawala wa Nabongo Mumia na vikaragosi wake. Hii iliwawezesha kutunga nyimbo bila hofu yoyote. Walikuwa wakialikwa katika baraza ya Chifu na ya Mkuu wa Wilaya. Kitendo hiki kikawafanya kupata safa hasa walipotunga kwa Kiswahili.

**4.10 Usetla**

Kufikia Novemba 29, 1912, Masetla walikuwa wamechukua mashamba ambayo ni Bungoma ya sasa, Lugari, Mlima Elgon na Uasin Gishu kuanzia mto Kamukuywa hadi makutano ya mito Kibisi na Nzoia kuelekea mto Kipkarren au Sosiani, karibu na Mlima Marabusi (KNA/PC/NZA/3/7/2/2 1912-1913 Report on Eastern boundary, North Kavirondo Reserve). Ni muhimu kuelewa kuwa, kufikia mwaka wa 1910, mkuu wa wilaya ya North Kavirondo, Geoffrey Archer, alikuwa amebuni maeneo manane ya utawala ambayo yalikuwa:

- Butsotso
- Kabras
- Marama
- North Kitosh
- South Kitosh
- Nabakholo
- Samia
- Wanga.

Kwa hivyo utawala huu ulihitaji wafanyikazi wa lazima. Chifu Suleiman Murunga wa North Kitosh aliwalazimisha Babukusu na hata Wabok, Bongomek na Kony kufanya kazi ya lazima kama ujenzi wa Barabara au wabeba mizigo. Kuepuka dhuluma hizi, Babukusu na jamii zingine zilitorokea kwa mashamba ya Masetla ili kutafuta kazi. Sababu nyingine ya kutoroka ilikuwa ni kuepuka kuandikishwa kwa lazima katika jeshi ili kushiriki katika Vita vya Pili vya Dunia. Kwa hivyo walipata afueni katika mashamba haya na hata wengine walitorokea Misheni ya Kikristo ili kuhepa ilipaji ushuru wa nyumba au wa kibinafsi.

Babukusu waliogopa kuandikishwa katika jeshi kama 'Carrier Corps' -'Kariakor'- au 'Pioneer Corps-' Panyako. Mkuu wa majeshi wa eneo hili John Ainsworth aliwasajili Wanajeshi zaidi ya 162,000 kati ya 1917-1918 ambapo wanajeshi 24,000 waliuawa vitani (Wafula 2000). Kwa hivyo mashamba ya Masetla yalipata wafanyikazi wengi waliotoroka dhuluma ya utawala wa mkoloni akishirikiana na Mumia. Wafanyakazi walitoka katika jamii mbalimbali wakiwemo Babukusu, Wateso, Wanandi, Wamaasai, Bamasaaba (kutoka Uganda), Waturkana na Wakaramoja.

Wafanyikazi hawa waliajiriwa kama washika kamba[32], washika jembe[33], kazi za nyumbani (Udobi, Toto jikoni), kulima, na kukamua ng'ombe. Wengine walikubali kuwa maskwota ambao walikubali kufanyia masetla, huku wakipewa kipande cha shamba ili kupata chakula chao wenyewe. Walifanya kazi kwa miezi mitatu hadi sita kwa mwaka, huku wakilipwa shilingi nne na kipimo cha posho. Wanawake wa Kizungu waliwalipa wafanyakazi wa nyumbani ilhali Mabwana waliwalipa wale wa mashambani (J. Webi, 2008).

Baadhi ya masetla wanaojulikana Ubukusuni ni "Tobasi na shamba lake la Namanjalala, Mittford MacGowan Barberton, Jecksen, Bwana Mfupi, miongoni mwa wengine. Kujumuika kwa wafanyikazi kutoka jamii mbalimbali tofauti kulikuwa na athari kubwa. Kuna wale walioajiriwa wasiojua Kiswahili, waliofahamu kidogo na wale waliokuwa wazungumzji wazuri. Ushahidi simulizi unashadidia kuwa hawa masetla walitumia Kiswahili vizuri sana katika shughuli zao. Mzee Johnstone Khisa alipohojiwa Oktoba 2006 anakiri kuwa alipoajiriwa kama mshika kamba hakuelewa Kiswahili vizuri. Aliajiriwa kati ya mwaka wa 1923 Februari hadi Oktoba 1924. Alijifunza Kiswahili hadi kumfurahisha bwana mkubwa ambaye aliimpa pesa ili arudi shuleni. Katika mwaka wa 1931 Johnstone Khisa alihitimu kama mwalimu. Masetla walipoingia katika koloni ya Kenya, walijifunza Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano na wafanyikazi wao na watawala wa Kiafrika. Mkoloni alikuwa amewekea msingi sera ya elimu na kwa

[32] Washika kamba ni wale wafanyikazi walioongoza fahali wa kulima kwa kuwaelekeza kwa kutumia kama walikuwa mbele ya fahali hao kumi na sita au zaidi.
[33] Washika jembe ni kama dereva walioshika lile jembe kubwa za kulimia. Jembe hili lilivutwa na fahali zaidi ya kumi na sita.

hivyo, Kiswahili kilikuwa somo mojawapo. Ushahidi wa Johnstone Khisa ni ishara kamili. Nabongo Mumia alihakikisha machifu wanatekeleza majukumu yao ili kuharakisha sera zote za utawala. Mseto wa wafanyikazi hawa katika mashamba ya masetla uliwasaidia kuwasiliana kwa sababu ya uelewa wao wa lugha ya Kiswahili. Machifu walidhihirisha utiifu na uaminifu wao kwa kuhakikisha kuwa masetla walikuwa na wafanyikazi wa kutosha. Machifu walikuwa ishara ya utawala wa mamlaka. Hii ndiyo sababu serikali ya mkoloni iliwalipa rupia thelathini kwa mwaka. Johstone Khisa anakumbuka jinsi alivyokuwa akilipwa shilingi kumi kwa mwezi katika juhudi zake za kufunza Wazungu Kiswahili kati ya mwaka 1936 hadi 1956.

Kwa sababu ya mseto wa wafanyikazi mashambani mwa masetla mlitoa nafasi mzuri ya wao kuzungumza Kiswahili kwa lengo la mawasiliano ilitokea. Ikiwa mshika kamba ni Mbukusu na mshika jembe (dereva) ni Mnandi ilibidi wao kutumia Kiswahili, kwani wasetla wenyewe walitumia Kiswahili. Hii ilikuwa changamoto kubwa kwa hawa wafanyi kazi. Kando na Mzee Johnstone Khisa, Maruti khwa Nasioko, Khatambi Khasolo, Jesse Khwituta Kusimba Khwa Manyololi, miongoni mwa wengine walifanya kazi mashambani. Ingawa hawakupata elimu kama ya sasa, wazee hao walikimudu Kiswahili barabara. Mzee Khatambi (2008) anakiri kuwa uzoevu wa matumizi ya Kiswahili ulichangia pakubwa kuelewa lugha hiyo na hivyo kuifanya kuenea.

### 4.11 Vita vya Kwanza na vya Pili

Vita vya kwanza na vya pili vilishuhudia usajili wa vijana wenye nguvu katika jeshi la mkoloni. Kamanda wa jeshi wa eneo la Kavirondo John Ainsworth alisajili takriban wanajeshi 162,000 wakati wa 1917 na 1918. Waliosajiliwa waliunda jeshi la Afrika Mashariki. Waliosajiliwa katika jeshi walikuwa mchanganyiko wa waliosoma na wenye kisomo cha chini. Jeshi lilikuwa na idara ya elimu ambayo baada ya kusajiliwa, wanajeshi walipata mafunzo. Wale waliopasi mtihani wa Kiingereza walivalia sare ya alama – E. Kiswahili nacho kilikuwa lugha ya taifa ya wanajeshi wa Waingereza, Afrika Mashariki. Afrika ya Kati walitumia Kiingerza huku Afrika Magharibi wakitumia Kinyasa (Nandeyoka, 2008)[34].

Kabla ya wanajeshi waafrika kuondoka kwenda Malaysia, Indonesia na kwingineko, walipewa keki na Meya wa Nairobi, Bw. Alexander iliyokuwa na maandishi haya: 'Kwenda na urudi salama'. Hii ilikuwa ishara kamili kuwa wanajeshi wote walihamasishwa kukielewa Kiswahili barabara. Wanajeshi walitoka katika nchi ya Nyasaland, Nothern Rhodesia, Tanganyika, Uganda, Kenya, Sudan, Somalia miongoni mwa nchi tofauti. Matumizi ya Kiswahili yaliwaunganisha pamoja kama jamii ya Mwafrika.

Wakiwa safarini, bendi ya wanajeshi iliimba wimbo wao maarufu ulioitwa, 'funga safari'. Hii ilikuwa ishara kamili kuwa, ufahamu wao wa lugha ya Kiswahili haukuwa na shuku hata kidogo. Kule vitani wanajeshi wa kizungu waliwapa

[34] Mahojiano na Mzee Jamini Nandeyoka, Aprili, 2008.

wanajeshi hawa Waafrika jina la 'Nyama ya risasi'. Ingawa wahojiwa wanasema kuwa risasi haikumbagua Mwafrika au Mzungu. Wengi wa wanajeshi walirudi salama, walikuwa na ufahamu mkubwa katika Kiingereza, Kiswahili na masuala ya utawala.

Nafasi iliyopewa lugha ya Kiswahili katika jeshi la Afrika Mashariki iliinua hadhi ya lugha hii. Ushahidi simulizi unaonyesha kuwa wanajeshi kutoka Kenya, Uganda, Tanzania, Somalia na Wanubi waliwasiliana kwa lugha hii . Shughuli zote ziliendeshwa kwa Kiswahili. Wanajeshi wa Afrika Mashariki walipata mafunzo yao ya hatua ya kwanza huko Maseno - Maseno Army Recruitment Deport. Hapa baada ya kuandaliwa mtihani na idara ya elimu,waliwagawa katika sehemu kutegemea kiwango cha elimu. Wale waliokuwa na elimu nzuri walifunzwa kozi kama utabibu, katika shule ya matibabu ya Afrika Mashariki – East African Medical Corps and Establishment, Nairobi- na baadaye kupata mazoezi katika hospitali ya Kabete. Kisha baadaye walipelekwa kambi la wanajeshi huko Langata kwa miezi mitatu.

Kwa hivyo umoja wa jeshi hili ulitokana na kuwa na lugha ya kuwaunganisha. Wanajeshi hawa hasa wa Afrika Mashariki walisafiri hadi India, Madagascar, Egypt Ethiopia, Ceylon, Burma, Tokyo, China, na Somalia. Ingawa walisafiri huko kote lakini waliunganishwa na lugha ya Kiswahili. Wale walioajiriwa wakiwa na uelewa mchache wa Kiswahili baada ya muda huu wote walianza kuwa weledi katika kutumia Kiswahili

Hiyo ndiyo sababu baada ya Vita walijitungia nyimbo za Kiswahili wakisherehekea ushindi wa Jeshi lao na kwamba sasa watarudi nyumbani ili kuoa wanawake wazae watoto.

Baadhi ya wazee waliohojiwa na ambao walishiriki katika vita hivi waliporudi nyumbani walijiunga na chuo cha Kabete wakijifunza taaluma mbalimbali ili kutoa huduma kwa umma. Jestimore Webi aliacha ualimu na kujiunga na jeshi na baada ya vita alichukua kozi huko Kabete na kufuzu kama Afisa wa ushirika. Alihudumia Babukusu kwa muda na baadaye ,1959, alitawazwa kuwa chifu wa Kimilili. Nandeyoka Jamin alijiunga na jeshi punde tu baada ya mtihani wake wa K.A.P.E. Akiwa jeshini, alishughulikia utabibu na akumbuka mwalimu wake Dkt. Piaji aliyemfunza namna ya kushughulikia wanajeshi waliojeruhiwa. Aliporudi nyumbani Januari 1946, alijiunga na Jeans school, Kabete kuchukua mafunzo ya uhasibu ambapo baadaye aliajiriwa kama mhasibu katika chama cha wakulima cha Kuywa. Mifano hii miwili inaashiria umuhimu wa elimu katika jeshi. Huduma ya hawa wanajeshi baadaye kwa umma katika nafasi mbalimbali serikalini ilisaidia katika kukiimarisha Kiswahili hasa walipoingiliana kutekeleza majukumu yao. Jestimore Webi, Isaiah Polisi Wamukota, Nicasio Tengeye, Jamin Nandeyoka Amudavi, Mzee Satia Burmastar, ni baadhi ya wazee Babukusu walio hai hadi sasa. Ushahidi wao ulitolewa katika Kiswahili sanifu, ishara kuwa Kiswahili kilipewa hadhi kuu katika kipindi hiki cha ukoloni, jeshini.

## 4.13 Mijini

Katika kipindi cha ukoloni mitaa iliibuka hasa katika mji wa Bungoma, Malakisi na Mumias. Mitaa hii iliitwa Mjini. Jabir Salim, (mhj. 2008) anasema kuwa mjini ni jumla ya watu wa Uislamu wanaokaa pamoja. Kulikuwa na Msikiti na basi kuwafanya wao kujitenga na jamii zingine labda kwa sababu ya wao kuwaona kama makafiri. Kundi hili lilihusisha Wanubi, Wasomalia, Waarabu na Waswahili. Juma Bakari (2008) atoa mwelekeo tofauti. Anasema kuwa Mjini ulihusisha wale wasiokuwa na mashamba. Walihusika na biashara ya kuuza vitumbua na wenyeji wakawaita "Waungwana wasiofanya kazi yoyote". Bakari anakubaliana na Jabir kuwa, walikuwa watu wa imani moja, kundi moja walioishi kwa undugu wa dini ya Uislamu.

Mitaa hii ilichangia maenezi ya lugha ya Kiswahili kwa njia moja au nyingine. Miji ya Bungoma, Malakisi na Kimilili ilipata kundi hili lililoshiriki dini ya Uislamu, na biashara katika miji hiyo mahsusi. Maingiliano na wenyeji-Babukusu- muda baada ya muda yalichangia ukuaji wa lugha katika miji hii na baadaye mashambani.

## 4.14 Elimu

Malengo ya elimu katika enzi ya mkoloni yalilenga kutayarisha kundi la Waafrika ambalo litaendeleza sera za kikoloni. Utawala wa mkoloni ulishirikiana na Wamishenari katika kujenga misingi ya Elimu. Makamishena wa kwanza Charles Eliot na Hayes Sadler waliunda halmashauri ya Wamishenari kuhusu elimu, 1908,

kando na tume ya Fraser ya Elimu, 1909, ili kujenga mikakati ya kuendeleza elimu. Walipendekeza kwanza elimu ya viwandani na pili Maadili mema kupitia dini miongoni mwa Waafrika. Kufikia mwaka wa 1922, kupitia sera ya serikali kuhusu elimu, shule zote za misheni zilizotoa elimu bora, zilipata msaada wa kifedha. Tume ya Phelps –Stokes, 1924, iliunga mkono msaada huu wa kifedha na kusisitiza kufunzwa kwa lugha za Kiafrika, Kiswahili kikiwa mojawapo.

Awali, 1909, kongamano la umoja wa Wamishenari kuhusu sera ya lugha katika elimu lilikubali kuwa Kiswahili kifunzwe kuanzia darasa la tatu nacho Kiingereza kifunzwe kuanzia darasa la nne. Ilikubaliwa pia kuwa Kiswahili kiingizwe katika mtalaa. Ingawa Wamishenari wengine walipinga pendekezo hili huku wakitetea lugha za kienyeji, changamoto kubwa ilikuwa, hawakuwa na pesa za tafsiri, wataalamu wa kutafsiri na hawakuwa na walimu waliofuzu ili kufunza lugha hizi za Kiafrika. Kufikia miaka ya hamsini, matumaini ya kuandika lugha za kienyeji yalikuwa yamedidimia na kwa hivyo watawala walijihusisha na swala la kutumia lugha inayoeleweka na kila mtu kwa mujibu wa kujenga utaifa na elimu- Kiswahili ilikuwa ndiyo lugha ya sifa hizi.

Uluyiani ilikuwa vigumu kusanifisha lugha mojawapo ya eneo hili ambazo ni kumi na sita. Ingawa kamati ya orthographia, 1942, iliteua lahaja nne- Lumarama, Luwanga, Lushitsa na Lutsotso ili kutumiwa, lakini kulikuwa na tofauti ya lafudhi hizi. Kwa mfano kulikuwa na Leksia ambazo zina muundo

tofauti wa lafudhi hizi. Kwa mfano kulikuwa na leksia ambazo zina muundo tofauti lakini humaanisha kitu kimoja, mfano:-

| **Babukusu** | **Maragoli** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| Likhese | Likondi | Kondoo |
| Ekhafu | Ing'ombe | Ng'ombe |

Baadhi ya leksia hutoa maana mbili tofauti kutegemea Jamii mahsusi, kwa mfano;

Khulaama - Kulaani (Babukusu)
- Kuomba (Kabras)

Ushahidi huu wa isimu mchangamano (Multilinguism) ulitatiza mapendekezo ya kutumia lugha za kwanza na basi kusisitiza matumizi ya Kiswahili. Ushahidi simulizi unaonyesha kuwa wanafunzi waliingia darasa la A na B. Madarasa yaliitwa Kamasomo ke chingubo - masomo ya nguo - ambapo herufi na hati ziliandikwa kwenye kitambaa kikubwa na kuangikwa ukutani. Shule zingine zilitumia Vibao vidogo vidogo (slate) vya kipimo cha nchi 9 kwa 12. Aliyesoma hati hizo aliingizwa darasa la kwanza. Kwa sababu shule hizi zilisimamiwa na Wamishenari, (Wakatoliki na Marafiki), shule za marafiki zilitumia Luloogoli na wakatoliki nao walitumia Luwanga (Nandeyoka J, (2008) na Webi J. (2008). Baadhi ya shule za kwanza zilizofunguliwa wakati huu Ubukusuni zilikuwa Kaptama, Kaptola, Kimilili F.A.M, Chesamisi, Kamusinga, Kuywa, Kibabii, Misikhu, Netima, Butonge. Shule hizi zilitahini mtihani wa C.E.E na K.A.P.E.

Masomo ya Kiswahili wakati huu yalishika kasi katika darasa la tatu ambapo kutokana na ushahidi simulizi vitabu vifuatavyo vya hadith vilifunzwa; *Safari za*

*Juma Japan, Hekaya za Abunwasi* na *Kitabu cha Essopo.* Wanafunzi walitungia kitabu cha Essopo wimbo mfupi kulingana na Mzee H. Cheloti (2008)[35]:

Essopo alikuwa Myunani
Essopo aliishi miaka mia tano
Essopo alikuwa na Kibyongo

Athari ya dini pia iliwapelekea kutunga nyimbo za kidini mfano:-

**Wimbo wa 1**

Bwana wangu alisema na Abram,
Akamwambia Abram
Akachukue mwanawe, Abram.
Nifanyie sadaka Abram

**Wimbo wa 2**

Tazameni yuapaa mwenye kushinda vita
Gari lake ni mawingu

(Nandeyoka Jamini, (2008)[36]

Nyimbo hizi zilitilia mshawasha wa kutaka kusoma zaidi Kiswahili hasa kwa watoto waliofurahia kucheza huku wakiimba. M. Tumbu (2008)[37] anakubali kuwa ilikuwa vigumu kuelewa Kiswahili, lakini walimu walijaribu kwa kutumia sentensi fupi fupi ili waelewe taratibu. Mfano:

| **Mwalimu** | **Mwanafunzi** |
| --- | --- |
| Sema, wewe | Wewe |
| Sema, huyu | Huyu |
| Wewe nani? | Wewe Nani? |
| Mimi huyu | Na wewe huyo. |

---

[35] Mahojiano na Mzee Henry Cheloti, Machi, 2008
[36] Mahojiano na Mzee Jamini Nandeyoka, Aprili, 2008
[37] Mahojiano na Mzee Masinde Tumbu, Aprili, 2008

Mifano mifupi kama hii ilichangia wao kuanza kutumia Kiswahili. Walimu wengine walitumia Kiswahili kueleza baadhi ya masomo mengine kwa mfano katika hesabati-walimu walitumia maneno kama Hesabu ya kuondoa (M. Tumbu, 2008).

Silabasi ya Kiswahili ilitahini yafuatayo;- Sarufi, Imla, Insha, Matamushi, Vitendawili, Ufahamu, Methali. Ushairi ndio ulipuuzwa. Wangala I, (2008)[38] akumbuka alipokuwa akisoma kitabu kama "Nakupenda lakini..." Magazeti ya Baraza na Mwananchi,' huku wakiunda sentensi darasani. Kiswahili kilipata nafasi zaidi katika kiwango cha shule za 'Intermediate' kwa sababu shule hizi zilichukua wanafunzi kutoka kila sehemu na kuwafanya watangamane basi kusaidia kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili. Ingawa Luwanga na Luloogoli zilitahiniwa lakini Kiswahili pia kilitahiniwa katika kiwango cha C.E.E, K.A.P.E hadi C.S.E. Hii iliwezekana hasa eneo hili lilipopata walimu waliofuzu katika Kiswahili kutoka chuo cha Kabaa.

Kwa hivyo misingi hii ya utawala wa mkoloni na Mmishanari kupanua elimu ilisaidia kujenga misingi ya Kiswahili. Utawala ulihakikisha kuwa watoto wanaenda shuleni kwa lazima. Wazazi waliokiuka amri hii waliadhibiwa vikali. Daniel Amudavi mwalimu wa kwanza Kimilili F.A.M alifungua DC[39] (Mabweni) mbili ya wasichana na wavulana katika boma lake. Kanisa la Marafiki lilisimamia watoto hawa ambao Wazazi wao walikataa kuwapeleka shuleni.

---

[38] Mahojiano na Mzee Isaac Wangala, April, 2008

[39] DC ni kifupisha cha neon linalosimamia mabweni yaliyojengwa na Kanisa la Marafiki.

Chifu Amtallah alisaidia sana juhudi za kanisa hili ili kuhakikisha kuwa watoto wanaelimika kwa hivyo katika misingi hii ya elimu na kisha baadaye maingiliano kanisani, michezoni, biasharani, ilichangia sana kueneza Kiswahili katika eneo hili la Ubukusu.

**Hitimisho**

Sehemu hii imezungumzia mchango wa asasi mbalimbali katika kueneza lugha ya Kiswahili katika eneo la Ubukusu. Jambo linalodhihirika ni tangamano kuhusu swala hili la lugha. Asasi hizi zilitegemeana kwa njia moja au nyingine ingawa asasi ya utawala ndiyo inayojitokeza kama mwavuli wa asasi nyingine. Utawala ulilenga kutafuta wafanyikazi ambao wangeweza kutimiza malengo yao. Asasi hizi zote zilifikia malengo yaliyokusudiwa kwa sababu ya heri njema kutoka kwenye utawala huu. Asasi zilitagusana katika mazingira mazuri yaliyowezeshwa na Nabongo Mumia. Kwa hivyo, mtagusano wa asasi hizi na kisha katika kutimiza malengo yaliyodhamiriwa chini ya mwavuli wa utawala wa Nabongo Mumia, lugha ya Kiswahili ilipata nafasi ya kuenea Ubukusuni.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa ripoti kuhusu utafiti huu kwa jumla, pamoja na kutoa muhtasari wa utafiti. Sura hii inalenga kuonyesha matokeo, mchango na baadhi ya changamoto zilizokabiliwa na mtafiti. Hatimaye, mtafiti ataonyesha mapendekezo zaidi kuhusu utafiti mwingine unaoweza kufanywa kwenye mada hii.

## 5.1 Muhtasari

Utafiti huu umeainisha, kueleza na kuchanganua mikakati iliyotumiwa na utawala wa Nabongo Mumia katika uenezaji wa lugha ya Kiswahili Ubukusuni, mkoani Magharibi mwa Kenya. Isitoshe utafiti huu ulichunguza asasi nyingine (kando na utawala) zilizochangia kueneza kwa lugha ya Kiswahili katika eneo hili.

Nadharia mbili, Nadharia ya utegemezi na Nadharia ya lugha kama mfanyiko wa kijamii, zimetumiwa. Mihimili ya nadharia hizi iliongoza utafiti huu. Utafiti ulijikita nyanjani na maktabani. Utafiti wa mahali ulihusisha maeneo ya Mumias, Matungu, Bungoma, Malakisi na Kimilili ambapo sampuli ya Wajibu au wahojiwa iliteuliwa. Kundi hili lilihusisha wazee wenye tajriba kubwa katika utawala, dini, biashara na maisha kwa jumla - kutoka jamii hizi mbili za Babukusu na Abawanga. Pia, baadhi ya wazee hawa walishiriki katika utawala

wa Nabongo Mumia. Mahojiano na hojaji ni mbinu mbili muhimu zilizotumiwa. Utafiti ulichunguza, vigezo muhimu - utawala , dini, biashara, usetla, vita vya dunia miongoni mwa asasi nyingine – vilivyochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili Ubukusuni. Katika hali hizi zote, utawala wa Nabongo Mumia ulikuwa na athari kubwa.

Kazi hii imepangwa katika sura tano. Sura ya kwanza inajumuisha utangulizi, swala la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia, mbinu ya utafiti na uchanganuzi wa data.

Katika sura ya pili, historia ya Ababukusu na Waswahili imeshughulikiwa. Historia ilihusu uelewa wa ukuaji wa jamii hizi mbili, maingiliano yao na wageni hasa Waswahili na Waarabu kisha Wakoloni, huku athari ya maingiliano hayo zikichunguzwa.

Sura ya Tatu imeshughulikia dhima ya utawala wa Nabongo Mumia katika uenezaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti umeainisha mikakati ya utawala wa Nabongo Mumia, maeneo aliyoyatawala na athari ya utawala huo kwa watawaliwa. Katika kuchunguza haya, utafiti umebainisha kazi ya utawala wa Nabongo Mumia katika kusaidia kueneza lugha ya Kiswahili Ubukusuni.

Katika sura ya nne asasi kama dini, mahakama, biashara, elimu miongoni mwa zingine zimechanganuliwa. Uchanganuzi unahusu maendeleo ya asasi hizi wakati wa ukoloni na namna ambayo maendeleo haya yalichangia uenezaji wa lugha ya Kiswahili Ubukusuni. Sura hii imebainisha nafasi muhimu ya asasi hizi katika maenezi ya lugha ya Kiswahili. Sura ya tano ni muhtasari, matokeo na mapendekezo kwa utafiti zaidi.

## 5.2 Matatizo

Matatizo kadhaa yaliukabili utafiti huu. Tafsiri ya kazi za Kiingereza ilikuwa kazi ngumu sana. Ili kupata maana na dhana mbalimbali mtafiti alilazimika kusoma kazi za Kiingereza, hasa vitabu vya historia kisha kutafsiri ujumbe uliokusudiwa.

Shida ya pili ilikuwa juu ya maelezo ya nadharia. Ilikuwa vigumu kupata nadharia zinazoafiki matakwa ya utafiti huu. Nadharia mbili zilizotumiwa na mtafiti zimeandikwa katika vitabu vya Kiingereza- Nadharia ya utegemezi na nadharia ya lugha kama mfanyiko wa kijamii. Tafsiri ya dhana hizi na ujumbe uliokusudiwa ili kukidhi malengo ya utafiti huu ilitatiza.

Wataalamu wachache wameshughulikia masuala ya uenezaji wa lugha barani na basi tahakiki ni chache mno. Mtafiti alilazimika kukimbilia kitengo cha Historia ili kushadidia utafiti huu.

Wahojiwa wengine walitoa ujumbe au maelezo yanayokinzana, hasa kuhusu masuala ya historia ya jamii ya Babukusu na Abawanga. Ilitaka uchanganuzi wa pande zote mbili ili kufikia uamuzi mzuri. Ingawa utafiti ulikumbwa na changamoto hizi zote, mtafiti alijitahidi kufanya uchunguzi kamilifu na wa kutegemewa.

## 5.3 Matokeo na Mchango

Utafiti huu ulinuia kuchunguza mikakati aliyotumia Nabongo Mumia katika utawala wake katika kueneza Kiswahili Ubukusuni. Uchambuzi uliofanywa unadhihirisha kuwa utawala ulichangia nafasi kubwa sana katika kueneza Kiswahili. Lugha ya Kiswahili iliweka misingi ya utawala. Kiswahili kama lugha zingine zilizotumiwa na watawala kilinasibishwa na silaha. Nguvu hizi zilidhihirika kupitia ushawishi na hata shuruti kwa jamii husika - Babukusu - kwa mujibu wa kutekeleza majukumu ya utawala, huku lugha ya Kibukusu ikipoteza hadhi. Kwa kufanya hivyo, utawala huo ulipanua jamii ya wazungumzaji lugha, hasa katika kutumia lugha kama chombo cha ustaarabu huku Babukusu wakiunga mkono utamaduni wa kigeni. Babukusu basi walikuwa wategemezi maana utawala ulikipa Kiswahili ushawishi mkubwa ikawa kwamba aliyekumbatia lugha hii alihakikishiwa kazi katika utawala wa mkoloni, ustaarabu na maisha bora hasa kupata elimu, vyakula, na kupanda ngazi kitabaka. Kwa hivyo watumizi wa lugha hii waliitegemea kama nyenzo muhimu ya uzalishaji wa mali na kupanda kiuchumi mradi wakubali sera za utawala wa Nabongo Mumia chini ya uongozi

wa Mkoloni. Kwa hivyo utawala ulichangia kukuza Kiswahili kama lugha ya utawala huku lugha za kienyeji zilikosa nafasi ya kukua.

Mumias ilipokua kama mji wa biashara na utawala, Kiswahili kikapata nafasi ya kuchipuka kutoka kitovu hiki hadi maeneo yaliyotawaliwa, hasa Ubukusuni. Babukusu mwanzo walikataa kutawaliwa, lakini ziliwanyamazisha. Mwanzo Babukusu waliteta na hata kukinai sera hizi, lakini baadaye walipogundua umuhimu wa kukumbatia Kiswahili katika utawala huu, walivumilia, wakajifunza lugha hii na baadaye wakajitegemea kutokana na faida zilizoambatana na matumizi yake.

Uchunguzi huu pia umebainisha kuwa lugha ni watu, ni maingiliano ya watu na lugha ni watu katika mawasiliano au majibizano. Mifanyiko ya kijamii hurahisishwa kwa sababu ya lugha. Utafiti huu umebaini jinsi Kiswahili kama lugha ni watu, ni maingiliano na basi ni watu katika mawasiliano. Mifanyiko ya kijamii huwezeshwa kupitia lugha. Utafiti huu umebainisha kuwa asasi kama ndoa, dini, biashara, korti za Kiafrika, elimu, muziki, michezo na miundo misingi zilifanikiwa Ubukusuni kwa sababu ya lugha ya Kiswahili. Kwa kiasi kikubwa, asasi hizi zilifanikishwa na utawala wa Nabongo Mumia.

Asasi hizi zilitoa mchango mkubwa na basi kusababisha mifanyiko ya kijamii iliyopelekea kusaidia kueneza Kiswahili. Maingiliano huchangia mfanyiko wa mtu binafsi ambapo mtu binafsi hujifunza lugha ya Kiswahili na kumfaidi yeye

mwenyewe kama ilivyobainika katika utawala wa Nabongo Mumia. Mfanyiko mwingine ni zaidi ya mtu mmoja. Babukusu waliingiliana kwa njia nyingi mfano biashara. Kwa sababu wamepitia mfanyiko wa mtu binafsi, hufanikisha mfanyiko wa mawasiliano. Makundi mawili yanapowasiliana basi utafiti huu ulibainisha kuwa mifanyiko ya elimu, maendeleo na utamaduni inadhihirika wazi. Jamii hii kwa sababu ya lugha ,sekta ya elimu ilichangia upanuzi wa maendeleo, mfano, miundo msingi. Jamii hii pia ilistaarabika hasa kwa kuiga utamaduni wa Waswahili na Wakoloni kwa sababu ya maingiliano na basi kusababisha mifanyiko ya kijamii. Lugha ya Kiswahili, ilichukua hadhi kuu sana katika himaya hii kwa sababu aliyejifunza lugha alitazamwa kama kiumbe kipya ambapo lugha ilimwezesha kujieleza na kujitosheleza. Ni muhimu kusema kuwa mihimili ya nadharia tulizotumia ilituongoza vyema katika kufanikisha utafiti wetu.

### 5.2 Mapendekezo

Utafiti huu ulichunguza dhima ya utawala wa Nabongo Mumia katika maenezi ya Kiswahili Ubukusuni katika misingi ya Kihistoria. Utafiti huu unapendekeza kuwa kando na asisi hizi, swala la Wamishenari katika kuendeleza elimu lilikuwa la muhimu sana. Swala hili lapaswa kuchunguzwa kwa kina zaidi maana ni asisi mojawapo ambayo ilichangia maendeleo ya elimu na hasa lugha ya Kiswahili Ubukusuni.

Suala la chimbuko na kuhamia kwa jamii ya Babukusu ni muhimu kiakademia. Kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa kuhusu jamii hii, itahitaji mchango wa taaluma tofauti tofauti. Taaluma kama akiolojia, isimu, historia zitajenga msingi bora wa kuweza kuelewa historia ya jamii hii. Kwa sababu ya ukubalifu wa Esibakala kama mahala pa asili ya jamii ya Babukusu na wanahistoria na ushahidi simulizi, itakuwa changamoto kwa wasomi ili kujaribu kufikia mtazamo unaokubalika kuhusu asili ya jamii hii, uhamiaji wao na kisha hadi kufikia maeneo yao ya sasa. Kwa msomi wa lugha ya Kiswahili, itakuwa bora kutafitia swala la isimu kwa sababu jamii hii ya Babukusu ilitagusana na makabila mengi wakiwa safarini. Athari ya uwingilugha ilijitokeza na kwa hivyo, utafiti katika mkondo huu ni muhimu.

Itakuwa muhimu pia kwa wanaakademia kuchunguza asili ya Abawanga na watawala wao. Utafiti mahsusi unaweza kuthibitisha msimamo wa ushahidi huu tiliokusanya. Utafiti ujikite katika asili yao kuhama kupitia Cameroon, Ethiopia, Uganda hadi Kenya huko Tiriki, kabla ya kuzaliwa na kutambulika kwa jamii ya Abawanga. Isitoshe, ithibati juu ya uhusiano wao wa karibu na Baganda yastahili kuchunguzwa na kufafanuliwa. Ushahidi wa kihistoria pia utatuwezesha kupata ufahamu kuhusu ukweli wa watawala ishirini na vipindi vya utawala, hasa ithibati kuhusu miaka ilivyoainishwa katika vipindi hivyo mahsusi. Kwetu wasomi wa Kiswahili, itakuwa vizuri kuchunguza uhusiano kiisimu na jamii ya Baganda ili kuthibitisha ukuruba waliokuwa nao hapo awali.

Utafiti huu pia unapendekeza kuwa ujirani wa Ubukusu - Mlima Elgon, unaokaliwa na Wasabaot hadi sasa una tatizo kubwa katika kujieleza kwa Kiswahili. Maeneo yanayopakana na Babukusu ndiyo yanayoonyesha ishara ya uelewa wa lugha ya Kiswahili. Maeneo ya ndani ya mlima huu yamefungiwa sana nje ya ulimwengu mwingine. Utafiti unapaswa kufanywa ili kutafuta ni nini hasa inayopelekea eneo hili kubaki nyuma katika matumizi ya Kiswahili. Utafiti huu unapaswa kujikita katika misingi ya kihistoria.

Kuna maeneo ambayo yalikuwa na uhusiano mzuri na Mumia. Utafiti unapaswa kuchunguza maeneo haya ili kuelewa ikiwa fimbo ya utawala ilichangia maenezi ya Kiswahili kama Ubukusuni au kulikuwa na sababu tofauti. Miongoni mwa maeneo haya ni kama vile Bakhayo, Banyala na Maragoli. Uelewa wa namna maeneo hayo yalivyopokea Kiswahili ni hatua kubwa katika misingi ya historia kubaini jinsi lugha hii ilivyoenea barani. Licha ya mapendekezo haya, utafiti huu umeonyesha kwa mafanikio dhima ya utawala wa Nabongo Mumia katika maenezo ya lugha ya Kiswahili Ubukusuni, mkoani Magharibi, Kenya.

## MAREJELEO


Abdulaziz, M.H, (1982): *Patterns of Language Acquistion and Use in Kenya in International Journal of Sociology of Language*

Ake, C. (1981): *A Political Economy of Africa,* New York, Longman

Amin, S. (1974): *Accumulation on Word Scale; Acritique of the Theory of Underdevelopment,* Enland: The harvester Press.

Angongo, RM & Hancock, 1F *(1980) "English in Africa" Emerging Standard of Diverging Regionalism?"* English worldwide 1PP (67-96)

Aseka, E.M (1989): A Political Economy of Buluyia 1900-1964. Ph. D Thesis. Kenyatta University

Boachen, A.A. (1981): *Colonial Era: Conquest and Colonialism in Africa (1870-1960),* London, Cambridge University Press

Bode, F.C (1984): *"Anti-colonial Politics within a Tribe. The case of the Abaluhyia of Western Kenya"* in Ojuke and Ochieng. W. (eds), Politics and Leadership in Africa, NRB: KLB

_________ (1978): Leadership and Politics among the Abaluyia of Kenya, 1894-1963, Ph.D. Thesis, Yale University.

_________ (1972): Reactions too the Imposition of Colonial Rule Among the Abaluyia C 1894-1920 Seminar Paper, History Dept, University of Nairobi

Bogonko, S.N (1992): *A history of Modern Education in Kenya* (1895-1991)

Chikati, J.M. (1988): "The Biography of Chief Musa Namutala (1930-1973)". B.A. Dissertation University of Nairobi

De Wolf J.L. (1971): Religious Innovation and Social Change among the Bukusu". Ph. D. Dissertation University of London.

__________*(1971)*: "Politics and Religion among the Bukusu." Universities Social Services Council Conference

Dealing, J.R. (1974):"Politics in Wanga Kenya C 1650 to 1914'' Ph.D Dissertion, North Western University

De Silvia, S. B. D *(1982): The Political Economy of Underdevelopmen, London,* Routebdge and Kegan Paul

Furaha, J. H. (1991): Matumizi ya lugha mjini Malindi: Jinsi Mielekeo Inavyoathiri Uteuzi wa Lugha. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Gordon, D.C (1978): *The French Language and National Identity (1920-1975). Contributions to the Sociology of Language:* No. 2: The Haque, Mouton

Gorman, T.P (*1970*) (ed): *Language in Eduaction in Eastern African.* NRB O.U.P.

Hudson, R.A (1980): *Soiololinguistics,* Cambridge University Press

Kachru, BB, (1986a): *The Alchemy of English: the Spread, Functions and Model of Non-Native Englishes,* Oxford, Pergamon Press

_________ (1986c): "*The Power and Politics of English''* in World Englishes, Vol. 5 No. 2/3: PP 121-140.

________ (1987): "The Spread of English and Sacred Linguistic *Cows". In Gurt, Language Spread and Language Policy Issues, Implications and Case Studies;* Washington DC: Georgetown University Press: PP 207-228.

Kakai, P.W. (1997): The Northen Luhyia Anti-Colonial Resistance: The Lumboka Chetambe War, ''Unpublished Paper, Kenyatta University.

Kay, S. (1973): "The Southern Abaluhyia, The Friends African Mission and the Development of Education in Western Kenya, 1902 – 1965", Ph.D *Thesis,* University of Wisconsion

Kenyanchui S.S.S. (1992*)*: *Nabongo Mumia*, NRB, Heinemann.

Kusimba, C. M. (1999): The Rise and Fall of Swahili States, Walnut Greek, Alta Miva Press.

Lonsdale, J.M (1970):*Political Association in Western Kenya: In Robert 1 and Mazrui (eds). Protest and Power in Black Africa N.Y. O.U.P*

Makila, F.E (1980): *An outline History of the Babukusu.* NRB: *Kenya Institute Bureau*

Massamba D.P.M (1987*): "The Impact of Politics on Language Development in Tanzania''.* In Kiswahili, Vol. 54/2, 180-191

__________ *(1992): "Thirty years of Swahili Development in Tanzania"* Shuriya Hino (Ed). African Urban Studies II, Institute For The Study Of Languages And Culture Of Asia And Africa (IlCAA)

Mazrui Ali (1973): *"The English Language and the Origin of African Nationalism''. In the Varieties of Present Day English* edited by Richard W.B. and S.C. Robinson pp56-70. NY. Macmillan. Co.

_________*(1980): "Beyond Dependency in the Black World: Five strategies for Decolonization"* In Aquisiton Y.Y. (Ed) Decolonization and dependency: Problems of Development of African Societies. Westport, Connecticut, greenwood Press, PP 84-97

Mbaabu I. (1978a*): Kiswahili, Lugha ya Taifa,* Nairobi, KLB

_________*(1978a): Language Planning in Kenya; Some Practical Considerations''.* In claessen, Mbaabu and Blackburn

_______*(1996)*: *Language Policy in East Africa,* Nairobi, EAEP

Mnyampala, M. na Chiraghdin*, S.* (1977): *Historia ya Kiswahili.* Nariobi, OUP

Murunga G. R. (1998*):* The Evolution of Mumias settlement into an Urban Centre to Circa 1940, Unpublished M.A Thesis Kenyatta University.

Nasimiyu R. (1980): "The Tradition of Resistance among the Babukusu" Staff Seminar Paper No. 7 Dept. of History, University of Nairobi.

Osogo J. (1966): *A History of Baluhyia. Nairobi, OUP*

_________(1971): The Dismantling of the Wanga Kingdom, During the British Administration (1895-1926)", A Historical Association of Kenya Annual Conference

Ochieng, W.R. (1974): *An Outline History of Nyanza upto 1914, EAEP*

_________(1985): *A History of Kenya, Nairobi, Macmillan*

Onimonde, B. (1985*): An Introduction of Marxist Political Economy London,* Zed Books Ltd

Polome, E (1967): *SwahiliLanguage Handbook. Washington Centre for Applied Linguistics*

Rodney, W. (1972): *How Europe Underdeveloped Africa,* Nairobi, Heinnman

Sakwa M' Sake *G.C.* (1971): "A History of the political organization of Wanga C 1880-1926" M.A. Dissertation University of Nairobi

Senghor, L.S. (1975*):* "The Essence of Language, English and French" Culture No. 2 pp75-98

Shimanyula, J.M. (1978*):* *Elijah Masinde and Din ya Musambwa NRB Trans Africa Publishers*

Staniland M. (1985*): What is political Economy? A Study of Social Theory and Underdevelopment New Haven;* Yale University Press.

Wagner G. (1949): *The Bantu of North Kavirondo with special reference to the Vugusu and Logoli*

Wardhaugh, R. (1987): *Language in competition, Dominance, Diversity and Decline,* Basil Blackwell in Association with Andres Deutch London

Wafula P.W (2000): *Politics and nationalism in colonial Kenya. The Case of the Bukusu of Bungoma District (1894-1963)* Unpublished M.A. Thesis, Kenyatta University

Wafula M. (1997*): "Leadership From the Graves, The Case of the Bukusu Traditional society, In journal of the Institute of African Studies,* University of Nairobi Vol. 2

Were G.S (1967): *History of Abaluhyia of western Kenya. (1500 –1930), Nairobi, EAEP*

Wesonga R. (*1967)*: *The Pre-colonial organization of the Bukusu wandibba (ed) History and culture in Western Kenya: Nairobi, G. S. Were Press*

Whiteley, H. W (1969): *Swahili: The Rise of a National Language,* London Methuen and Co. Ltd.

_________*(1974) (ed): Language in Kenya,* London, *OUP*

Wipper, A. (1977*): Rural Rebels: A Study of Two Protest Movements in Kenya Nairobi, OUP*

Wright, M. (1962*): Swahili Language Policy 1890-1940.* In Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Research

Zeleza, P.7 (1982*):* Kenyan Working Clan during the Colonial Period''. Ph. D Dissertation, Dalhouse University.

## VIAMBATISHO

**(a) Waliohojiwa (mhj)**

1. Amtallah Pwoka (mhj) 2008, mkazi wa Kimilili
2. Cheloti Henry W. (mhj) 2008, mkazi wa Bokoli.
3. Nabangi P. (mhj) 2008, mkazi wa Mateka
4. Naibei H. (mhj) 2008, mkazi wa Kapsokwony.
5. Nabutola J. M (mhj) 2008, mkazi wa Mateka
6. Manya R. (mhj) 2008, mkazi wa Khabukosie Mumias.
7. Wamukoya A. (mhj) 2008, mkazi wa Panyako, Mumias.
8. Nyangweso K. R. (mhj) 2008, mkazi wa Shibale Mumias.

9. Ali Wasiali Juma, 1926, Elukoye, Mumias.
10. Ramadhan Nyangweso Kandwi, 1932, Shibate, Mumias.
11. Peter Makokha Nanjira, 1938, Shibale, Mumias.
12. Athman Khasolo Nakibongochi Khatambi, 1927, Musakasa, Malakisi.
13. William Pwoka Kisiang'ani Amtallah, 1940, Kimilili
14. Jacob Neyole, 1933, Maeni, Kimilili.
15. Hesbon Chesbol Naibei, 1936, Chepkarai, Kapsokwony.
16. Jamini Nandeyoka Amudavi, 1925, Kibinga, Kimilili.
17. Jestomore Masinde Tumbu 1924, Wabukhonyi, Kamukuywa.
18. Stanley Omonya Iliwa, 1928, Kaptola, Mt. Elgon.
19. Juma Bakari, 1939, Musikoma, Bungoma
19. Alfred Kundu Amtallah, 1929, Bokoli.
20. Wanyonyi Manguliechi, 1930, Kibingei, Kimilili.
21. Jestimore Webi, 1916, Lutonyi, Kimilili.
22. Julius Wandati Nandasaba, 1929, Kamtion'gi Mt. Elgon
23. Ramadhani Salim Jabir, 1926, mjini Bungoma.

## HOJAJI KWA AJILI YA MAHOJIANO NYANJANI

**HOJAJI YA 1(Abawanga)**
**Maelezo Mafupi Juu ya Mjibu**

1. Jina lako?.........................................................................
2 Ulizaliwa wapi na lini?..........................................................................
3. Babake Nabongo alikuwa nani? Na alizaliwa lini na wapi ..................
4 Kwa ufupi tueleze Abawanga waliishi wapi kabla ya wao kuingia katika makazi yao ya sasa?
........................................................................................
.......
5 Kwa ufupi tutolee orodha ya watawala au Nabongo tangu Shiundi hadi sasa.........................................................................
.............
6. Nabongo Mumia alitawala eneo lipi kwa ujumla
........................................................................................
................
7 Kwa Muhtasari tueleza mabalozi waliotawala kwa niaba yake na maeneo waliyoyatawala
........................................................................................
8 (i) Je, Nabongo Mumia Alisoma?
........................................................................................
(ii) Ikiwa ndio wapi na lini?..............................................................................................
9 Wageni wa kwanza katika himaya hii walikuwa nani na walikuja lini?
........................................................................................
10. Wakoloni waliingia lini?..........................................................................
11 Kwa muhtasari ni vipi wenyeji walihusiana na
(a) Waswahili/waarabu...........................................................
(b) Wakoloni.............................................................................
12. Je, uhusiano huu ulikuwa wa manufaa? Ikiwa ndio au la. Toa sababu zako
........................................................................................
13. Ni jamii zipi zilizowazunguka? Mlihusianaje na wao?
........................................................................................
14 Taja namna mlivyohusiana na Babukusu.A.Vizuri B.Vibaya.Toa sababu za uhusiano huo.............................................................
15 Nini kilimshawishi Nabongo Mumia kushirikiana na mkoloni katika utawala wake?
........................................................................................
...............
16 Nabongo Mumia alizungumza Kiswahili? ikiwa ndio
(a) Alijifunza wapi?..........................................................................
(b) Alizungumza wakati gani?..........................................................
(c) Kulikuwa ni lazima yeye kutumia lugha ya Kiswahili...........................................................................

(d) Matumizi ya lugha hii kulimsaidia vipi katika utawala wake……………………………………………………………………..

17 Nabongo Mumia alisilimu? Ikiwa ndio eleza umuhimu wa dini ya Kiislamu katika jamii ya Abawanga…………………………………………………………………

(b) Dini hii iliwaathiri ………………….………………………………

18 Je, maingiliano ya jamii jirani yalichangia katika maenezi ya Kiswahili. eleza

(a) (i) Utawala……………………………………………………

(ii) Askari waswahili……………………………………..

(b) Ndoa………………….…………………………………

(c ) Biashara……………………………………………...

(d) Reli……………………………………………………..

(e) Mahakama za kienyeji……………………………………

(f) Miji …………………………………………………

(g) Ajira……………………………………………………

(h) Kushurutiswa?..............................................................................

19 Je, vita vya Lumboka na Chetambe dhidi ya Babukusu vilisaidia vipi utawala wa Mkoloni na Nabongo katika kueneza lugha ya Kiswahili?

……………………………………………………………………………

20 Wewe binafsi, tutolee tajriba yako katika misingi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili…………………………………………………………………

21 Kando na uislamu, Je, dini ya kikristo ilisaidia vipi katika kueneza lugha ya Kiswahili?…………………………………………………………

22 Ni nini chanzo cha majina kama Juma, Baraza, Mjini, Nyongesa?.......................................................................................

***Ahsante kwa Mchango Wako***

**HOJAJI YA II (Ababukusu)**
**Maelezo mafupi ya Mjibu**

1 Jina lako........................................................................................

2 Ulizaliwa wapi lini..........................................................................

3 kwa ufupi tueleza historia ya Babukusu, walipotoka hadi kupelekea wao kupata makazi yao ya sasa...................................................

4 Je, wewe ulisoma wakati wa ukoloni?..........................................................................................

(i) Eleza kwa ufupi uhusiano uliokuwepo kati ya Babukusu kwa upande mmoja na Abawanga na wakoloni upande mwingine..........................................

(ii) Uhusiano wenu ulikuwa vipi?

(a) Mzuri ...............................................................................

(b) Mbaya...............................................................................

Eleza.....................................................................................

(iii) Jina 'Wangisieki' lilitumiwa katika misingi gani?...................................................................................

........

(iv) Nani ndiye aliyetawala Babukusu kwa niaba ya Nabongo Mumia?..................................................................................

(v) Toa maelezo kuhusu utawala wake na vipi uliathiri watawaliwa?

..................................................................................................

5. Waarabu na Waswahili waliingia lini katika eneo hili la Babukusu?

..................................................................................................

6. Eleza kwa ufupi mahusiano yenu na wao na vipi Babukusu waliathirika na maingiliano haya?....................................................................

(i) Kibiashara...........................................................................

(ii) Lugha...............................................................................

7 Je, nyinyi mlipokeaje dini ya kiislamu. Eleza?..................................................................................

8 Eleza jinsi dini hii ilivyotia mizizi katika eneo hili...............................................................................

9 Utawala wa Nabongo Mumia kupitia balozi wake ulitumia lugha ipi katika mawasiliano?

..................................................................................................

(i) Je, kuna lugha zilizo lazimishwa kwenu. Eleza..................................................................................

(ii) Kwa nini mlilazimishiwa lugha hizi?.................................................

10 (i) Ni vipi mahakama za kienyeji ziliendeshwa katika eneo hili?.............................................................................

(ii) Walitumia lugha zipi?.................................................................

11 (i) Wale walioajiriwa kama 'washika kamba' katika mashamba ya wakoloni waliwasiliana vipi na wakoloni? ..............................................

(ii) Ni vipi watawala wa kikoloni hasa DC Wakizungu alivyowasiliana na Babukusu katika mikutano ya hadhara? .....................................

12 (i) Mlilazimishwa kupeleka watoto shuleni? Eleza?.....................

(ii) Ni lugha zipi zilizotumiwa shuleni?...........................................

(iii) Kiswahili kilikuwa na nafasi gani miongoni mwa lugha nyingine?.........................................................................

13 (i) Ajira ya Babukusu katika utawala huu ulitegemea nini? Eleza kwa undani .........................................................................

(ii) Toa mifano ya Babukusu walioteuliwa katika utawala huu katika misingi ya matumizi ya lugha hii.........................................

14 Eleza juu ya maingiliano haya?

(i) Ndoa na wageni hawa kwa jumla..................................

(ii) Mawasiliano na jamii nyingine jirani?...........................................

(iii) Je, uhusiano na hawa wageni uliathiri jamii jirani zilizowazunguka Eleza............................................................

15 Kwa nini baadaye nyinyi mlichoshwa na utawala wa Nabongo Mumia kupitia balozi wake?.............................................................

16 Mbona nyinyi mliitwa na Abawanga kama 'Nywele ngumu'.........................................................................

17 (i) Wewe kama Mzee uliye na tajriba kubwa kwa sababu ya umri yako, kwa maoni yako, utawala wa Nabongo ulichangia katika kueneza Kiswahili katika eneo hili?.............................................................................................

(ii) Toa vigezo vingine ambavyo unaona vilichangia katika kueneza lugha hii ..........................................................................

18 Je, kulikuwa na fahari yoyote ya kuelewa na kukitumia Kiswahili. Eleza?......................................................................... .........

19 Wewe ni Mzee lakini wazungumza Kiswahili sanifu, je, kutokana na tajriba yako, eleza jinsi wewe ulivyoweza kukimudu Kiswahili jinsi hii.........................................................................

20 Linganisha matumizi ya lugha hii wakati wa kikoloni na jinsi ilivyo sasa.....................................................................

21 Dini za Kikristo zilichangia vipi katika kukieneza Kiswahili?....................................................................

22 Majina kama **Nyongesa, Juma, Barasa, Namtala, Mandizini Mjini** yanatokana na athari ya lugha ya Kiswahili? Eleza.......................................................................

*Ahsante na Shukrani kwa Mchango Wako*